

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Thelathini na Tano – Tarehe 23 Mei, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH ISSA – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Taarifa ya Mheshimiwa Spika ambayo inaletwa kwenu kwa mujibu wa Kanuni ya 33(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba tarehe 10 na tarehe 14 Mei 2018, Mheshimiwa Spika alitoa taarifa hapa Bungeni kuhusu Wabunge wenzetu waliochaguliwa na kupata nafasi za uongozi katika Bunge la Afrika (*Pan African Parliament - PAP*) kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu alioelekeza Mheshimiwa Spika wataingia Mheshimiwa mmoja mmoja kwa hivyo niwataje wote wawili halafu nitawaita. Moja Mheshimiwa Stephen Julius Masele Mbunge wa Shinyanga Mjini, alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika akiongoza kwa kura kati ya wagombea wanne wa nafasi hiyo. (*Makofii*)

Mbunge Mwenzetu mwingine ni Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Handeni

Vijijini alichaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Vijana wa Bunge la Afrika akimshinda Mbunge kutoka nchi ya Chad ambaye alikuwa anatetea nafasi yake. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, nimearifiwa kwamba Mheshimiwa Stephen Masele na Mheshimiwa Mboni Mhita wamesharejea nchini na wapo maeneo ya Bunge, kwa hivyo muda si mrefu wataruhusiwa kuingia hapa ndani lakini baada ya kipindi chetu cha maswali na majibu watapewa fursa ya kutusalimu Waheshimiwa Wabunge. (*Makof!*)

Kwa sasa naagiza waingie ndani ya Bunge na wataingia kwa utaratibu wa mmoja mmoja tutaanza na Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita ambaye ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pia ni Mbunge wa Jimbo la Handeni Vijijini, ye ye ni Rais wa Umoja wa Vijana wa Bunge la Afrika.

Mpambe wa Bunge sasa amlete Mheshimiwa Mboni Mhita. (*Makof!*)

*(Hapa Mheshimiwa Mboni M. Mhita aliingia ukumbini)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Mheshimiwa Stephen Julius Masele ambaye ni Mbunge wa Shinyanga Mjini ambaye alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika.

Sasa Mpambe wa Bunge amlete Mheshimiwa Stephen Masele. (*Makof!*)

*(Hapa Mheshimiwa Stephen J. Masele aliingia ukumbini)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge kwa salamu hizo, lakini pia nichukue fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Spika kuwapongeza sana wenzetu hawa wawili kwa heshima kubwa waliyoletea Bunge hili pia kwa heshima kubwa waliyoletea nchi yetu. (*Makof!*)

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Waheshimiwa Wabunge, kwa namna ya kipekee kabisa nichukue fursa hii tena kwa niaba ya Mheshimiwa Spika kuwashukuru sana Wabunge wengine ambao walikuwa pamoja na hawa wenzetu wakati wakifanya kampeni Mheshimiwa Mheshimiwa Asha Abdullah Juma 'Mshua' na Mheshimiwa David Ernest Silinde ahsanteni sana. Mmefanya kazi nzuri, mmeonesha umoja, kwa hivyo nasi kama Bunge tunawashukuru sana kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH ISSA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Taarifa ya mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 (*The Annual Report and Audited Acccounts of Arusha International Conference Center (AICC) for the Financial Year 2016/2017*).

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (K.n.y - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo za Nchi za Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu utekelezaji wa

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; Pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Katibu.

**NDG. ABDALLAH RAMADHANI ISSA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mombasa, sasa aulize swali lake.

Na. 297

**Mpango wa Kuongeza Ajira kwa Wahitimu wa Vytho**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza ajira kwa Watanzania waliohitimu Vyuo bila kujali kada walizosomea ambao mpaka sasa wapo mitaani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mombasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha wahitimu wa vyuo wanapata ajira za kuajiriwa na kujiajiri Serikali imeendelea na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza fursa za ajira kama ifuatavyo:-

(i) Kusimamia utekelezaji wa sera ya uchumi wa viwanda kwa kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji katika

viwanda nchini kupitia sekta binafsi kwa lengo la kutengeneza nafasi nyingi za ajira.

(ii) Utekelezaji wa miradi mikubwa nchini, ikiwemo mradi wa bomba la mafuta, ujenzi wa reli ya kisasa na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa nishati kupitia miradi mbalimbali ambayo yote kwa ujumla itasaidia kupanua wigo wa nafasi za ajira.

(iii) Kutoa elimu kwa vijana kuhusiana na masuala ya ajira kwa lengo la kuongezea ufahamu mpana katika masuala ya ajira na kuongeza uwezo wa kujamini katika kujajiri kupitia sekta mbalimbali za kilimo, ufungaji, uvuvi na ujasiliamali.

(iv) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa programu ya Taifa kukuza ujuzi nchini ambayo ina lengo ya kutoa mafunzo kwa vitendo sehemu ya kazi kwa wahitimu wa vyuo. Mafunzo haya yatawapatia wahitimu wa vyuo ujuzi unaohitajiwa na waajiri, hivyo kuwawezesha kuajirika.

(v) Kuendelea kuwzesha vijana kujajiri kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu kupitia Mfuko Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji programu ya Taifa kukuza ujuzi ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuwzesha vijana kuajirika na kupunguza tofauti ya ujuzi uliopo katika nguvu kazi na mahitaji ya soko la ajira.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa David Ernest Silinde swali la nyongeza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. majibu ya Serikali ni majibu ya siku zote ambayo yameshindwa kutatua tatizo la ajira nchini. Unaweza kuonesha tu mifano midogo kwa mfano, sera ya uchumi na viwanda kwenye bajeti tu peke yake Serikali imeshindwa kupeleka fedha ambayo ingeweza kuwzesha hivyo viwanda

kuanzishwa na wananchi kupata ajira, kipengele cha tano utaona kabisa kwamba inasema kwamba Serikali moja ya mkakati wake ni kuwapa mikopo nafuu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, lakini kwenye bajeti tulioipitisha hapa unakuta Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ni bilioni moja wakati vijana ambao wako mtaani ni wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la kwanza, ni kwa nini Serikali isikubali ama ikashauriana na taasisi za kifedha ili wanafunzi wa Vyuo Vikuu watumie vyeti vyao walivyomalizia elimu ya juu, kama sehemu ya kukopea ili kuwasaidia waweze kujiajiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, ni kwa nini sasa Serikali kupitia Wizara ya Ardhi wasigawe ardhi katika yale maeneo muhimu kabisa bure kwa wanafunzi wote wanaomaliza Vyuo Vikuu ili waweze kujiajiri kwa kufanya hizo kazi na baada ya hapo warejeshe hiyo mikopo yao, kwa nini wasitumie hii mikakati ya muda mfupi ambayo inaweza kuwawezesha hawa watu kupata hiyo ajira au kujiajiri?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, swal lake la kwanza ni kweli katika taasisi za kifedha moja ya masharti ya mtu ye yote kuweza kupata mkopo ni uwasilishaji wa dhamana (*collateral*) ili aweze kufikia uwezo huo wa kupata mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Silinde kwamba asilimia kubwa ya wahitimu wa vyuo vikuu na vyuo vya elimu ya juu bado hawajawa na uwezo wa kuwa na hizo *collateral* ndiyo maana Serikali na kupitia Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi tumeona njia pekee na bora ya kuweza kusaidia kundi hili la vijana kwa kuanzia, kwanza ni kuwahamasisha kukaa katika vikundi, pili ni kuwawezesha kupitia mifuko mbalimbali ya

uwezeshaji ambao chini ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi tuna mifuko takribani 19 ya uwezeshaji inayotoa mikopo na inayotoa ruzuku ambayo ina ukwasi wa kiasi cha shilingi triliuni 1.3 kwa maana ya *liquidity*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa wahitimu wote wa Vyuo Vikuu na Vyuo vya Elimu ya Juu bado wanayo fursa kutumia mifuko yetu hii ambayo ina riba nafuu sana, ambayo pia inaweza ikawasaidia wakabadilisha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mfano ukienda pale Sokoine *University* tuna vijana wana kampuni yao wanaitwa *SUGECO* ambao walihitimu pale wamekaa pamoja ninavyozungumza hivi sasa *SUGECO* wanafanya miradi mikubwa ya kilimo hapa nchini na wameanza kuwasaidia mpaka na vijana wenzao kwa sababu walipitia utaratibu huu, Serikali ikawawezesha na sasa hivi wamefika mbali sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusiana na masuala ya ardhi, Novemba mwaka 2014, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwaita Wakuu wa Mikoa wote hapa Dodoma likatengenezwa Azimio la Wakuu wa Mikoa wote kwenda kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za vijana, juzi Waziri Mkuu amesisitiza hilo jambo na mpaka ninavyozungumza hivi sasa zimeshatengwa takribani hekari 200,000 nchi nzima kwa ajili ya shughuli za vijana ambao maeneo haya tumeyapa jina mahsus i kabisa kwamba ni *Youth Special Economic Zones* (Ukanda Maalum Uchumi kwa ajili ya vijana).

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu ni kwamba niendelee kuwaomba Wakuu wa Mikoa na viongozi wote katika Tawala za Mikoa kwa agizo la Waziri Mkuu watekeleze kwa kutenga maeneo ili vijana wengi zaidi wapate nafasi ya kwenda kufanya shughuli za ufugaji, kilimo na biashara. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuwa ajira ambazo ni rasmi zimekuwa na ukakasi mkubwa kulingana na idadi kubwa ya vijana na Serikali ilishaanzisha mfumo wa kuwasaidia vijana kupitia ajira zisizo rasmi kwa vijana ambao tayari wana ujuzi, nini sasa mkakati wa Serikali kuwarasimisha vijana hawa ili wapate mafunzo na vyeti wanavyoendelea vitakavyowasaidia, hasa wale ambao ni mafundi gereji, mafundi uwashi na mafundi seremala walioko Nyamagana na nchi nzima kwa ujumla?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya kuwatetea vijana hasa vijana wa Jimbo lake la Nyamagana. Pia nimwondoe hofu kwamba chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu tuna mpango wa miaka mitano wa ukuzaji ujuzi kwa vijana ambao lengo lake ni kuwafikia vijana takribani milioni nne na laki nne ifikapo mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango huo moja ya *component* iliyopo tunaita ni *RPL - Recognition of Prior Learning*. Huu ni mfumo wa urasimishaji ujuzi kwa vijana ambao wana ujuzi lakini hawajapitia mfumo rasmi wa mafunzo. Hivi sasa tunao takribani ya vijana 22,000 ambao wameomba kupitia ofisi ya Waziri Mkuu kufanya mafunzo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza hivi sasa vijana 3,448 nchi nzima wamenufaika na nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka huu wa fedha tunaendelea pia kuwachukua vijana hawa kwa ajili ya kuwarasimisha katika ujuzi walionao na kuwapa cheti bila kupitia katika mafunzo maalum ya vyuo vya ufundi stadi. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa James Mbatia swalii la nyongeza.

**MHE JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Tatizo kubwa la ajira ni mfumo wetu wa elimu ambao hauwapi fursa vijana wetu kuwa *creative* na *innovative*, yaani unakuwa na mfumo wa elimu ambao unaangalia miaka 50 unataka uwe na Taifa la namna gani badala ya elimu yetu ya *copy and paste*. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuhakikisha mitaala yake inaandaa Taifa ambalo linakuwa *innovative and creative* badala ya *copy and paste*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, alichokisema Mheshimiwa Mbunge pia kimeripotiwa na taarifa mbalimbali, moja kati ya changamoto iliyopo ni namna ambavyo tunawenza tukawa tuna vijana wahitimu wenye ujuzi ambao utawapa sifa za kuajiriwa katika soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama ofisi ya Waziri kupitia mpango wa ukuzaji ujuzi, moja kati ya eneo ambalo tumelipa kipaumbele ni hilo. Mwaka jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua miongozo kwa ajili ya kuhakikisha vijana wetu wahitimu wa Vyuo Vikuu wanapata mafunzo ya vitendo ili waongeze sifa ya ziada kwenda kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi katika msingi wa swalii lake ni kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Wizara ya Elimu tunafanya kazi hii kwa pamoja ili kuona namna bora kuja na mitaala ambayo itamfanya kijana wa Kitanzania akihitimu elimu yake awe na sifa za kuajiriwa ili apate nafasi ya kuajirika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba kuna hoja ya kuhakikisha vijana wetu wanakuwa wabunifu ili watakapomaliza vyuo kama hawajapata ajira rasmi waweze kujiajiri. Kwa sasa Wizara ya Elimu ina mkakati mkubwa sana kuhakikisha kwamba tunakuza stadi za kazi ili vijana wanapohitimu wasiwe wanaangalia kuajiriwa tu vilevile waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa sasa inatekeleza mradi unaitwa *ESPJ - Education and Skills for Productive Jobs*, mradi ambao unafadhiiliwa na Wadau wa Maendeleo kwa dola milioni 100. Moja kati ya malengo yake ambalo ni kubwa, ni kuhakikisha kwamba kwenye shule zetu, vyuo vyetu vijana wanafundishwa stadi za kazi ili wakitoka hata kama hawajapata ajira rasmi waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitumie fursa hii kuendelea kusisitiza kwamba zamani tunapoenda kusoma shuleni tunafikiria kwenda kuajiriwa, kwa sasa *focus* tokea mwanzo tunataka watu wajue kwamba ajira ni pamoja na kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Catherine Magige, swali fupi.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa waajiri wengi nawapotoa nafasi za ajira, wanahitaji waombaji ambao wanaomba wawe na *experience* na wanachuo wengi wanaomaliza vyuo wanakuwa hawana uzoefu. Je, Serikali ina mpango gani kuwasaidia wanavyuo wanapotoka vyuoni waajiriwe bila kuulizwa *experience*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu amesimama. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, siyo kazi zote zinahitaji uwe umepata uzoefu. Kuna kazi ambazo zinatangazwa ambazo wanachukuliwa wanafunzi waliotoka vyuoni moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kama nilivyosema lengo la kuanzisha mfumo wa elimu ambao vilevile unafundisha stadi za kazi ni kuhakikisha kwamba hata tunapokuwa mashulenii tayari kuna uzoefu ambao tumekuwa tumeupata. Ndiyo maana hata Serikali kwa sasa inawekeza sana kwenye elimu ya ufundi ili wanafunzi wanapokuwa mashulenii na vyuoni wawe tayari wameshaanza kufanya *practicals* ili wakienda kwenye ajira kwamba wawe tayari wanawenza kuajiriwa. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaenda sasa kwenye Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Nassor Suleiman Omar, Mbunge wa Ziwani, sasa aulize swalii lake.

Na. 298

**Athari za Uhakiki wa Vyeti Feki**

**MHE. NASSOR SULEIMAN OMARY** aliuliza:-

Uhakiki wa vyeti feki umeathiri wafanyakazi wengi na wengine wamepoteza ajira zao:-

Je, ni wafanyakazi wangapi wamepoteza ajira zao sekta ya elimu pekee?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Nassor Suleiman Omar, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 na 2017/2018, Serikali ilifanya uhakiki wa vyeti vya watumishi wa umma ili kubaini waliokuwa na vyeti halali na waliokuwa na vyeti vya kughushi. Katika uhakiki huo, jumla ya Walimu 3,655 walibainika kuwa na vyeti vya kughushi, hivyo walipoteza sifa za kuendelea kuwa watumishi wa umma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nassor Omar, swali la nyongeza.

**MHE. NASSOR SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Serikali ilitoa kauli kwa wale wote walioathirika na zoezi hili kimakosa; Je Serikali imeshawarejesha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuna wale ambao walioathirika kimakosa na wako karibu na kustaafu; je Serikali ina kauli gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baada ya zoezi hili yalitokea manung'uniko na vilevile zilitokea rufaa mbalimbali za watumishi ambao walidhani kwamba wameonewa. Serikali ilifanya uchambuzi wa kina, wale ambao walionekana kwamba kulikuwa na makosa katika mchakato huo wamesharejeshwa kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameuliza swali lingine kwamba wale ambao walikuwa wanakaribia kustaafu Serikali imewaangalia namna gani? Ukweli ni kwamba kwa makosa ambayo walikuwa wameyafanya walitakiwa wapelekwe Mahakamani, lakini Serikali ilisema tuwasamehe mambo ya kuapeleka mahakamani kwa makosa ya kughushi na wao wasilet madai mengine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Madini.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kwanza kupongeza majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini napenda tu kuongezea kuhusiana na idadi ya waliokata rufaa na kurudishwa kazini, jumla ni watumishi 1,907.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, zalio la vyeti feki ni Chama cha Mapinduzi na Serikali yake, Mheshimiwa Rais akiwa ni sehemu ya CCM kwa kipindi chote hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba Walimu ama Watumishi wengi walanza na cheti cha mtu wakaenda wakasomea taaluma, wakafaulu taaluma zao, wakaenda kulitumikia Taifa hili kwa miaka mingi sana. Serikali ya watu ni Serikali yenye ubinadamu. Sasa nauliza, hivi ni kweli Serikali ya CCM inadhani ni sahihi kwa watu ambao wametumikia hili Taifa kwa miaka 20, wengine mpaka miaka 40 wengine miaka 30, waondoke hivi hivi bila hata kupata kifuta jasho, wanadhani ni sahihi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge swali lako umesauliza na umeshaeleweka. Mheshimiwa Waziri wa Madini majibu.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri dada yangu ama mdogo wangu naye ni Mwanasheria. *You cannot benefit from your own wrong*, suala hili lilikuwa ni jinai, huwezi ukarufaika hata kama uliweza ku-penetrate katika mfumo ikafikia hapo na ndiyo maana Mheshimiwa Rais aliweza kutoa *amnesty* hii haikuweza kutoka bure.

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Halima aweze kuelewa suala hili halijazalishwa tu hivi na Serikali ya CCM ni *Criminal Offence* na ilikuwa ni lazima kufanya hivyo. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, msizipige sana hizo meza nawaona mkiwa mmesimama. Mheshimiwa Juma Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA KOMBO HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu la msingi amesema kwamba jumla ya Walimu 3,655 walipoteza kazi baada ya uhakiki na kugundulika na vyeti feki. Nataka kujua tu katika mwaka 2016/2017 na 2017/2018 Serikali kama ilipoteza Walimu hawa; je, hadi sasa imeajiri Walimu wangapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya zoezi hilo kukamilika Serikali katika miaka hii miwili 2016/2017 na 2017/2018 imeajiri jumla ya Walimu 6,495. Kati ya hao Walimu wa shule za sekondari wa masomo ya sayansi na hisabati ni 3,728 na Walimu wa shule za msingi ni 2,767. Idadi hiyo ni zaidi ya walioachishwa kazi ni kwa sababu ya kuwa na vyeti vya kughushi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 299

**Huduma ya Maji Sekondari ya Masengwa**

**MHE. AZZA H. HAMAD** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupeleka maji katika Sekondari ya Masengwa?

## **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza ahadi yake ya kupeleka maji kwenye Shule ya Sekondari Masengwa. Serikali imeandaa mradi wa kutoa maji Kijiji cha Bugweto Manispaa ya Shinyanga kwenda katika Kijiji cha Masengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tararibu za kumpata Mkandarasi atakayetekeliza mradi wa kupeleka maji katika Kijiji cha Masengwa zimekamilika. Utekelezaji wa mradi huo utaanza katika mwaka wa fedha 2018/2019. Matarajio ni kwamba mradi huu utakapokamillika utawanufaisha wakazi wa Kijiji cha Masengwa ikiwemo na Shule ya Sekondari Masengwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, swalii la nyongeza.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Mradi huu wa maji ni ahadi ya toka mwaka 2006 ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais Mstaafu hivyo imekuwa ni ahadi ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, je, Wizara ya Maji ipo tayari sasa kuondoa vikwazo vyote vilivyopo Wizara ya Maji na kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha mradi huu unaanza mara moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, kumekuwa na hofu kubwa kwa wananchi wangu wa Mji Mdogo wa Tinde kutokana na kwamba mradi wa maji wa Ziwa Victoria bomba kubwa linapita mbali sana na Mji Mdogo wa Tinde, hivyo kuwa na hofu kubwa kwamba mradi huu

hautawezekana kufika kwa wananchi wa Tinde. Je, Wizara ya Maji imefikia wapi kuwaondoa hofu wananchi wa Tinde kuhakikisha kwamba wanapata maji safi na salama katika mradi huu wa mkubwa wa maji ya Ziwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Azza kwa jinsi ambavyo anawapenda wananchi wa Shinyanga na jinsi anavyowatetea katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza la Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kabisa kwamba miradi hii ilianza bajeti ya mwaka 2006/2007 na Mheshimiwa Mbunge naomba tu akumbuke ndipo tulioanza ile *program* ya maendeleo ya sekta ya maji, tukaweka kwamba tutajenga miradi 1,810. Tumeshakamilisha miradi 1,468, bado miradi 366 na mradi wake ukiwa ni mmojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, umechelewa kwa sababu usanifu ulichelewa, lakini kwa sasa tunamhakikishia kwamba hakuna vikwazo vya aina yoyote, tunatekeleza kwa mujibu wa sheria. Mradi wowote baada ya usanifu, baada ya manunuzi ili kuepuka upotevu wa fedha lazima tuupeleke kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali akaufanyie *vetting*, tusaini, ndiyo tuanje utekelezaji. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba mradi utatekelezwa bila ya wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, ni kweli bomba la *KASHIWASA* limepita mbali kidogo mbali na ule Mji wa Tinde, nimemwagiza Mhandisi Mshauri anayesimamia huu mradi wa Tabora na tayari ameshabaini vijiji vitakavyopelekewa maji ukiwemo Mji wote Tinde na vitongoji vyake na amekamilisha utaratibu wa awali sasa hivi tunaingia kwenye usanifu wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati tunaendelea na utekelezaji wa

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

mradi wa Tabora basi wakati unakamilika na Tinde yote itakuwa imeshapata maji. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba niiulize Serikali ni lini itapeleka maji kwenye Kata ya Mjele ambayo ni ahadi ya muda mrefu ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayofanya na nimeshafika hadi Mjele. Namwomba sana Mhandisi wa Maji wa Jimbo la Mbeya Vijijini asilale ili kuhakikisha wananchi wale wanapata maji safi, salama na ya kuwatosheleza. Jambo la msingi sisi kama Wizara *a-raise certificate* tuko tayari kulipa kwa wakati ili wananchi waweze kupata maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri naomba uwatazame hawa Wabunge, sitawaruhusu kuuliza maswali wana mambo ya maji katika Majimbo yao.

Tutaendelea na Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, sasa aulize swali lake.

Na. 300

**Mradi wa Maji toka Mto Kalumbaleza**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Kutokana na tatizo kubwa la ukosefu wa maji katika Mji Mdogo wa Muze Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga

ilipitisha mpango wake wa kuondokana na tatizo hilo kwa kuanzisha mradi mkubwa wa kuchukua maji toka Mto Kalumbaleza na kusambaza katika Vijiji vya Muze, Mlia, Mnazi Mmoja Asilia, Ilanga, Mbwi Kalakala, Isangwa na Uzia:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili kutekeleza mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Jimbo la Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutenga fedha za utekelezaji wa miradi ya maji ili kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma ya maji. Kwa sasa Mtaalam Mshauri anaendelea na kazi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi wa maji wa Muze *Group* ili utekelezaji wake uweze kufanyika katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga kiasi cha Sh.500,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Muze *Group*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ignas Malocha, swali la nyongeza.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA.** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Kwanza nimpongeze Naibu Waziri na Waziri wake kwa utendaji wa kazi, lakinii ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, mradi huu wa Muze *Group* unategemewa kupeleka maji katika vijiji 10 vyenye wakazi 40,000 ambavyo ni Kijiji cha Kalumbaleza A, B, Muze, Mbwi, Mlia, Mnazi mmoja Asilia, Ilanga Kalakala, Izia na Isangwa. Maeneo haya hukumbwa na kipindupindu kila mwaka kutokanana na shida ya maji, mwaka huu wananchi wapatao 605 waliugua kipindupindu, katika hao wananchi 15 walikufa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuharakisha ujenzi wa mradi huu ili kunusuru vifo kwa wananchi?

Swali la pili, kwa vile Mtaalam Mshauri wa mradi huu alishaanza kazi na amesha- *raise certificate* Wizara ya Maji; Je, ni lini watamlipa fedha zake haraka ili mradi huu uweze kuanza mapema? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ya kipekee anavyowatetea wananchi wake. Nataka niwahakikishie kwamba maji ni uhai, Wizara ya Maji hatutakuwa sehemu ya kupoteza uhai wa wananchi wake. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutakuwa sehemu ya kusimamia mradi huu ili uweze kutekelezeka kwa wakati wananchi wake waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya Bunge cha saa saba tukutane ili twende kuhakikisha Mkandarasi huyu analipwa kwa wakati ili mradi usikwame na wananchi waweze kupata maji. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naamini utaweza kuonana na hawa Wabunge wote, hebu waangalie vizuri wamesimama. Wabunge hawa wana miradi imekwama katika maeneo yao.

Mheshimiwa Deo Ngalawa, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Mji wa Makambako ni Mji mkubwa na ni Mji ambao una tatizo kubwa sana la maji. Baadhi ya wananchi wanashindwa kujenga viwanda kwa sababu ya uhaba wa maji. Kuna miradi 17 ya fedha kutoka Serikali ya India. Serikali iniambie hapa je, ni lini sasa miradi hii ambayo mmojawapo ni ya Mji wa Makambako utaanza ili wananchi wa Makambako waweze kunufaika na wajipange kwa ajili ya kujenga viwanda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kabla hujajibu hilo, nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Deo Ngawala, kwa hiyo inabidi Mheshimiwa Deo Ngalawa aulize swalii halafu utajajibu yote mawili kwa pamoja.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii. Tatizo la maji katika Wilaya ya Ludewa limekuwa ni la kudumu na ikizingatiwa kwamba Wilaya ya Ludewa ina vyanzo vya maji vingi sana. Je, Serikali inajipangaje katika kuhakikisha kwamba Ludewa inapata maji ya uhakika hususan Ludewa Mjini na Mavanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mbunge wa Makambako pamoja na Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Mheshimiwa Mbunge wa Makambako, kwanza kabisa tunaishukuru Serikali kwamba mkataba wa kifedha kati ya Serikali ya India na Tanzania umeshasainiwa tayari. Pili, kulingana na masharti ya mkataba huo, Serikali ya India imeshaleta Wahandisi Washauri tayari, wengi ambao sasa hivi tutafanya manunuzi kuititia kwenye hilo *group*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba shughuli hii inakwenda kwa kasi sana na matarajio yake ni kwamba kabla ya mwaka huu tulionao 2018 haujafika Desemba, tunataka tuhakikishe kwamba Wakandarasi wako *site* na wanaanza utekelezaji wa miradi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalii la Mheshimiwa Mbunge wa Ludewa. Mheshimiwa Mbunge yeye mwenyewe ni shahidi kwamba nilishaelekeza mamlaka yangu ya maji ya Iringa na wanaendelea kutekeleza miradi katika Jimbo

lake na mwaka huu tumetenga fedha. Kwa hiyo, tutaendelea kutekeleza pamoja na pale Mjini ambapo mimi mwenyewe nilipatembelea, tutahakikisha kwamba tunawapatia maji safi na salama wananchi wake. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rarya, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

Na. 301

**Hitaji la Mahakama ya Mwanzo na Watumishi  
Wilaya ya Rarya**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE (K.n.y. LAMECK O. AIRO)**  
aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Rarya ilianzishwa mwaka 2007 na ina ukubwa wa kilometa za mraba 9,345 na idadi ya watu wapatao 400,000, lakini inakabiliwa na tatizo la uhaba wa watumishi katika Mahakama za Mwanzo za Kineri, Ryagoro, Obilinju na Shirati; hadi sasa Wilaya ya Rarya inatumia Mahakama ya Wilaya ya Tarime hali inayosababisha kesi kucheleva kusikilizwa kwa wakati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama ya Wilaya kwenye Jimbo la Rarya?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okambo Airo, Mbunge wa Rarya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa Mahakama wa kujenga na kukarabati majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali, Mahakama ya Wilaya ya Rarya imepangiwa kujengwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nadhani sasa umefika wakati kwa Serikali kuamua kuangalia haya mambo ya majengo ya Mahakama kwa sababu duniani kote haki ndiyo inajaaliwa, lakini kumekuwa tu na mazoea ya kujibu kwa sababu nimemuona Mheshimiwa Lameck Airo akiwa na hoja hii miaka mitatu iliyopita na ni miaka 11 sasa toka Wilaya hii ianzishwe. Sasa uhakika ni upi? Kila mwaka anauliza wanasema mwaka unaofuata, kila mwaka anauliza anaambiwa mwaka unaofuata. Sasa Waziri atuthibitishie kwamba ni kweli bajeti inayokuja hiyo Mahakama itajengwa kwa Wilaya ya Rarya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Jimbo la Bunda kuna Mahakama ya Nyamswa, imekuwepo muda mrefu sana hiyo Mahakama ilijengwa na Mtemi Makongoro miaka hiyo mpaka leo, ni lini sasa Serikali itaenda kukarabati ile Mahakama na kuifanya iwe ya kisasa kwa ajili ya kusaidia watu wa Jimbo la Bunda? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mbunge aliyeuliza swali kwamba Mahakama hiyo itajengwa katika mwaka huo wa 2019/2020 na siyo Mahakama hiyo tu bali Mahakama zote ambazo zimepangwa kujengwa katika mwaka huo kwa Mkoa wa Arusha ikiwa ni Arumeru na Ngorongoro; kwa Mkoa wa Dodoma ikiwa Bahi; kwa Mkoa wa Geita ikiwa Geita; kwa Mkoa wa Kagera ikiwa ni Muleba, Bukoba, Ngara, kwa Mkoa wa katavi ikiwa ni Mpanda na Tanganyika; na kwa Mkoa wa Kigoma ikiwa ni Uvinza na Buhigwe.

Vile vile kwa Mkoa wa Kilimanjaro ikiwa ni Same; kwa Mkoa wa Lindi ikiwa ni Nachingwea; kwa Mkoa wa Manyara, Babati, Hanang', kwa Mkoa wa Mara ni Rarya na Butiama;

kwa Mkoa wa Mbeya itakuwa Rungwe; kwa Mkoa wa Morogoro Gairo, Mvomero, Morogoro, Malinyi; kwa Mkoa wa Mtwara, Newala, Mtwara, Tandahimba; kwa Mkoa wa Mwanza, Kwigwa; zote hizo ni Mahakama ambazo zitajengwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na fedha yake inatokana na mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo vyanzo vya fedha vipo na bado zipo Wilaya nyingine nyingi ambazo Mahakama zitajengwa mwaka huu wa 2019/2020. Kwa hiyo ningependa nimhakikishie hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mahakama ya Nyamswa, kabla ya Bunge hili kuanza nilifanya ziara ya Mkoa wa Mara na mahali ambapo nilipita pia ni Nyamswa. Hili ni jengo la zamani ambalo linahitaji kukarabatiwa na hilo litatafutiwa fedha katika mpango wa dharura, itakapopatikana ili Mahakama hiyo ya Nyamswa iweze kukarabatiwa. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Wilaya ya Tanganyika ni Wilaya ambayo haina Mahakama ya Wilaya, sambamba na Mahakama za Mwanzo ni zile ambazo zimechakaa na hazina watumishi wa kuzifanya kazi hizo Mahakama. Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa Mahakama za Mwanzo sambamba na Mahakama ya Wilaya na ujenzi wa Mahakama ya Wilaya? Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, maswali mengi katika swali moja. Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Wilaya katika Wilaya ya Tanganyika itajengwa mwaka

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

2019/2020 na kama nilivyosema fedha imepatikana kwa hiyo tuna uhakika kwamba Mahakama hiyo itajengwa kwa kipindi hicho huko Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watumishi wa Mahakama, ningependa kusema kwamba upo upungufu wa watumishi wa Mahakama ya Mwanzo 3,000 kwa sababu sasa hivi wako watumishi 6,000 na wanahitajika watumishi wengine 3,000. Wizara inaendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupata vibali vya ajira. Mara vibali hivyo vitakapopatikana mionganoni mwa Mahakama ambazo zitapewa kipaumbele ni Mahakama za Mwanzo naamini pia zitagusa Wilaya ya Tanganyika. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini, sasa aulize swali lake.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijauliza swali, kwanza naomba nitoe neno la shukrani kwa Spika wa Bunge, Katibu wa Bunge pamoja na Kamati ile yote ya Wahasibu na Wabunge wenzangu hasa Wabunge wa Mkoa wa Tanga kwa mchango mkubwa ambao wamenisaidia katika kuuguza familia yangu pale Muhimbia. Mungu awabariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya maneno machache, naomba swali langu sasa lipate majibu.

Na. 302

**Kufungua Mahakama ya Mwanzo Magoma  
Korogwe Vijijini**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI** aliuliza:-

Katika Kata ya Magoma, Korogwe Vijijini kumejengwa Mahakama ya Mwanzo ya Kisasa, lakini toka ijengwe imefika miaka saba sasa haijafunguliwa:-

Je, ni lini Serikali itafungua Mahakama hiyo ili wananchi waachane na usumbufu wa kufuata huduma za Mahakama Korogwe?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Mwanzo ya Magoma ilijengwa muda mrefu kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge wa Korogwe, lakini jengo lile halikukamilika. Mahakama ilijoengwa ni ya kisasa, iliyohusisha ujenzi wa jengo la Mahakama, nyumba ya Hakimu na kantini.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo haya yalisimama kwa muda mrefu kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo ukosefu wa fedha. Mradi huu sasa umefufuliwa na unatekelezwa na SUMA JKT, chini ya usimamizi wa TBA Mkoa wa Tanga na unatarajiwa kukamilika na kuanza kutumika kabla ya Julai mwaka huu 2018.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Ngonyani, swalii la nyongeza.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Profesa mwenzangu. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza, kwa kuwa Tarafa ya Magoma ina Kata Nane na katika Kata hizi ina Mahakama moja tu ya Mwanzo ambayo ni hiyo ya Mashewa na huu mradi umechukua muda mrefu bila kufunguliwa. Nataka Serikali iniambie ni tarehe ngapi Mahakama hii itakuwa imefunguliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, maneno anayoelezwa hapo Mheshimiwa Waziri, naomba kama kutakuwa na uwezekano aende. Hayo anayoambiwa kwenye karatasi

yanalingana na jinsi Mahakama yenyewe inavyotengenezwa kule nilipo? Nitaomba twende wote ili akahakishe, aone kwamba imechukua muda mrefu, wanafanya kazi bila kudhibiti na tunapata usumbufu sana kwa walalamikaji na washtakiwa kwenda zaidi ya kilometra 35. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Kata ile inahitaji Mahakama zaidi na naamini katika mpango utakaofuata wa maendeleo wa miaka 10 wa Mahakama baada ya huu unaoisha 2020 kukamilika, tutatazama tena maeneo ambayo Kata zao ni kubwa na Mahakama ni chache ili katika mpango huo wa awamu ya pili wa ujenzi wa Mahakama nchini maeneo hayo yaweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili la kutembelea eneo la Mashewa ili kujiona jinsi Mahakama hiyo inavyojengwa, niko radhi kufika huko na sina wasiwasi Profesa kwa sababu na mimi mjomba wangu ni fundi kama wewe, kwa hiyo nitafika na kuondoka salama. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda, kwa hiyo tutaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Swalii la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Kibamba, Mheshimiwa Julius Kalanga aulize kwa niaba yake.

Na. 303

### **Ujenzi wa Barabara za Pete na Mchepuo**

**MHE. JULIUS K. LAIZER (K.n.y. MHE. JOHN J. MNYIKA)**  
aliuliza:-

Barabara za pete (*ring roads*) na barabara za mchepuo (*feeder roads*) ni muhimu katika kupunguza msongamano na matatizo ya miundombinu kwa wananchi:-

(a) Je, Serikali itakamilisha lini ujenzi wa barabara hizo zilizoanza kujengwa katika Jimbo la Kibamba?

(b) Je, Serikali itaanza lini ujenzi wa barabara ambazo zimetajwa katika mipango ya Serikali lakini hazijaanza kujengwa mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John John Mnyika, Mbunge wa Kibamba, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mkakati wa kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, Serikali kuitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano mnemo mwaka 2010 ilianza kutekeleza ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara za pete (*ring roads*) na barabara za mchepuo (*bypass*).

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zilizoingizwa kwenye mpango huo ambazo ziko kwenye Jimbo la Kibamba na hatua za utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali ni kama ifuatavyo:-

Barabara ya Bunju B – Mpigi Magohe – Victoria – Kifuru hadi Pugu yenye urefu wa kilometra 33.7 (*outer ring road*); barabara ya Mbezi – Msigani – Malambamawili – Kifuru – Kinyerezi – Banana (sehemu ya Kinyerezi – Mbezi – Malambamawili – Kifuru) yenye urefu wa kilometra 10; na barabara ya Tegeta – Kibaoni – Wazo Hill -Goba – Mbezi/ Morogoro Road yenye urefu wa kilometra 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambazo ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika ni sehemu ya barabara ya Mbezi – Msigani – Malambamawili – Kifuru – Kinyerezi – Banana kuanzia Msigani – Kifuru yenye urefu wa kilometra nane

na barabara ya Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba Mbezi/Morogoro road sehemu ya Goba Mbezi/Morogoro Road yenye urefu wa kilometra saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambazo ujenzi wa kiwango cha lami unaendelea ni barabara inayoanzia Msigani mpaka Mbezi yenye urefu wa kilometra mbili zikiwemo barabara za kutoka na kuingia kwenye kituo cha mabasi ya Mbezi na barabara nyingine ni Goba – Madale yenye urefu wa kilometra tano. Barabara ambayo usanifu wake bado unaendelea ni barabara ya pete (*outer ring road*) ya Bunju B – Mpiji Magohe – Victoria – Kifuru hadi Pugu yenye urefu wa kilometra 33.7.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Halima Mdee kwa niaba ya Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer ambaye pia ameuliza kwa niaba ya Mheshimiwa Mnyika. (*Makofii/Kicheko*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Mheshimiwa Kalanga na Mheshimiwa John Mnyika, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; moja kati ya barabara muhimu za *ring road* ama barabara za pete ambazo zimeainishwa hapa ni barabara ya Goba kwenda Makongo – Chuo cha Ardhi, barabara hii kama ambavyo mnafahamu kwa siku yanapita magari zaidi ya laki moja (100,000) lakini vilevile ni barabara yenye umuhimu mkubwa sana pale ambapo tutakuwa tunajenga *interchange* ya pale Ubungo kwa sababu magari mengi yatahitaji barabara za kuweza kuchopoka kwenda Mbezi na hatimaye Morogoro Road.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nipate majibu ya Serikali, kwa sasa zimejengwa kilometra nne tu halafu zinaonekana zime-stuck hakuna kitu kinachoendelea. Naomba majibu ya Serikali ni lini uendelezaji wa barabara kwa kilometra tano zilizobaki utafanyika kwa kiwango cha lami? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, maelezo ama majibu ya Mheshimiwa Waziri yanaainisha kama vile barabara ya Goba – Madale – Tegeta Kibaoni imekamilika, lakini ukweli ni kwamba barabara iliyokamilika ni kipande cha Goba, kipande cha Goba – Madale ndiyo kinajengwa sasa hivi kwa kilometra tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri ambayo inaanza sasa kufanywa, swali langu ni dogo, kiwanda cha Twiga kimekuwa kinafanya matumizi mabovu ya hii barabara kwa kupaki magari yake barabarani, hali ambayo inahatarisha uhai wa barabara, lakini inahatarisha uhai wa wananchi wetu. Kama Serikali ya mtaa imejaribu kuingilia kati, Serikali ya Kata imeingilia kati, Mbunge nimeingilia kati, lakini kiwanda kinaonekana ni kiburi. Nataka *commitment* ya Serikali kwamba itafuatilia kiwandani ili matumizi ya barabara yaachwe kwa ajili ya barabara na isihatarishe uhai wa wananchi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nashukuru kuona kuwa, Mheshimiwa Halima Mdee anatambua juhudii kubwa ambazo Serikali hii inazifanya katika kujenga barabara na kuweza kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyopitisha kwenye bajeti barabara zinazohusiana na kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam ziko kama kilometra 156, baadhi ya barabara zimekamilika lakini baadhi ya barabara juhudii zinaendelea kuweza kukamilisha. Kwa hiyo, niseme tu kwamba Mheshimiwa Halima, hii barabara ambayo unaizungumzia barabara ambayo inapita Madale kwamba kuna kipande cha kilometra tano kinaendelea kukamilishwa, ni mpango wetu na hata ukiangalia kwenye bajeti ni kuweza kuikamilisha barabara hii nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwombe tu avute subira na wananchi wavute subira, tunafahamu umuhimu na uharaka wa kutengeneza barabara katika Jiji la Dar es Salaam kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko awamu nyingi zitakuja, kila awamu ikikamilika ni fursa ya kuanza awamu nyingine ili hatimaye tumalize kabisa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza juu ya barabara kipande ambacho unasema kilometra tano kutoka Makongo Juu kwenda Chuo cha Ardhi, najua tunafanya juhudhi ya kumaliza tatizo la *compensation* eneo lile ili wananchi waweze kupisha barabara ikamilike. Niseme tu kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na watumiaji wa barabara kwamba, ni mkakati wa Serikali kwamba wakati wa ujenzi wa *interchange* ya Ubungo barabara hiyo anayoitaja Mheshimiwa Mbunge ni muhimu sana. Ni muhimu sana kuhakikisha kwamba tunapunguza msongamano kipindi chote cha ujenzi wa barabara pale Ubungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo Serikali tunaona uko umuhimu na kwa haraka sana kukamilisha barabara hii. Kwa hiyo avute tu subira, barabara hii tutaitengeneza pamoja na barabara zingine. Iko mipango mingi tu mizuri katika kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe tu Mheshimiwa Halima, akisoma pia kwenye hotuba ya bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri aliwasilisha hapa ukurasa wa 17 hadi wa 18 na ukurasa wa 25 ataona mambo mazuri yaliyoko huku. Angepitia tu ili aone namna tulivyojipanga kuhakikisha kwamba Dar es Salaam inabakia vizuri barabara zinakuwa zinawasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiwanda cha Twiga Cement kupaki magari, naomba nilichukue hilo, lakini niseme

tu kwamba tunao mpango kabambe wa kuwashughulikia wanaotumia barabara vibaya katika Jiji la Dar es Salaam, pia tunafanya *patro/na* kwenda na mizani ile ya kuhama.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe tu watumiaji wa magari, siyo hao wa barabara hii lakini na maeneo mbalimbali ambao na wengine wanatumia wakati wa usiku. Tumeshalionia hilo tunalifanyia kazi ili kuhakikisha kwanza magari yanaegeshwa vizuri kwa ajili ya usalama, lakini pia kwa ajili ya kufanya barabara zetu zisiweze kuharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili nimelichukua nakushukuru tutaendelea kulfanyia kazi ili tuweze kuondosha hili tatizo. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula, swalilala nyongeza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Hali ya ahadi kwa barabara za Dar es Salaam inafanana sana na ahadi ya barabara ya Tanga - Mabokweni - Maramba - Bombo Mtoni - Kitivo hadi Same ambapo barabara hii ilikuwa kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami kuititia fedha za *MCC II*, lakini mradi ule ukashindikana. Sasa ni lini Serikali itaanza usanifu wa barabara hii ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, najua suala la barabara hii ya Tanga - Maramba Mawili-Bombo Mtoni kupanda mpaka kwenda upande mwingine tunakwenda Same na upande mwingine tunapita Lushoto, barabara hii nimeipita nimeionta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ilikuwa kwenye mpango hauku-*mature* nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge

na mara nyingi nampa *feedback* kwamba tunaitazama sasa ili tuone namna bora ya kuweza kuitengeneza barabara hii muhimu. Wananchi wa Maramba kwa kweli barabara hii nilipita nilliona wana shauku kubwa sana ya barabara hii. Mheshimiwa Mbunge naomba avute subira na nitaendelea kumpa mrejesho namna tunavyoweza kujipanga kuitengeneza barabara hii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 304

**Waendesha Bodaboda Kuwapa Wanafunzi Mimba**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Imebainika kuwa baadhi ya Madereva wa bodaboda wamekuwa wakifanya ukatili kwa kufanya ubakaji, ulawiti na kuwapa baadhi ya wanafunzi mimba:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti hali hii hasa kwa wale bodaboda wanaowahadaa baadhi ya wanafunzi wa kike?

(b) Je, ni wanafunzi wangapi walioripotiwa kupewa mimba na waendesha bodaboda katika kipindi cha miaka mitatu (3) iliyopita?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa kuna wanaume wanaojihusisha na vitendo vya ubakaji,

ulawiti na kuwapa mimba baadhi ya wanafunzi. Baadhi ya Madereva wa bodaboda wameripotiwa kujihusisha na vitendo hivyo viovu, vitendo hivyo hutokana na tabia mbaya, vishawishi na changamoto za mazingira kama vile umbali kutoka nyumbani kwenda mashulenii kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na vitendo hivyo mwaka 2016 Serikali ilifanya Marekebisho ya Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 ambapo mtu atakayepatikana na hatia ya kumpa mimba mwanafunzi akihukumiwa hufungwa miaka 30. Aidha, Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16 inabainisha Hukumu ya kifungo cha maisha kwa mtu atakayetenda kosa la kubaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sheria hizo Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kudhibiti vitendo hivyo kwa kutoa huduma za ushauri na unasihi ambapo shule zimeelekezwa kuwa na Walimu washauri wa kike na kiume. Hivyo, mwongozo wa ushauri na unasihi shulenii na vyuoni umeandaliwa. Vilevile Serikali kwa kushirikiana na wadau inaendelea na ujenzi wa mabweni, *hostel* na shule katika maeneo ambayo wanafunzi wanalazimika kutembea umbali mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi hupewa mimba na wanaume mbalimbali, wanaweza kuwa ni wakulima, wafugaji, wafanyakazi au wafanyabiashara wakiwemo Madereva bodaboda. Hata hivyo takwimu za wanafunzi waliyopata mimba hazikokotolewi kwa kuanisha makundi ya wanaume waliowapa ujauzito. Hivyo ni vigumu kupata idadi ya wanafunzi waliyopewa mimba na madereva wa bodaboda.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali

mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa suala la ubakaji na ulawiti linazidi kuongezeka; je Serikali haioni imefika wakati wa kuwa na *hotline* maalum ya kutoa taarifa za ukatili kwa wale ambao wanapata tatizo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali imeweka mpango mzuri wa kuwa na dawati la jinsia. Kwa nini Serikali isiweke utaratibu wataalam hawa wakaenda kutoa elimu katika shule zetu mbalimbali hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi maswali yake yote mawili ni kutoa ushauri na mapendekezo, nimhakikishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mapendekezo ambayo anayotoa, nitayafikisha Serikalini tuone namna ya kuyafanyia kazi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumalizie maswali yaliyobaki, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Desderius John Mipata Mbunge wa Nkasi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 305

**Shule Iliyojengwa na Wananchi Kuhamishwa  
Kupisha Jeshi**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Nkandasi wamejitahidi kujenga Shule ya Sekondari ya Kata ya Milundikwa hadi kufikia Kidato cha Sita, lakini Serikali kuititia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeamua shule hiyo kuhamishwa mara moja kuanzia tarehe 1 Januari, 2017 ili kuliachia Jeshi:-

(a) Je, Serikali inatoa mchango gani katika uhamishaji na ujenzi mpya wa shule hiyo?

(b) Je, Serikali iko tayari kufanya tathmini ya miundombinu yote ya shule na majengo yaliyojengwa na wananchi na thamani hiyo kuitoa katika fedha taslimu kwa ujenzi mpya wa shule?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbuge wa Nkasi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Milundikwa lilikuwa ni Kambi ya JKT iliyokuwa ikiendesha shughuli za malezi ya vijana na uzalishaji mali kabla ya Serikali kusitisha mpango wa kuchukua vijana mwaka 1994. Wakati JKT linasitisha shughuli zake katika Kambi hiyo liliacha majengo ya ofisi na nyumba za makazi, baadaye Halmashauri ya Wilaya ilianzisha shule ya Sekondari ya Milundikwa na kuongeza miundombinu michache katika shule hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya kuliogezea Jeshi la Kujenga Taifa uwezo wa kuchukua vijana wengi zaidi mwezi Novemba mwaka 2016 Serikali ilitoa maelekezo kwa JKT kufufua makambi yaliyokuwa yameachwa mwaka 1994 likiwemo la Milundikwa. Kufuatia maagizo hayo ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nkasi na Halmashauri ya Wilaya hiyo waliratibu na kusimamia utaratibu wa kuhamisha Walimu na wanafunzi waliyokuwa katika shule Milundikwa kwenda katika shule jirani. Baadhi ya wanafunzi walihamishiwa katika shule ya Sekondari ya Kasu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia maendeleo ya wanafunzi waliokuwa wakisoma katika Shule ya Sekondari ya Milundikwa mnamo tarehe 9 Februari, 2017 Wizara ya Ulinzi na JKT kuitia Makao Makuu ya JKT ilitoa mabati idadi 2,014 ili kuhakikisha kuwa vyumba vya madarasa vilivyokuwa vinaendelea kujengwa vinakamilika

na kuanza kutumika. Wizara yangu itakuwa tayari kuendelea kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya katika kutoa vifaa vya ujenzi kadri uwezo utakavyoruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Desderius Mipata, swali la nyongeza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nakiri kwamba ni kweli Jeshi la Kujenta Taifa wametusaidia na wanaendelea kutusaidia hata katika kazi nyingine, lakini wakati shule hii inatwaaliwa ilikuwa na miundombinu mingi sana na sasa miundombinu bado hajarejeshwa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule hii sasa haina nyumba hata moja ya Mwallimu na ukizingatia kwamba ina Kidato cha Tano na Sita ambayo ni *boarding* ni wasichana wanakaa peke yako. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuendelea kutupatia pesa zaidi na hasa pesa za kujenga nyumba za Walimu ambapo sasa hivi hakuna hata nyumba moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili wakati Serikali inatwaa eneo hili na kuipatia Jeshi limezuka suala lingine ambalo ni gumu zaidi. Wanajeshi walipokuja pale wamechukua eneo sasa la mashamba wanayolima wananchi na kufanya wananchi zaidi ya elfu tano wa Vijiji vya Kasu, Milundikwa, Kisula na Malongwe zaidi ya elfu nne kukosa mahali kabisa pa kulima. Naiomba Serikali je, iko tayari kufikiria upya na wakati mwingine ione uwezekano wa kuwagawia wananchi sehemu ya eneo ili waendelee kuendeleza maisha yao? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivoyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba Wizara yangu iko tayari kuendelea

kusaidiana, kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya katika kutoa vifaa vya ujenzi ili waweze kukidhi mahitaji yao ya kuifanya shule hii ipate miundombinu inayotakiwa. Bila shaka kutakuwa kuna bajeti za kawaida za kupitia Halmashauri nazo hizo wakizielekeza huko na sisi tutakuwa tayari kutoa mchango wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali kutwaa eneo hili na kufanya watu wengi karibu elfu nne kukosa sehemu ya kulima nataka nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali haijalitwaa eneo hili bali eneo hili lilikuwa ni mali ya Serikali mali ya JKT toka mwanzoni. Kama wakati wa JKT kurudi pale imetokea kwamba eneo lilidochukuliwa ni zaidi ya lile la awali hilo naweza nikalingalia, lakini ukweli ni kwamba taarifa tulizokuwa nazo ni kwamba JKT wamekwenda kuchukua eneo lao la awali walilokua nalo kabla ya mwaka 1994 kusitisha shughuli za JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitamwomba Mheshimiwa Mbunge tukae ili tulijadili suala hili na ikiwezekana tufanye ziara pale tuone tunaweza kusaidia vipi. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tumalizie swali la mwisho Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo sasa aulize swali lake.

Na. 306

#### **Ununuzi wa Meli za Uvuvi**

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza:-

Uvuvi wa Bahari Kuu unaingiza kipato kikubwa sana na unaweza ukachangia katika bajeti ya nchi yetu:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kununua meli za uvuvi?

(b) Je, Serikali imefikia wapi katika ujenzi wa Bandari ya Uvuvi nchini?

## **NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020 inaelekeza Serikali umuhimu wa nchi kuvuna rasilimali za uvuvi zilizopo katika ukanda wa Bahari Kuu kwa kuwa na meli za Kitanzania. Lengo la kununua meli hizo ni kuwa na meli za Kitaifa kuwezesha uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika ukanda wa Bahari Kuu kwa lengo la kupata chakula na lishe, kuongeza Pato la Taifa na kutoa ajira kwa Watanzania watakaofanya kazi katika meli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanikisha azma hiyo Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeanza utaratibu wa kufufua lililokuwa Shirika la Uvuvi Tanzania (*TAFICO*) hatua itakayowezesha meli zitakazonunuliwa kuwa chini ya usimamizi wa *TAFICO*. Makadirio ya kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (*TAFICO*) ni jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 45 ikiwemo maandalizi ya ununuzi wa meli za uvuvi. Aidha, Wizara inahamasisha Mifuko ya Kijamii, Taasisi, Mashirika ya Umma na Watanzania kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara tayari imempata mtaalam mwelekezi atayefanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ambapo kukamilika kwa kazi hii kutawezesha kujua gharama halisi za ujenzi na aina na ukubwa wa bandari itakayojengwa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mattar Salum, swali la nyongeza.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri anafanya kazi vizuri, lakini nimfahamishe Mheshimiwa

Waziri eneo hili la uvuvi na ununuaji wa meli za uvuvi na ujengaji wa Bandari ya uvuvi ni suala *very important* lazima tulifanyie kazi kwa kina. Sasa swali la kwanza, Shirika la *TAFICO* ni lini litakamilika ili hizi meli ziweze kununuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kila siku tunasema tuna wataalam ambao wanafanya upembuzi yakinifu, lakini nimwambie Mheshimiwa Waziri hebu atueleze ni lini hawa wataalam watakamilisha huu upembuzi wao yakinifu ili hii bandari ya uvuvi iweze kujengwa kwa maslahi ya Watanzania. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza hapa kwamba tumeshampata mshauri elekezi na tayari attingia mkataba mwezi huu huu na kulipwa malipo ya awali na atafanya kazi ndani ya miezi nane. Baada ya miezi nane tayari tutakuwa tumeingia hatua sasa ya ujenzi wenyewe. Kwa hiyo, atuvumile katika hiyo hatua, Mshauri Elekezi ameshapatikana na tayari zoezi litaanza. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka wakati nikisoma taarifa ya Mheshimiwa Spika kwamba tutawasikia wenzetu waliyotuletea heshima wakitusalimu, tutaanza na Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita atusalimu kwa dakika tatu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Stephen Masele. (*Makof!*)

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na kulishukuru Bunge letu Tufuku, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa mapokezi mazuri ambayo mmetuandalia pia nimshukuru Mheshimiwa Spika

na Watumishi wote wa Bunge kwa namna ya pekee ambavyo wametusaidia, wametuombea kuhakikisha kwamba tunaliteea heshima nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa John Pombe Magufuli na Serikali kwa ujumla kwa msaada mkubwa waliotupatia, bila kusahau kwamba leo ni siku muhimu ambayo Wizara ya Mambo Nje inawasilisha bajeti yake. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe niwasilishe pongezi na shukrani za dhati kabisa kwa Waziri wa Mambo ya Nje Mheshimiwa Dkt. Mahiga, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Waheshimiwa Watendaji wote, Naibu Katibu Mkuu, Waheshimiwa Mabalozi walioko Afrika na waliyoko nje ya Afrika. Nitawataja wachache wakiwemo Balozi wetu aliye po Addis Ababa; Balozi wetu Mama Asha Rose Migiro aliye po London, yuko mbali yuko Ulaya lakini aliweza kufanya kubwa ya kutusaidia. Balozi wetu aliye po Nairobi, Balozi Emmanuel Nchimbi aliye po Brazil pamoja na Balozi wa Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Balozi Grace ambaye yupo Mkoo wa Idara ya Afrika wapo Grace wawili pale, Grace Mujuma na Grace Martin ambaye ni Mkoo wa Itifaki kwa kweli wamekuwa msaada mkubwa sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niwashukuru wajumbe wote wa Bunge la Afrika wanaotoka Tanzania, tukiongozwa na Mheshimiwa mama Asha Abdullah Juma maarufu kama Bi. Macron na ndugu yangu Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Mboni Mhita kwa ushirikiano mkubwa sana ambao wameutoa katika kampeni ambazo tulikuwa tukifanya kule Afrika Kusini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimechaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika ambayo ni *organ* muhimu ya Umoja wa Afrika. Moja ya majukumu kama *First*

Vice President ni kusimamia shughuli za Utawala, za Fedha, *Human Resources na Operation* zote za Bunge la Afrika. Jukumu kubwa la haraka ambalo ninalo sasa hivi ni kusimamia timu inayofanya *reform ya African Union*. Timu hii ipo chini ya Rais Paul Kagame, kwa hiyo kwa nafasi yangu *automatic* naingia kusimamia timu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naomba Bunge lako Tufuku liweze kunipa ushirikiano ili niweze kutimiza majukumu yangu vizuri. Kwa nafasi hii nawashukuru sana, Mungu awabariki sana, sina maneno mazuri ya kuwashukuru zaidi ya hayo. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau naomba niwashukuru wananchi wa Shinyanga na naomba niwashukuru kwa kunivumilia, kwa sababu haikuwa kazi rahisi, nilihitaji muda wa kutosha kufanya kampeni. Nawashukuru sana na Jumamosi nitakwenda Shinyanga kuwasalimia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika. Mheshimiwa Mboni Mhita. (*Makofi*)

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, timu nzima ya *Staff* wa Ofisi ya Bunge, naomba kutumia fursa hii kwanza kuwashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa ambao mmekuwa mnatupa. Ushirikiano mkubwa ambao pia mmetupa kwa kipindi hiki ambacho tulikuwa kwenye uchaguzi, lakini kikubwa zaidi naomba nitumie fursa hii kuwashukuru sana kwa kutuamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mjuavyo sisi ni Wabunge ambao ni Bunge hili mlituchagua kuweza kwenda

kuwakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mliweza kutuchagua pia kuweza kuwakilisha Bunge letu hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweza kwenda kuwakilisha katika Bunge la Afrika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi ambayo Tanzania, nasema Tanzania kwa sababu sikugombea kama Mheshimiwa Mboni, bali nimegombea kama Tanzania, nafasi ambayo tumeipata ni ya Urais wa *Caucus*. Ni mara ya kwanza kabisa kwamba, tumeweza kupata Binti kushika nafasi hii toka *Caucus* hiyo ya Vijana ya Bunge la Afrika ambayo ndiyo jukwaa kubwa kabisa ambalo linazungumzia kutatua na kusikiliza changamoto na kero za Vijana Afrika lianzishwe katika Bunge la Afrika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie kwamba, nitafanya kazi kwa uadilifu mkubwa nikweka maslahi ya nchi yangu mbele, nikweka maslahi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mbele. Nawaomba tu Bunge letu pamoja na *Caucus* yetu ya vijana ambayo sisi tuko hatua ya mbele kabisa, nchi nyngi bado hawana *caucus*, lakini nilijivunia sana pale ambapo nilisema kwamba, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuko hatua za mbele na tuna *Caucus* ya Vijana katika Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitawaomba sana wadogo zangu na uongozi mzima, niko hapa kwa lolote lile ambalo litahitaji *intervention* yangu kwenye *platform* ya Bunge la Afrika na Afrika kwa ujumla niko tayari kuwatumikia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii pia kumshukuru sana Mama yangu ambaye ameongozana nami leo, ndugu Zabein Muhaji Mhita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rais wa *Caucus* ya Vijana Bunge la Afrika. Waheshimiwa Wabunge nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo, tutaanza na matangazo ya wageni:-

Kwanza ni wageni walioko jukwaa la Mheshimiwa Spika. Tutaanza na wageni 133 wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Mahiga ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni Ndugu Elizabeth Mahiga ambaye ni Mke wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Mahiga. Tunaye pia, Profesa Adolf Mkenda ambaye ni Katibu Mkuu. Tunaye pia, Balozi Ramadhan Mwinyi ambaye ni Naibu Katibu Mkuu na Dkt. Stergomena Tax ambaye ni Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC*). (*Makofi*)

Vile vile tunaye pia, Balozi Dkt. Ladislaus Komba ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Afrika (*AICC*). Tunaye pia, Ndugu Ali Said Matano ambaye ni Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Viktoria. Tunaye pia Ndugu Alishilia Kaaya ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa *AICC*. Tunaye pia, Dkt. Benard Achiula ambaye ni Kaimu Mkuu wa Chuo cha Diplomasia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hawa viongozi wetu wameambatana na Mabalozi wa nchi mbalimbali na mashirika ya Kimataifa ambao ni Mheshimiwa Eugen Kayihura ambaye ni Balozi wa Rwanda. Mheshimiwa Lucas Domingo ambaye ni Balozi wa Cuba. Tunaye pia, sasa sijui kama hili ni jina la mtu mmoja ama vipi, lakini Balozi Hernandes Polledo, pengine ni huyohuyo mmoja, *many thanks*, sawa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia Mheshimiwa Benson Keith Chali ambaye ni Balozi wa Zambia; Mheshimiwa Sahabi Isa Gada ambaye ni Balozi wa Nigeria; Mheshimiwa Gervais Abayeho ambaye ni Balozi wa Burundi; na Ndugu Joel Cumbo ambaye ni Kaimu Balozi wa Angola. (*Makofi*)

Tunaye pia, Ndugu Joerg Herrera ambaye ni Naibu Balozi wa Ujerumani; Ndugu Alexandre Peaudeau ambaye ni Naibu Balozi wa Ufaransa; Balozi William Ruben ambaye ni Naibu Balozi wa Sudan Kusini; Ndugu Peter Sang ambaye ni

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Mwakilishi wa Balozi wa Kenya; Ndugu Zhu Jianzheng ambaye ni Mwakilishi wa Balozi wa China; Ndugu Vassily Chitaez ambaye ni Mwakilishi wa Balozi wa Urusi. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia, Ndugu Andrea Heath ambaye ni Mkuu wa Shirika la Msalaba Mwekundu (*Red Cross Tanzania*); Ndugu Amin Kurji ambaye ni Mwakilishi Mkazi wa mtandao wa Agha Khan Tanzania; Ndugu Nima Sitta ambaye ni Mkuu wa Ofisi Ndogo ya Shirika la Chakula Duniani (*World Food Program*); tunaye pia, Ndugu Justine Kajerero ambaye ni Mwanzilishi wa Taasisi ya Diplomasia ya Uchumi Tanzania (*TEDEF*). (*Makof*)

Vile vile tunaye Ndugu Lunda Asmani ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Baraza la *Diaspora* la Watanzania Wanaoishi Marekani (*DICOTA*); pia Ndugu Emmanuel Kasoga, ambaye ni Mkurugenzi wa Asasi ya Kidiplomasia ya Vijana (*YDI*); na Ndugu Renatus Muabhi ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama cha Kijamii Taifa. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo Mabalozi ndani ya Wizara, Mkuu wa Itifaki, Wakurugenzi na Wakuu wa Idara na Vitengo vilivyopo chini ya Wizara hii. Mabalozi na wageni wetu wote tunawakaribisha sana Bungeni. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni wawili wa kwangu ambao ni marafiki zangu kutoka Dar-es-Salaam na hawa ni mtoto wa Mheshimiwa Richard Ndassa, anayeitwa Ndugu Annie Ndassa na Ndugu Kauye Mageleja ambaye ni dada wa Mheshimiwa Ndassa. Karibuni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge na tutaanza na mgeni wa Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita, ambaye ni mama yake mzazi, Ndugu Zabein Mhita, ambaye ni Mbunge Mstaafu. Karibu sana mama. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge tunao pia, wageni wawili wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde Naibu Waziri, Ofisi

ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), ambao ni Wakurugenzi wa kampuni ya *Ecosol Design & Consultant* inayo jishughulisha na utengenezaji wa mashine za kutengeneza mkaa kupitia pumba na taka ngumu, ambao ni Ndugu Kareem Hassan na Ndugu Jamal Mohamed. Karibuni sana. (*Makof!*)

Tunaye pia Mgeni wa Dkt. Rashid Chuachua, ambaye ni rafiki yake na huyu ni Ndugu Faya Almasi kutoka Masasi Mkoani Mtwara. Karibu sana. (*Makof!*)

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Flatei Massay, ambaye ni Mke wake, Ndugu Zamzam Abdi kutoka Mbulu, Mkoani Manyara. Karibu sana. (*Makof!*)

Kuna mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mwenyekiti wa CCM Kongoto, Mkoani Mara. Naye huyu ni Ndugu Nestory Matiku. Karibu sana. (*Makof!*)

Tunao pia, wageni wawili wa Mheshimiwa Pauline Gekul, ambao ni wadogo zake kutoka Babati, Mkoani Manyara. Karibuni sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia, wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Kundi la kwanza ni wanafunzi 58 na Walimu sita kutoka Shule ya Msingi ya Marangu *Hills* ili yopo Marangu, Mkoani Kilimanjaro. Karibuni sana. (*Makof!*)

Tunao pia, wanafunzi 10 na Wahadhiri wawili kutoka Chuo Cha Biblia, *ETBC* cha Dodoma. Karibuni sana. (*Makof!*)

Tunao pia, wanafunzi 48 na Walimu Watano kutoka shule ya Sekondari ya Wasichana – Huruma ya Dodoma. Karibuni sana. (*Makof!*)

Tunao pia, wanafunzi 80 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaosomea Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia. Karibuni sana na Mheshimiwa Waziri naona kweli hawa wanaosomea Diplomasia, kwa suti walizopiga leo hapo hatari kabisa. Karibuni sana. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge ninalo pia, tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Joseph Mhagama ambaye ameleta kwa niaba ya uongozi wa *volleyball*/*Basketball*, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa mazoezi kwa wachezaji wa timu za Bunge za mpira wa wavy (*volleyball*) na mpira wa kikapu (*basketball*) kwamba, mazoezi yameshaanza katika viwanja vya Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*) kila siku kuanzia saa 12.00 mpaka saa 1.00 asubuhi, mnaombwa kuhudhuria bila kukosa. Pia, Wabunge wapya ambao wangependa kujunga na michezo hiyo wanakaribishwa kujunga.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa matangazo na tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH ISSA – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa ruhusa yako nitoe pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Stephen Masele kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika, ni fahari kwa Tanzania, ni fahari kwa Bunge, ni fahari kwa mgombea mwenyewe, hongera sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia, kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Mboni Mhita, Rais wa Kikosi cha Vijana –

Bunge katika Afrika. Sisi kama Wizara tumepata heshima ya kuwasaidia hawa Wabunge wetu kugombea na kushinda nafasi hizo walizowania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano Afrika Mashariki Mwaka 2017/2018. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha mpango wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa fadhila na rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika Bunge lako Tukufu, kujadili mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu walionitangulia kuwashukuru na kuwapongeza watoa hoja waliozungumza kabla yangu, hususan, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa utekelezaji na wa majukumu ya Serikali kwa Mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo pia imetoa dira na kuainisha masuala muhimu ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ambayo baadhi yake yanagusa majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi yetu imekuwa nyepesi zaidi kutohana na ushirikiano mzuri na ushauri tunaoupata mara kwa mara kutoka kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, hivyo naomba pia nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii imetoa mchango mkubwa na imekuwa mhimili muhimu katika kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa kutoa ushauri kuhusu masuala mbalimbali ya kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaposimama mbele yenu kusoma hotuba hii, nyuma yangu kuna kundi kubwa la Watendaji na Watumishi walioniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. Sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa kuwa, kwa kiasi kikubwa ndiyo wanaowezesha nisimame mbele yenu leo kuwasilisha hotuba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Susan Alphonse Kolimba, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Profesa Adolf Faustine Mkenda, Katibu Mkuu; Balozi Ramadhan Muombwa Mwinyi, Naibu Katibu Mkuu; Mabalozi wa Tanzania nje ya nchi, Wakuu wa Idara na Vitengo, Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu kwa kujituma na kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kufanikisha kwa kiwango cha juu utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na kuandaa bajeti ya Wizara ya mwaka wa fedha 2018/2019. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa Jimbo la Songea Mjini kifo cha Mheshimiwa Leonidas Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo kilichotokea mwezi Novemba 2017. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Wabunge wote waliochaguliwa na kuteuliwa kisha kuitishwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Kuchaguliwa na kuteuliwa kwao ni kielelezo cha kuaminiwa na wananchi ili kuwawakilisha ipasavyo katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba nichukue fursa hii kumpongeza Dkt. Stergormena L. Tax kwa kuchaguliwa tena kuendelea kushika nafasi ya Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Aidha, napenda kumpongeza Bi. Sabina Seja kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Umoja wa Afrika kuhusu Masuala ya Rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kuwapongeza tena Mheshimiwa Stephen Masele kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika; na Mheshimiwa Mboni Mhita kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Kamati ya Vijana ya Bunge la Afrika. Kuchaguliwa kwao tena ni kielelezo cha kuaminiwa kwa Taifa letu katika medani za kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru kwa dhati mke wangu mpendwa Elizabeth Mahiga pamoja na watoto wetu kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais katika kujenga na kutetea maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu hii kama inavyoonekana katika kitabu cha hotuba kilichowasilishwa kwako naomba iingizwe kwenye kumbukumbu za Bunge hili Tukufu; hivyo basi nitasoma muhtasari wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Mahusiano ya Tanzania na Nchi Nyingine. Mahusiano ya Tanzania na nchi na mashirika mbalimbali ya kikanda na kimataifa yameendelea kushamiri kwa manufaa ya pande zote zinazohusika. Kutokana na mahusiano hayo, tunazo ofisi za ubalozi katika nchi zote ambazo ni majirani zetu kwenye nchi kavu na pia visiwa vya Comoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Tanzania ina jumla ya balozi 41 zinazotuwakilisha nje ya nchi. Pamoja na balozi hizo nchi yetu ina ofisi tatu za Konseli (*Consular*) Kuu katika

Miji ya Mombasa, Jeddah na Dubai. Kadhalika, Tanzania ina jumla ya Makonseli (*Consulars*) wa heshima 35 wanaotuwakilisha katika mijji mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kuwa na mahusiano mazuri ya kidiplomasia na nchi mbalimbali duniani. Hadi sasa jumla ya nchi 62 zina Mabalozi Wakaazi na Makonseli (*Consulars*) wa heshima 24 wanaowakilisha nchi zao hapa nchini Tanzania. Aidha, nchi 39 zinawakilishwa nchini na mabalozi wasio wa makaazi ambao ofisi zao zipo nje ya Tanzania. Katika kuonesha kuimarika kwa mahusiano, nchi za Ethiopia na Belarus zipo katika hatua za kufungua balozi zao hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu hali ya mahusiano kati ya Tanzania na nchi nyingine yanapatikana kuanzia aya ya tisa hadi aya ya 14 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Misingi ya Nchi katika Mahusiano Kimataifa; Tanzania inaheshimu misingi ya mahusiano na mataifa mengine duniani ambayo tuna mahusiano ya kidiplomasia na yale ambayo bado hatuna mahusiano ya kidiplomasia. Ni kwa misingi hiyo mataifa mengine nayo yanawajibika kuheshimu misingi ya Tanzania ambayo ni pamoja na kulinda uhuru wetu, umoja wetu, kujamulia mambo yetu wenyewe bila kuingiliwa, kulinda mipaka ya nchi yetu, kulinda haki, kuimarisha ujirani mwema na kuunga mkono Sera ya Kutofungamana na Upande wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania italinda misingi hiyo daima. Aidha, napenda tueleweke wazi kuwa Tanzania inaendelea kushirikiana na mataifa yote duniani na kushiriki kikamilifu katika mijadala ya majukwaa ya kimataifa katika kutetea uhuru, haki za binadamu na usawa kwa kuzingatia mahusiano yaliyopo kwa kila nchi kwa ajili ya maslahi mapana ya uchumi, jamii na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa mantiki hiyo, Tanzania itaendelea kutekeleza Sera ya Kutofungamana na Upande wowote kama ambavyo imekuwa ikifanya miaka yote na siku zote. Tanzania haitarajji nchi nydingine yoyote kuiamulia mambo yake, kushinikizwa, kutishwa au kuingiliwa na nchi yoyote katika mambo yetu ya ndani. Marafiki wetu ni lazima waheshimu msimamo wetu kwamba hatutachaguliwa nani awe rafiki yetu na nani awe adui wetu. Maslahi ya nchi yetu ni imani yetu ya haki na usawa wa ubinadamu ndio dira ya msimamo wetu kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu misingi ya nchi yetu katika mahusiano ya kimataifa yanapatikana kuanzia aya ya 15 hadi 17 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msimamo wa Tanzania katika Masuala Mbalimbali ya Kimataifa; napenda kutumia fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa msimamo wa Tanzania kuhusu suala la Palestina na Israel haujabadilika. Tanzania inaunga mkono msimamo wa Umoja wa Mataifa wa suluhu ya kuwa na mataifa mawili yaani Palestina huru na Israel salama. Tunaendelea kuunga mkono kufanyika kwa majadiliano yatakayosaidia kumalizika kwa mgogoro huo wa Mashariki ya Kati uliodumu muda mrefu kati ya nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mahusiano yetu na Israel yanaongezeka na tutahakikisha yanaimarika kwa manufaa na maendeleo ya Taifa letu. Tanzania inatambua kuwa Israel ina haki ya kuishi kama Taifa huru na salama; na hivyo ndivyo iwe kwa Wapalestina ambaao ni majirani zao. Tutashiriki katika mijadala yote kimataifa katika kutafuta suluhu ya Mashariki ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania pia inaendelea kuunga mkono juhudzi za usuluhishi wa mgogoro wa Sahara Magharibi katika mchakato wa maelewano unaosimamiwa na Umoja wa Mataifa na kuungwa mkono na Umoja wa Afrika. Tuna imani kuwa kurejea kwa

Morocco katika Umoja wa Afrika kutatoa fursa kwa umoja huo kutoa mchango wake katika kutafuta suluhu ya mgogoro huo ambaao kwa muda mrefu umekuwa ukishughulikiwa na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfalme Mohamed VI wa Morocco alitembelea hapa nchini mwishoni mwa mwaka 2016 na kutiliana saini mikataba 21 ya ushirikiano katika sekta mbalimbali. Tanzania iliunga mkono Morocco kurudi katika Umoja wa Afrika na kuingia katika Baraza la Usalama na Amani la Umoja wa Afrika. Tanzania itaendelea kushirikiana katika vikao mbalimbali vyta kutafuta suluhu ya mgogoro huo. Tunatarajia uhusiano wetu na nchi ya Morocco utaendelea kukua katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, *POLISARIO* ni chama cha ukombozi wa Western Sahara ambacho kilipewa hadhi ya nchi yenye Serikali na uanachama wa Umoja wa Afrika tangu mwaka 1982. Suala hili limeanza kuleta utata kisheria katika Umoja wa Afrika na katika duru za kimataifa. Kihistoria Morocco inadai kuwa eneo hilo lilikuwa ni sehemu ya ufalme wa Morocco kabla ya ukoloni wa Hispania. Kwa kuzingatia maamuzi ya *OAU* Tanzania imekuwa na uhusiano wa Kibalozi na Western Sahara kupitia chama cha *POLISARIO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushiriki wa Tanzania katika Masuala ya Kulinda Amani na Kulinda Amani; Tanzania imeendelea kuunga mkono jithada za kikanda na za Umoja wa Mataifa za kuimarisha amani na usalama duniani. Maelezo ya kina kuhusu jithada hizo yanapatikana katika aya ya 20 hadi 24 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa mwaka 2017/2018, Wizara yangu ilitengewa kiasi cha Sh. 157,980,248,704/= . Kati ya fedha hizo, Sh.149,980,248,704/= ilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.8,000,000,000/= ilikuwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa

matumizi ya kawaida; Sh.140,496,296,704/= ilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo; na Sh.9,483,952,000/= ilikuwa kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ilitarajia kukusanya maduhuli kiasi cha Sh.25,773,882,820/=. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2018, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha Sh. 22,198,966,840/=. sawa na asilimia 86 ya makisio ya makusanyo yote ya maduhuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2018, balozi zetu nje zimerejesha katika Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha Sh.13,025,539,324/=. Wizara yangu inaendelea kusimamia na kutekeleza na kuhakikisha kuwa kiasi chote cha maduhuli kitakachokusanya kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kinarejeshwa katika Mfuko Mkuu kama ilivyoagizwa na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2018, Wizara ilipokea jumla ya Sh.114,185,986,274/=. sawa na asilimia 72 ya bajeti iliyopitishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo, Sh.104,534,835,394/=. ilikuwa kwa ajili ya bajeti ya matumizi mengineyo; Sh.6,226,955,225/= ilikuwa kwa ajili ya mishahara; na Sh. 3,420,195,655/= ilikuwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ilipangiwa bajeti ya maendeleo kiasi cha Sh.8,000,000,000/=. Hadi kufikia mwanzoni mwa mwaka huu mwezi Mei 2018, Wizara ilipokea kutoka Hazina mgao wa fedha wa bajeti ya maendeleo kiasi cha Sh.3,420,195,655/=. sawa na asilimia 42.7 ya fedha za bajeti ya maendeleo iliyokadiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha hizo, Sh. 1,815,527,215/= zimepangiwa kutumika kufanya ukarabati wa jengo la ofisi ya makazi ya watumishi kweneye Ubalozi wa Tanzania Kampala; Sh. 315,425,000/= ni kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balozi Kinshasa; Sh.593,300,000/= kutumika kukarabati nyumba ya Ubalozi wa Tanzania Lilongwe;

Sh.195,943,440/= kukarabati makazi ya Balozi wa Tanzania Brussels; na Sh.500,000,000/= kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya Chuo cha Diplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kufuatilia Wizara ya Fedha na Mipango upatikanaji wa fedha za maendeleo kiasi cha Sh.4,579,804,343/=, sawa na asilimia 57.3 ambazo hazijatolewa ili kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya fedha za umma kama inavyothibitika mapato na matumizi ya Serikali. Kwa kudhihirisha hilo, Wizara pamoja na Balozi zake 39 zimepata hati safi isipokuwa Balozi mbili tu zimepata hati zenye shaka katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2016/2017. Nachukua fursa hili kuwashukuru watendaji wa Wizara na kuwahimiza kwamba waendelee kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya matumizi ya fedha za umma na ununuzi wakati wote wanapotekeliza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, naomba sasa nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi baadhi ya mafanikio ya Wizara katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika malengo ya Sera ya Mambo ya Nje kuna malengo ambayo ni ya kudumu yanayoiwezesha nchi kuwa katika nafasi yake ndani ya jumuiya ya mataifa, kama taifa huru lenye umoja, usalama na lenye hadhi na sifa inazostahili. Hii hasa ni diplomasia ya siasa. Pia kuna malengo ambayo yanaendana na wakati huo na uongozi uliopo na vipaumbele vyta Serikali kwa wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya sitini hadi themanini malengo ya ziada katika Serikali na Sera ya Tanzania yalikuwa ukombozi wa Bara la Afrika kutoka kwa ukoloni na ubaguzi wa rangi. Baada ya kukamilisha hayo

Tanzania iliona umuhimu wa kuwa na Sera ya Mambo ya Nje yenyenye msisitizo wa diplomasia ya uchumi ili kusukuma maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, diplomasia ya uchumi ni msisitizo wa Sera ya Mambo ya Nje yenyenye mikakati, malengo, mbinu na maarifa yanayoelekeza Taifa kupata na kuvuna rasilimali na utaalam kutoka Jumuia ya Mataifa ili kuleta na kuchochaea maendeleo ya Taifa letu. Katika Awamu hii ya Tano, Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli alitangaza mapema kuwa Tanzania iwe ni nchi ya viwanda ili kusukuma zaidi maendeleo ya uchumi na ajira katika uchumi wetu ili ifikapo mwaka 2025 tufikie uchumi wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, azma hii inamaanisha kuwa diplomasia ya uchumi lazima iongeze mkakati wa Diplomasia ya Uchumi wa Viwanda ili kutekeleza maono na mawazo ya Mheshimiwa Rais ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda vilivyojikita kwenye sekta ya kilimo. Kwa hiyo, Diplomasia ya Uchumi wa Viwanda lazima itoe vipaumbele katika uwekezaji, miundombinu, nishati, biashara na masoko ya bidhaa kutoka kwenye viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Diplomasia ya Uchumi wa Viwanda ni nyongeza iliyokuja katika Awamu hii ya Tano. Sambamba na mkakati huo, dhana ya Diplomasia ya Uchumi wa Viwanda lazima ilenge sekta nyingine kama kilimo, utalii na madini ambavyo kwa namna moja au nyingine zinawiana na viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Wizara yangu imeendelea kutekeleza Diplomasia ya Uchumi wa Viwanda kuititia ziara za viongozi, mikutano ya Tume za Pamoja za Kudumu na ushirikiano wa balozi zetu na nchi nyingine na kwa makongamano ya biashara na uwekezaji yaliyofanyika ndani na nje ya nchi. Kuititia juhudii hizo tumeweza kufanikisha kuleta ujumbe wa wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nchi mbalimbali duniani; kuwezesha wafanyabiashara wa Tanzania kutafuta masoko ya bidhaa nje ya nchi na kuvutia utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kurahisisha mazingira ya biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine; kupata misaada na mikopo yenyé masharti nafuu; na kupata ufadhili wa miradi ya maendeleo katika maeneo ya kimkakati. Kwa ujumla nchi imenufaika kuitia sekta za viwanda, biashara, uwekezaji, kilimo, ufugaji, uvuvi, umwagilajji, ujenzi wa miundombinu, afya, nishati, madini, elimu pia mafunzo ya ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hatua inayofanywa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine ni kushawishi nchi marafiki kutufutia madeni, kuyapunguza au kuweka masharti nafuu ya kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa nilipofanya ziara nchini Iran mwezi Oktoba 2017, Serikali ya nchi hiyo iliridhia na kutangaza kusamehe riba ya deni lillillokuwa tangu mwaka 1984 ambayo kwa sasa imefikia kiasi cha Dola za Marekani milioni mia moja hamsini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mwezi Septemba 2017, Serikali ya Brazil pia ilitoa msamaha wa thamani ya Dola za Marekani milioni 203.6 ambayo ni asilimia 86 ya deni lote tunalodaiwa na nchi hiyo. Misamaha hiyo ni wazi itaipa nafuu nchi yetu katika kulipa madeni. Naomba kutumia nafasi hii kuzishukuru Serikali za Iran na Brazil kwa kutusamehe madeni hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa diplomasia ya uchumi na hasa uchumi wa viwanda yanapatikana kuanzia aya ya 32 hadi 54 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushiriki wa Tanzania Katika Jumuiya za Kikanda na Kimataifa. Katika kipindi hiki, Wizara iliendelea kuratibu na kushiriki katika masuala ya ushirikiano wa kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Jumuiya ya Nchi zinazopakana na Bahari ya Hindi na Umoja wa Afrika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara inaendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kutekeleza kikamilifu majukumu mbalimbali kwa lengo la kuendeleza maslahi mapana ya Taifa letu katika Mtangamano wa Afrika Mashariki. Aidha, Wizara inaendelea kuratibu utekelezaji na uondoaji wa vikwazo visivyo vya forodha, wigo wa pamoja wa ushuru wa forodha, itifaki ya soko la pamoja, Itifaki ya Umoja wa Fedha ya Afrika Mashariki, na Ushirikiano baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kanda nyingine. Vile vile, Wizara inaendelea kuratibu sekta za uzalishaji, uendelezaji wa miundombinu na uchumi na huduma za jamii na masuala ya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu hatua hizo ndani ya Afrika Mashariki yanapatikana kuanzia aya ya 55 hadi 77 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Katika kuimarisha ushirikiano na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika mikutano na majukwaa mbalimbali ya Jumuiya hiyo. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara iliratibu ushiriki wa nchi yetu katika masuala ya siasa, ulinzi, usalama na ushirikiano katika *SADC* na Umoja wa Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ushiriki wetu katika Jumuiya hiyo, Tanzania imenufaika kwa kupata ufadhili wa *Euro* milioni 1.4 kati ya *Euro* milioni 31.6 zilitolewa na Umoja wa Ulaya. Fedha hizo zitatumika kufanya mapitio ya sera za viwanda ndani ya Tanzania, kuhamisha biashara na kuondoa vikwazo vya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu ushirikiano wetu na *SADC* yanapatikana katika aya ya 78 hadi 82 ya kitabu changu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Nchi Zinazopakana na Bahari ya Hindi. Wizara inaendelea kushiriki katika masuala yote yanayohusu Jumuiya ya Nchi

zinazopakana na Bahari ya Hindi. Katika kipindi cha mwezi Oktoba, 2017 Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na *Indian Ocean Rim Association (IORA)* ilifanya warsha ya kuandaa Mkakati wa Kikanda wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali ya Uvuvi katika Ukanda wa Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania imeanza kunufaika na mtandao wa kupeana taarifa za biashara (*trade repository*) ikiwemo mfumo wa kodi, uajiri na bidhaa, taratibu za forodha na upatikanaji wa leseni za kuingiza na kutoa bidhaa kwa kila nchi iliyo ndani ya Jumuiya ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wa Afrika; katika kuimarisha ushirikiano na sera na Bara la Afrika, Wizara iliratibu na kushiriki katika mikutano ya 29 na 30 ya Umoja wa Afrika iliyofanyika Addis Ababa Julai, 2017 na Januari, 2018, ambayo ilipitisha maazimio mbalimbali. Maelezo ya kina kuhusu ushiriki wa Tanzania katika Umoja wa Afrika, maazimio yaliyofikiwa pamoja na mikataba iliyosainiwa yanapatikana kuanzia ukurasa wa 85 hadi 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikiano wa Kimataifa; katika kutekeleza jukumu lake la kuratibu masuala ya kimataifa, Wizara yangu iliratibu na kushiriki mikutano mbalimbali. Baadhi ya Mikutano hiyo ni pamoja na:-

Mkutano wa 72 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa; *UN-HABITAT; UNIDO; Kamisheni ya Umoja wa Mataifa* kuhusu Hali ya Wanawake; Mikutano ya Kimataifa inayohusu wakimbizi na uhamiaji; Baraza la Haki za Binadamu; Shirika la Chakula Duniani (*FAO*); na Mkutano wa 25 wa Wakuu wa Serikali wa Jumuiya za Madola. Maelezo ya kina kuhusu masuala haya na mikutano hiyo yanapatikana kutoka ukurasa wa 91 hadi 94 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuratibu na Kusimamia Masuala ya Watanzania Waishio Ughaibuni. Wizara inaendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuwashirikisha na kuwashirikisha Watanzania waishio ughaibuni katika

kuchangia maendeleo ndani ya nchi yetu. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ililanda Kongamano la Nne la *Diaspora* ililowakutanisha Watanzania zaidi ya 200 kutoka nchi mbalimbali za wadau wa maendeleo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ambapo kipaumbele cha Taifa ni viwanda, tunahitaji kufikiria na kuleta ujuzi maalum walionao Watanzania wanaoishi katika *diaspora* au ughaibuni; na vile vile mchangwa kifedha ambao wanaweza kuchangia kutoka kwenye vyanzo vyao binafsi au kwa kushirikiana na raia wa nchi za nje, mabenki na taasisi nyingine za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha viwanda vyetu kukua na kuwa na masoko huko nje tunahitaji kutambua, kupima na kupenya katika masoko mbalimbali ya kigeni. Watanzania walioishi nchi za kigeni na watoto wao wanaweza kuchangia zaidi kutokana na ujuzi wao kwa kupata masoko kwa kutumia ujuzi wao na lugha ya nchi waliko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi walio *diaspora* wanachangia sana maendeleo ya kijamii, uchumi na familia zao za Tanzania na wako tayari kushiriki katika jukumu kubwa la kujenga uchumi wa Taifa hili. Pengine tunahitaji kuwa na mfumo rasmi wa kisheria na kisera ili kuwapa nafasi na fursa Watanzania walio nje kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu. Inakisiwa kuwa Watanzania walio nje wanatuma Tanzania trilioni shilingi moja kila mwaka. Maeleo ya kina kuhusu mchangwa wa *diaspora* katika maendeleo ya nchi yanapatikana kuanzia aya ya 106 mpaka 110.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Hali ya Dunia. Hali ya usalama duniani imeendelea kuimarika pamoja na kwamba changamoto kadhaa zinaendelea kuwepo katika baadhi ya nchi zetu. Changamoto hizo ni pamoja na migogoro ya kisiasa katika baadhi ya nchi, matukio ya kigaidi

na kuongezeka kwa makundi yenye itikadi kali na dhati za kiuchumi na kiusalama zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Tanzania imeendelea kuunga mkono jitihada za kikanda na za Umoja wa Mataifa za kuimarisha amani na usalama duniani. Maelezo ya kina kuhusu tathmini ya hali ya usalama duniani yanapatikana kuanzia aya ya 112 hadi 131 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa dunia umeendelea kuimarika ambapo kwa sasa unakadiriwa kukua kwa asilimia tatu ikilinganishwa na asilimia 2.4 mwaka 2016. Ukuaji huo umechangiwa zaidi na kuimarika kwa uchumi wa mataifa yaliyoendelea, uwekezaji na mitaji kwenye nchi zinazolbukia kiuchumi, pamoja na kupanda kwa bei za bidhaa. Hali hii inatoa matumaini ya kuimarika kwa biashara ya bidhaa hususan kutoka nchi zinazoendelea. Maelezo ya kina yanapatikana kuanzia aya ya 132 hadi 137.

Mheshimiwa Spika, Taasisi Zilizo Chini ya Wizara; Wizara yangu inasimamia taasisi tatu ambazo ni Chuo cha Diplomasia, Taasisi ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani katika Afrika na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano wa Arusha, ambacho pia kinasimamia Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kilichopo Dar es Salaam. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo yanapatikana katika ukurasa wa 138 hadi 146.

Mheshimiwa Spika, Kusimamia Utawala na Maendeleo ya Rasilimali Watu. Wizara yangu ina jumla ya watumishi 456 wa kanda mbalimbali. Kati ya hao 347 wapo Makao Makuu ya Wizara na 109 wapo katika Balozi zetu nje ya nchi. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara ilipata kibali cha kuajiri watumishi 10 wa kanda mbalimbali ambapo hadi sasa watumishi watano tayari wameripoti kazini na watumishi watano tayari ajira zao zinakamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa mabalozi watano ambapo kati yao watatu wamepangia vituo na wawili taratibu za kuwapangia vituo zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliandaa Semina Elekezi kwa Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki iliyofanyika mwaka huu, Januari, 2018, Jijini Dar es Salaam. Lengo la semina hiyo lilikuwa ni kuwajengea uelewa Waheshimiwa Wabunge hao katika masuala yatakayowawezesha kutekeleza kazi zao kikamilifu. Niseme hapa pia kwamba Wizara na Chuo chetu cha Diplomasia tunaandaa mkakati wa kutoa semina kama hizo kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara yangu inakabiliana na changamoto mbalimbali za kimfumo wa dunia, pamoja na zile za kiutendaji. Hata hivyo, pamoja na changamoto hizo Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi mkubwa kwa kuendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wote wa ndani na wa nje, kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali yetu na ushirikiano wa kimataifa yanaendelea na kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shukrani. Kwa namna ya pekee naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Mabalozi, Wawakilishi wa Tanzania katika Nchi za Umoja wa Mataifa na mashirika mengine ya kimataifa kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kupitia nchi na mashirika yao wanayoyawakilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kupata mafanikio makubwa kutokana na mchango wa wadau na washirika wa maendeleo kutoka nchi na asasi mbalimbali za kitaifa, kikanda, kimataifa pamoja na sekta binafsi. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi za Afrika Kusini, Algeria, Australia, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Denmark, Finland, Hungary, India, Italia, Ireland,

Israel, Iran, Japan, Korea Kusini, Kuwait, Malaysia, Marekani, Malta, Misri, Morocco, New Zealand, Norway, Oman, Pakistan, Palestina, Poland, Qatar, Saudi Arabia, Sweden, Singapore, Sri-Lanka, Thailand, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ureno, Urusi, Uswisi, Uturuki na Vietnam. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani ziwaendee pia Umoja wa Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *African Capacity Building Facility*, Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani (*IMF*), *Investment Climate Facility for Africa*, UNDP na Mashirika mengine yote ya Umoja wa Mataifa. Pia *TradeMark East Africa*, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika, *The Association of European Parliamentarians with Africa*, *WWF*, *The Belinda and Bill Gates Foundation*, *Global Fund*, *International Committee of the Red Cross*, *International Federation of the Red Cross and Red Crescent Societies*, *Medecins Sans Frontieres* pamoja na Mifuko na Mashirika mbalimbali ya Misaada. Ni dhahiri kuwa mafanikio tuliyoyapata yamechangiwa kwa misaada wa pekee kabisa na mashirika na nchi hizo mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo pamoja na changamoto hizo, wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Katika mwaka wa fedha huu, pamoja na mambo mengine, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imepanga kutekeleza malengo muhimu kulingana na majukumu yake kama yalivyobainishwa katika aya ya 157 ya kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019, Wizara yangu imetengewa bajeti ya kiasi cha Sh.177,006,232,000/=. Kati ya fedha hizo Sh.154,410,812,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo; Sh.11,795,420,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh.10,400,000,000/= ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya matumizi mengineyo, Sh.116,010,729,689/= ni kwa ajili ya matumizi ya vifungu vya Balozini. Sh.35,324,806,566/= ni kwa ajili ya vifungu vya Makao Makuu ya Wizara; Sh.1,077,362,234/= ni kwa ajili ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala bora Tanzania; Sh.1,000,000,000/= ni kwa ajili ya fedha za matumizi mengineyo ya Chuo cha Diplomasia; Sh.1,239,633,751/= ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Sh.158,279,760/= ni kwa ajili ya Bodi ya Utekelezaji na Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika fedha za bajeti ya maendeleo, kiasi cha Sh.10,400,000,000/= zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kiasi cha Sh.6,180,676,000/= zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Muscat, Oman; Sh.1,819,324,000/= ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi yaliyopo Ubalozi wa Tanzania Khartoum, Sudan.

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani lazima sasa nimalizie; nadhani kumekuwa na mchanganyiko hapa. (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Omiba hela tu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.177,006,232,000/=. Katika fedha hizo Sh.166,606,232,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.10,400,000,000/= ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono.

**HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI DKT. AUGUSTINE PHILIP MAHIGA (MB), WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA BAJETI YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

#### **UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2017/18. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/19.
2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa fadhila na rehema, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika Bunge lako Tukufu, kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu.
3. **Mheshimiwa Spika**, naungana na wenzangu walionitangulia kuwashukuru na kuwapongeza watoa hoja waliozungumza kabla yangu, hususan Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango ambao kwa hakika hotuba zao sio tu zimezungumzia mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano, bali pia zimetoa dira katika mustakabali wa taifa letu kwa kuainisha masuala muhimu ya kitaifa,

kikanda na kimataifa ambayo baadhi yake yanagusa majukumu ya Wizara yangu.

**4. *Mheshimiwa Spika*,** naomba pia nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya uongozi wa Mhe. Mussa Azan Zungu (Mb) na Makamu wake Mhe. Salum Mwinyi Rehani (Mb). Kamati hii imetoa mchango mkubwa na imekuwa muhimili muhimu katika kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa kutoa ushauri kuhusu masuala mbalimbali ya kiutendaji.

**5. *Mheshimiwa Spika*,** kwa namna ya pekee naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Susan Alphonse Kolimba (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Prof. Adolf Faustine Mkenda, Katibu Mkuu; Balozi Ramadhan Muombwa Mwinyi, Naibu Katibu Mkuu; mabalozi wa Tanzania nje ya nchi; Wakuu wa Idara na Vitengo; watumishi wa Wizara; na taasisi zilizo chini ya Wizara yangu kwa kujituma na kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kufanikisha kwa kiwango cha juu utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18, pamoja na kuandaa Bajeti ya Wizara ya mwaka wa fedha 2018/19.

**6. *Mheshimiwa Spika*,** kwa masikitiko makubwa, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa Jimbo la Songea Mjini kifo cha Mhe. Leonidas Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo kilichotokea mwezi Novemba 2017. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi. Amina.

**7. *Mheshimiwa Spika*,** nawapongeza wabunge wote waliochaguliwa na kuteuliwa kisha kuapishwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Kuchaguliwa na kuteuliwa kwao ni kielelezo cha kuaminiwa na wananchi ili kuawakilisha ipasavyo katika Bunge hili.

**8. *Mheshimiwa Spika*,** nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitamshukuru kwa dhati mke wangu mpandwa Elizabeth

Mahiga pamoja na watoto kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu nillyopewa na Mheshimiwa Rais katika kujenga na kutetea maslahi ya taifa letu.

## **HALI YA MAHUSIANO NA NCHI NYINGINE**

**9.** *Mheshimiwa Spika*, mahusiano ya Tanzania na nchi na mashirika mbalimbali ya kikanda na kimataifa yameendelea kushamiri kwa manufaa ya pande zote zinazohusika. Tanzania tuna mahusiano mazuri na majirani zetu wote. Kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Tanzania ina makubaliano ya kuondoa vikwazo vya biashara na nchi zote jirani, yaani Msumbiji, Malawi, Zambia, Kongo DRC, Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya. Kwa kuzingatia misingi ya Sera yetu ya Mambo ya Nje, tumeendelea kuchukua kila hatua kudumisha ujirani mwema na nchi jirani. Tunazo ofisi za ubalozi katika nchi zote ambazo ni majirani zetu kwenye nchi kavu na pia katika visiwa vya Komoros. Tumeendelea na jitihada za kujenga ujirani mwema kwa jamii zinazoishi mipakani na jamii za nchi jirani.

Katika kuimarisha mahusiano hayo, viongozi wa nchi na mashirika mbalimbali wameendelea kufanya ziara hapa nchini. Mathalan, kwa mwaka wa fedha 2017/18, Tanzania ilipokea Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka Uganda, Misri, Burundi, Msumbiji na Rwanda. Aidha, Mawaziri na Naibu Mawaziri kutoka nchi za Ujeruman, Israel, Uingereza, Norway, Oman, Burundi, Misri, Poland, Shelisheli, Maldves, China na Brazil walitembelea Tanzania katika kipindi hicho. Pia, Tanzania ilipokea wajumbe maalum wa wakuu wa nchi na serikali kutoka nchi za Uganda, Rwanda, Misri, Poland, Burundi, Morocco, Mjumbe Maalum wa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa na Palestina. Aidha, Ethiopia ipo katika hatua za mwisho za kufungua ubalozi hapa nchini na Belarus nao wametuma timu ya uangalizi mwezi Desemba 2017 na kuahidi kufungua ubalozi wao mwezi Juni 2018.

**10.** *Mheshimiwa Spika*, nchi yetu.ilitembelewa.pia na

Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa yakiwemo Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Chakula na Kilimo (FAO); Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Ukimwi (UNAIDS); na Jumuiya ya Madola. Aidha, viongozi wengine na wataalam kutoka katika mashirika na taasisi mbalimbali za kimataifa ikiwemo Shirika la Maendeleo la Japan (JICA); Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA) na Aga Khan walitembelea Tanzania.

**11. *Mheshimiwa Spika*,** Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa yaani Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar nao walifanya ziara za kiserikali na kushiriki mikutano katika nchi mbalimbali.

**12. *Mheshimiwa Spika*,** Tanzania imeendelea kuwa na mahusiano mazuri ya kidiplomasia na nchi mbalimbali duniani. Hadi sasa jumla ya nchi 62 zina mabalozi wakaazi hapa nchini. Kati ya hizo, nchi za China, Oman, Msumbiji na India zinaendesha pia ofisi ndogo za ubalozi (konseli kuu) Zanzibar. Kadhalika, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, pamoja na kuwa na ubalozi Dar es Salaam, ina Konseli Kuu mjini Kigoma. Aidha, nchi 39 zinawakilishwa nchini na mabalozi wasio wakaazi ambao ofisi zao zipo nje ya Tanzania. Vilevile, wapo makonseli wa heshima 24 wanaowakilisha nchi zao hapa nchini na yapo mashirika 23 ya kimataifa yenye hadhi ya kidiplomasia yanayofanya kazi nchini.

**13. *Mheshimiwa Spika*,** Tanzania ina jumla ya balozi 41 zinazotuwakilisha nje ya nchi. Pamoja na balozi hizo nchi yetu ina ofisi 3 za Konseli Kuu katika miji ya Mombasa, Jeddah na Dubai. Kadhalika Tanzania ina jumla ya makonseli wa heshima 35 wanaotuwakilisha katika miji mbalimbali duniani.

**14. *Mheshimiwa Spika*,** katika hotuba yangu ya bajeti mwaka jana nilieleza kuhusu Serikali kufungua balozi mpya sita katika nchi za Algeria, Israel, Uturuki, Sudan, Qatar na Korea

Kusini. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba tayari tumepeleka mabalozi kwenye vituo hivyo.

### **MISINGI YA NCHI KATIKA MAHUSIANO YA KIMATAIFA**

**15.** *Mheshimiwa Spika*, taifa lolote duniani huongozwa na misingi ambayo lengo lake kuu ni kudumisha amani, ulinzi, usalama na mshikamano wa wananchi wake na taifa kwa ujumla. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaongozwa na misingi iliyowekwa na waasisi wa Taifa letu mara baada ya uhuru. Misingi hiyo ni pamoja na kulinda uhuru wetu; kujiamulia mambo yetu wenyewe bila kuingiliwa; kulinda mipaka ya nchi yetu; kulinda haki; kuimarisha ujirani mwema; na kuunga mkono Sera ya Kutofungamana na Upande wowote kama dira na msimamo wetu katika mahusiano na nchi nyingine katika Jumuiya ya Kimataifa.

**16.** *Mheshimiwa Spika*, misingi hiyondiyo inayotufanya leo tujivunie Taifa lenye amani, ulinzi imara na usalama duniani; taifa ambalo limekuwa mstari wa mbele kutetea wanyonge, haki na uhuru; kutafuta amani na kutatua migogoro ya nchi mbalimbali kwa gharama kubwa ya rasilimali watu na fedha; Taifa linalojitolea wanajeshi wake kwenye ulinzi wa amani, na kuwa tegemeo la mataifa katika misheni za kulinda amani; Taifa ambalo limekuwa kimbilio kubwa kwa wananchi wa mataifa mengine yenye migogoro na ambao wanalahazimika kukimbilia nchi nyingine kuokoa maisha yao na kupewa hifadhi nchini mwetu.

**17.** *Mheshimiwa Spika*, Tanzania inaheshimu misingi ya mahusiano na mataifa mengine duniani ambayo tuna mahusiano ya kidiplomasia na yale ambayo bado hatuna mahusiano ya kidiplomasia. Ni kwa misingi hiyo, mataifa mengine nayo yanawajibika kuheshimu misingi ya Tanzania kama ilivyoainishwa hapo juu. Nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania italinda misingi hiyo daima. Aidha, napenda ielevweke wazi kuwa Tanzania itaendelea kushirikiana na mataifa yote duniani na kushiriki kikamilifu katika mijadala na majukwaa ya kimataifa katika kutetea uhuru, haki za binadamu na usawa kwa kuzingatia mahusiano yaliyopo kwa

kila nchi kwa ajili ya maslahi mapana ya uchumi, jamii na maendeleo ya nchi yetu.

Ni kwa mantiki hiyo, Tanzania itaendelea kutekeleza Sera ya Kutofungamana na Upande wowote kama ambavyo imekuwa ikifanya siku zote. Tanzania haitarajii nchi nyingine yoyote kuiamulia mambo yake, kushinikizwa, kutishwa au kuingiliwa na nchi yoyote katika mambo yetu ya ndani. Marafiki wetu ni lazima waheshimu msimamo wetu kwamba hatutachaguliwa nani awe rafiki yetu na nani awe adui wetu. Maslahi ya nchi yetu na imani yetu ya haki na usawa wa binadamu ndio dira ya msimamo wetu kimataifa.

## **MSIMAMO WA TANZANIA KATIKA MASUALA MBALIMBALI YA KIMATAIFA**

**18.** *Mheshimiwa Spika*, napenda kutumia fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa msimamo wa Tanzania kuhusu suala la Palestina na Israel haujabadilika. Tanzania inaunga mkono msimamo wa Umoja wa Mataifa wa suluhu ya kuwa na mataifa mawili yaani Palestina huru na Israel salama. Tunaendelea kuunga mkono kufanyika kwa majadiliano yatakayosaidia kumalizika kwa mgogoro huo uliodumu muda mrefu kati ya nchi hizi mbili. Ni kweli kwamba mahusiano yetu na Israel yanaongezeka na tutahakikisha yanashamiri kwa manufaa na maendeleo ya Taifa letu. Tanzania inatambua kuwa Israel ina haki ya kuishi kama Taifa huru na salama na hivyo ndivyo iwe kwa Wapalestina ambao ni majirani zao. Tutashiriki katika mijadala yote kimataifa katika kutafuta suluhu ya mashariki ya katи.

**19.** *Mheshimiwa Spika*, Tanzania pia inaendelea kuunga mkono juhudzi usuluhishi wa mgogoro wa Sahara Magharibi, katika mchakato wa maelewano unaosimamiwa na Umoja wa Mataifa na kuungwa mkono na Umoja wa Afrika. Tuna imani kuwa kurejea kwa Morocco katika Umoja wa Afrika kutatoa fursa kwa Umoja huo kutoa mchangwo wake katika kutafuta suluhu ya mgogoro huo ambao kwa muda mrefu imekuwa ukishughulikiwa na Umoja wa Mataifa. POLISARIO ni chama cha ukombozi ambacho kilipewa hadhi ya Serikali

na uanachama waUmoja wa Afrika tangu mwaka 1982. Suala hili limeanza kuleta utata wa kisheria katika Umoja wa Afrika na katika duru za kimataifa. Morocco imeanzisha Ubalozi hapa nchini. Mfalme Mohamed VI alitembelea hapa nchini mwishoni mwa mwaka 2016 na kutiliana saini mikataba 21 ya ushirikiano katika sekta mbalimbali. Tanzania iliunga mkono Morocco kurudi katika Umoja wa Afrika na kuingia katika Baraza la Usalama na Amani la Umoja wa Afrika.Tanzania itaendelea kushiriki katika vikao mbalimbali vya kutafuta suluhu ya mgogoro huo. Tunatarajia uhusiano wetu na nchi ya Morocco utaendelea kukua hasa katika sekta mbalimbali.

## **UTEKELEZAJI WA SERA YA MAMBO YA NJE**

### **Kulinda Amani**

**20.** *Mheshimiwa Spika*, hali ya usalama duniani imeendelea kuimarika pamoja na kwamba changamoto kadhaa zimeendelea kuwepo katika baadhi ya maeneo. Changamoto hizo ni pamoja na migogoro ya kisiasa inayoendelea katika nchi mbalimbali duniani, matukio ya kigaidi na kuongezeka makundi yenye itikadi kali pamoja na athari za kiusalama zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Tishio jingine kimataifa ni biashara haramu kama vile za madawa ya kulevyu, usafirishaji wa binadamu na utakatishaji wa fedha ambayo haina mipaka. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Tanzania imeendelea kuunga mkono jitihada za kikanda na za Umoja wa Mataifa za kuimarisha amani na usalama duniani.

**21.** Mheshimiwa Spika, katika kuunga mkono jitihada za Umoja wa Mataifa zinazolenga kuimarisha amani na usalama duniani, nchi yetu imeendelea kutoa mchango wa askari wake kwenye misheni za kulinda amani za Umoja wa Mataifa. Mchango huu ni muhimu na umeiletea nchi yetu sifa kubwa kimataifa kwa askari kuwa na nidhamu na kujitoa katika kuifanya dunia kuwa salama. Ushiriki wa askari wetu katika misheni hizo umewaongeza weledi na ujuzi katika masuala ya medani za kijeshi na usalama wa kimataifa.

22. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, tumekuwa tukipata changamoto za kupoteza baadhi ya askari wetu katika misheni hizo. Kwa mfano, shambulio la tarehe 8 Desemba 2017 liliosababisha askari wetu 15 kupoteza maisha na wengine 43 kujeruhija nchini DRC, linabaki kuwa moja ya shambulizi baya zaidi kuwahi kutokea kwenye misheni za kulinda amani duniani kwa takribani miaka 25 iliyopita.

23. *Mheshimiwa Spika*, tunaushukuru Umoja wa Mataifa kwa kuunda timu ya kuchunguza chanzo cha tukio hilo iliyojumuisha maafisa wawili wa ngazi ya juu kutoka Jeshi la Wananchiwa Tanzania. Timu hiyo imeshakamilisha uchunguzi wake kuhusu chanzo cha tukio hilo na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua ili kuzuia matukio kama hayo yasitokee tena. Serikali inaendelea kuwasiliana na Umoja wa Mataifa kwa ajili ya utekelezaji wa taarifa hiyo ambayo itasaidia pia Umoja wa Mataifa kuboresha utendaji wake na ulinzi wa askari kwenye misheni za kulinda amani.

24. *Mheshimiwa Spika*, naomba ifahamike kwamba, pamoja na shambulio hilo kubwa na la kusikitisha, kamwe hatutarudi nyuma wala kukatishwa tamaa. Tunaamini kwenye misingi yetu ya kusimamia haki na kulinda amani kwa ajili ya kuokoa maisha ya watu na kuweka mazingira mazuri ya ustawi wa jamii. Tanzania itaendelea kusimamia misingi hiyo na kuimarisha ushiriki wetu katika misheni za kulinda amani duniani.

#### **MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18**

25. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu ya Wizara kwa mwaka 2017/18, Wizara yangu ilitengewa kiasi cha **Shilingi 157,980,248,704**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 149,980,248,704** ilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 8,000,000,000** ilikuwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 140,496,296,704** ilikuwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 9,483,952,000** ilikuwa kwa ajili ya mishahara.

26. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara ilitarajia kukusanya maduhuli kiasi cha **Shilingi 25,773,882,820**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2018, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 22,198,966,840**, sawa na asilimia 86 ya makisio ya makusanyo yote ya maduhuli. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2018, balozi zetu nje zimerejesha katika Mfuko Mkuu wa Serikali kiasi cha **Shilingi 13,025,539,374**. Wizara yangu itaendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa kiasi chote cha maduhuli kitakachokusanya kwa mwaka wa fedha 2017/18 kinarejeshwa katika Mfuko Mkuu kama ilivyoelekeza na Serikali.

27. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2018, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 114,185,986,274**, sawa na asilimia 72 ya bajeti iliyopitishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 104,538,835,394** ilikuwa kwa ajili ya bajeti ya Matumizi Mengineyo; **Shilingi 6,226,955,225** ilikuwa kwa ajili ya mishahara; na **Shilingi 3,420,195,655** ilikuwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

#### **Miradi ya Maendeleo ya Wizara**

28. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara ilipangiwa bajeti ya maendeleo kiasi cha **Shilingi 8,000,000,000**. Hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi Mei 2018, Wizara ilipokea kutoka Hazina mgao wa fedha za bajeti ya maendeleo kiasi cha **Shilingi 3,420,195,655**, sawa na asilimia 42.7 ya fedha za bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,815,527,215** zimepangwa kutumika kufanya ukarabati wa jengo la ofisi na makazi ya watumishi kwenye ubalozi wa Tanzania Kampala; **Shilingi 315,425,000** ni kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya balozi Kinshasa; Shilingi 593,300,000 kutumika kukarabati nyumba.za.ubalozi wa Tanzania Lilongwe; **Shilingi 195,943,440** kukarabati makazi ya balozi wa Tanzania Brussels; na **shilingi 500,000,000** kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya Chuo cha Diplomasia.

29. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inaendelea kufuatilia Wizara ya Fedha na Mipango upatikanaji wa fedha za maendeleo kiasi cha **Shilingi 4,579,804,345** sawa na asilimia

**57.3** ambazo hazijatolewa ili kutekeleza miradi ya maendeleo iliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2017/18.

**30.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya fedha za umma katika kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali. Kwa kudhihirisha hilo, Wizara pamoja na balozi zake 39 zimepata hati safi isipokuwa balozi mbili zimepata hati zenye shaka katika ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2016/17. Nachukua fursa hii kuwashukuru watendaji wa Wizara na kuwahimiza waendelee kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya matumizi ya fedha za umma na ununuzi wakati wote wanapotekeleza majukumu yao.

**31.** *Mheshimiwa Spika*, baada ya kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/18, naomba sasa nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi baadhi ya mafanikio ya Wizara katika kipindi hicho.

#### **DIPLOMASIA YA UCHUMI NA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA**

**32.** *Mheshimiwa Spika*, katika malengo ya Sera ya Mambo ya Nje kuna malengo ambayo ni ya kudumu yanayoiwezesha nchi kuwa katika nafasi ya jumuiya ya mataifa kama Taifa huru lenye umoja, usalama na lenye hadhi na siha nzuri. Hii hasa ni diplomasia ya siasa. Pia kuna malengo ambayo yanaendana na wakati huo wa uongozi na vipaumbele vya Serikali na Taifa kwa ujumla. Katika miaka ya sitini hadi themanini malengo ya ziada katika Sera ya Tanzania yalikuwa ukombozi wa Bara la Afrika kutoka kwa ukoloni na ubaguzi wa rangi. Baada ya kukamilisha hayo Tanzania iliona umuhimu wa kuwa na Sera ya Mambo ya Nje yenye msisitizo wa diplomasia ya uchumi ili kusukuma maendeleo ya Taifa letu.

**33.** *Mheshimiwa Spika*, Diplomasia ya uchumi ni msisitizo wa Sera ya Mambo ya Nje yenye mikakati, malengo, mbinu na maarifa yanayoelekeza taifa kupata na kuvuna rasilimali na utaalam kutoka jumuiya ya mataifa ili kuleta na

kuchochea maendeleo ya taifa husika. Mwaka 2001 Tanzania ilipitisha sera inayositisiza diplomasia ya uchumi ili kuendeleza maendeleo hasa katika sekta ya uchumi. Katika Awamu hii ya tano, Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli alitangaza mapema kuwa Tanzania iwe ni nchi ya viwanda ili kusukuma zaidi maendeleo ya uchumi na ajira kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Azma hii inamaanisha kuwa diplomasia ya uchumi lazima iongeze mkakati wa Diplomasia wa Viwanda ili kutekeleza maono na mawazo ya Mheshimiwa Rais kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda vilivyojikita kwenye kilimo. Diplomasia ya uchumi wa viwanda lazima itoe vipaumbele katika uwekezaji, miundombinu ikiwa ni pamoja na nishati, biashara na masoko ya bidhaa kutoka viwandani. Sambamba na mkakati huo, dhana ya diplomasia ya uchumi lazima iendelee kulenga sekta nyingine kama kilimo, utalii na madini ambayo kwa namna moja au nyingine zinashabihiana na viwanda.

### **Viwanda, Biashara na Uwekezaji**

**34. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza diplomasia ya uchumi, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine ndani ya Serikali na kutoka sekta binafsi inaratibu upatikanaji wa masoko, mitaji, na teknolojia kwa ajili ya kukuza biashara na uwekezaji nchini. Miongoni mwa juhudzi zilizofanywa na Wizara yangu ni kushawishi wawekezaji kupitia ziara za viongozi, balozi zetu nje ya nchi, na makongamano ya biashara na uwekezaji yaliyofanyika ndani na nje ya nchi. Kupitia juhudzi hizo, tumeweza kufanikisha kuleta ujumbe wa wawekezaji na wafanyabiashara kutoka nchi kadhaa zikiwemo Ujeruman, Ufaransa, Hispania, Misri, China, India, Falme za Kiarabu, Oman na Israel. Baadhi ya wawekezaji hao tayari wameingia ubia na kampuni za Tanzania na wengine wameanza hatua mbalimbali za uwekezaji nchini. Moja ya hatua hizo ni uamuzi uliofanywa na jumuiya ya wafanyabiashara wa Ujerumani mwezi Aprili 2018 wa kufungua ofisi maalum ya biashara ya nchi hiyo inayoitwa AHK kwa lengo la kuratibu kwa ukaribu zaidi uwekezaji na biashara zinazofanywa na zitakazofanywa na Ujerumani hapa nchini. Aidha, Ufaransa imefungua ofisi ya biashara kupitia

kampuni ya BASF kwa lengo la kuratibu shughuli za kibashara zitakazokuwa zikifanywa na kampuni hiyo na wabia wake hususan katika masuala ya uzalishaji wa kemikali za viwandani.

**35.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu pia iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye makongamano mbalimbali ya biashara na uwekezaji yaliyoandaliwa nje ya nchi. Makongamano hayo ni pamoja na yale yaliyofanyika nchini Kenya, Hispania, Uturuki, Uhlanzi, Indonesia, Korea Kusini, China, Vietnam, Ujeruman na Umoja wa Falme za Kiarabu. Aidha, viongozi wetu wanapopata fursa ya kufanya ziara mbalimbali nje ya nchi wamekuwa wakitumia fursa hiyo kuzungumza na kuwashawishi wawekezaji kuwekeza nchini, binafsi nimekuwa nikifanya hivyo na viongozi wenzangu pia wamekuwa wakifanya hivyo. Kwa mfano, mwezi Aprili 2018 Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein alitembelea Falme za Kiarabu na Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko wa Zanzibar, Mhe. Balozi Amina Salum Ali, alipofanya ziara ya kikazi nchini China walitumia fursa hiyo kushawishi wawekezaji katika sekta za uvuvi, viwanda, kilimo na utalii na hatimaye kuingia nao makubaliano ya kuanza hatua za uwekezaji kwenye sekta hizo.

**36.** *Mheshimiwa Spika*, mwezi Aprili 2018, Wizara ikishirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania; na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania kupitia ubalozi wetu nchini Kenya iliandaa maonesho ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya Tanzania, yaliyofanyika Nairobi. Haya yalikuwa ni maonesho ya kipekee kuwahikufanywa na nchi yetu. Jumla ya kampuni 27 zinazozalisha bidhaa za viwandani kutoka Tanzania zilishiriki ili kutangaza bidhaa zao na kuvutia utalii. Maonesho hayo yalitoa fursa kwa wafanyabiashara wa Tanzania kutafuta masoko ya bidhaa zetu nchini Kenya.

**37.** *Mheshimiwa Spika*, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maonesho hayo yamefungua soko.zaidi kwa bidhaa za Tanzania nchini Kenya na kuimarisha mahusiano

kati ya nchi zetu mbili na wafanyabiashara. Natoa wito kwa wafanyabiashara kuchangamkia fursa ya masoko ya bidhaa za Tanzania ndani ya Jumilya ya Afrika Mashariki. Balozi zetu nyingine pia zimekuwa zikiendesha makongamano na shughuli nyingine mbalimbali za kukuza utalii, kuvutia wawekezaji na kutafuta masoko.

**38.** *Mheshimiwa Spika*, juhudhi hizi zinazofanywa na Wizara yangu pamoja na wadau wengine ndani na nje ya Serikali zinatoa nafasi kwa wafanyabiashara na wawekezaji kujionea fursa mbalimbali za uwekezaji, biashara, masoko, teknolojia na upatikanaji wa mitaji. Hivyo, ninatoa rai kwa wadau wote wanaosimamia masuala ya biashara na uwekezaji kuendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wawekezaji walioonesha nia ya kuwekeza nchini. Nitumie fursa hii kutoa wito kwa wafanyabiashara wetu kutumia fursa hizo kikamilifu.

**39.** *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha biashara kati ya Tanzania na Misri, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau husika iliratibu majadiliano ya kuondoleana ushuru wa forodha na Misri. Majadiliano hayo yamekamilika mwezi Machi 2018 kwa pande zote kukubaliana kuwa, Misri iondoe ushuru kwa kiwango cha asilimia 100, na Tanzania iondoe kwa kiwango cha asilimia 96.89. Kiwango kilichosalia kwa Tanzania kitaondolewa katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

**40.** *Mheshimiwa Spika*, mwezi Februari, 2018 nilifanya ziara ya kikazi nchini Korea Kusini ambapo nilifungua kongamano la biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na nchi hiyo. Kufuatia kongamano hilo viongozi wa kampuni ya Hyundai walifika nchini kufanya mazungumzo na Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC) kwa lengo kuanzisha kiwanda cha kutengeneza vipuli vyta magari. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji itaendelea kufuatilia mazungumzo hayo. Halikadhalika, nilipotembelea China mwishoni mwa mwaka jana nilikutana na wawekezaji katika viwanda vyta magari ambao wameahidi kuja kuona uwezekano wa kuwekeza hapa nchini.

## Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Umwagiliaji

**41.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu iliratibu upatikanaji wa mkopo nafuu wa Dola za Marekani milioni 55 kutoka Serikali ya Poland ambazo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maghala na vihenge vya kuhifadhi nafaka katika mikoa ya Ruvuma, Njombe, Rukwa, Songwe, Dodoma, Shinyanga, Manyara, na Katavi. Kukamilika kwa mradi huo kutapunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno (post-harvest loss). Wizara yangu pia imeratibu upatikanaji wa ufadhili wa mradi wa kituo kikubwa cha ujenzi wa kuzalisha samaki cha Zanzibar unaodhaminiwa kwa ushirika kati ya Korea Kusini kupitia Shirika lake la maendeleo la KOICA pamoja na Shirika la Chakula Duniani (FAO) wenyewe thamani ya Dola za Marekani milioni 3.2.

**42.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine imefanikisha kupatikana ufadhili wa miradi ya umwagiliaji ya Muhongo-Kagera na bonde la Luiche-Kigoma kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait. Baada ya kukamilika kwa tathmini ya miradi hiyo mwezi Machi 2018, rasimu ya mkataba wa kuipatia Tanzania mkopo wa masharti nafuu wenyewe thamani ya Dola za Marekani milioni 15.3 ilisainiwa. Aidha, ushirikiano wa Tanzania na China kupitia jukwaa la FOCAC umeendelea kuchangia sekta ya maji ambapo katika kipindi hiki, Zanzibar imefadhiliwa mradi wa kujenga kituo kipyaa cha kutiba maji katika eneo la Donge Mbiji, wilaya ya Kaskazini Unguja wenyewe thamani ya Dola za Marekani milioni 5.5.

## Ujenzi na Miundombinu

**43.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu imeendelea kujenga mahusiano mazuri na nchi marafiki na mashirika ya kimataifa ambao ni washirika wetu wa maendeleo. Uhusiano huo mzuri umewezesha Serikali kupata ufadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Miongoni mwa ufadhili huo ni ule uliotoka Umoja wa Ulaya, Serikali ya Marekani kupitia shirika lake la maendeleo la USAID, Serikali ya Uingereza kupitia shirika lake la maendeleo la DFID, Serikali ya Japan kupitia

shirika lake la maendeleo la JICA, Serikali ya Korea Kusini kupitia shirika lake la maendeleo la KOICA, Serikali ya Ujerumanii kupitia GIZ, Serikali ya Denmark kupitia DANIDA, Serikali ya Canada kupitia CIDA, Serikali ya Ufaransa kupitia shirika lake la AFD, Umoja wa Falme za Kiarabu kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Abudhabi, Serikali ya Saudi Arabia kupitia Mfuko wake wa Maendeleo wa Saudia, pamoja na Serikali ya Kuwait kupitia Mfuko wake wa maendeleo wa Kuwait. Serikali ya Oman pia imekubali kusaidia kufadhili uboreshaji wa baadhi ya miundombinu katika mikoa mbalimbali ikiwa ni pamoja na Jiji la Dodoma.

**44. *Mheshimiwa Spika***, halikadhalika, China imezikaribisha nchi za Afrika kujunga na mpango wake wa One Belt One Road Initiative ambao unatoa manufaa mapana katika uwekezaji wa miundombinu ya nishati, reli, barabara, bandari na viwanja vya ndege. Kutokana na hatua hiyo, nilipofanya ziara yangu nchini China, niliwasilisha maombi ya Tanzania kujunga na mpango huo. Napenda kulifahamisha Bunge lako kuwa, mwezi Aprili 2018 Serikali ya China ilikubali ombi hilo na taratibu za kujunga na mpango huo zinaendelea.

#### **Afyा na Ustawi wa Jamii**

**45. *Mheshimiwa Spika***, sekta ya afya ni mionganii mwa sekta zinazonufaika na ufadhili wa miradi ya maendeleo kutoka nchi wahisani pamoja na washirika wetu wa maendeleo. Serikali ya Marekani mwezi Mei 2018 iliahidi kutoa Dola za Marekani milioni 512 kufadhili Mpango wa Kupambana na Virusi vya Ukimwi nchini chini ya program yake ijulikanayo kama *President's Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR)*. Serikali ya Kuwait pia imezindua mpango maalum wa kusaidia sekta ya afya hapa nchini wenye thamani ya Dola za Marekani 500,000. Mpango huo ujulikanao kama Half-Million Dollar Program umewezesha upatikanaji wa vifaatiba kwa watu wenye mahitaji maalum katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Mifupa ya MOI, pamoja na Hospitali ya Benjamin Mkapa ya Dodoma. Aidha, Kuwait imetoea Dola za Marekani milioni 13.6 kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa

katika Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja, Zanzibar; na Serikali ya China pia imesaidia ukarabati wa Hospitali ya Abdulla Mzee, Pemba kama moja ya miradi yake ya afya hapa nchini. Serikali ya Israel itaongeza misaada yake ya wataalam, mafunzo na vifaa kwa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Mrisho Kikwete.

**46. *Mheshimiwa Spika*,** Tanzania pia imenufaika na Mfuko wa Afya duniani ujulikanao kama Global Fund unaotoa ufadhili wa programu mbalimbali za kukabiliana na maradhi ya Malaria, Kifua Kikuu na Ukimwi. Tangu mfuko huo uanzishwe hapa nchini mwaka 2013, tayari Tanzania imenufaika na Dola za Marekani takriban bilioni 2 na hivyo kuifanya Tanzania kuwa mionganoni mwa nchi zinazonufaika zaidi na ufadhili wa mfuko huo barani Afrika. Aidha, mwezi Aprili 2018 Serikali ilisaini makubaliano na mfuko huo ya kiasi kingine cha Dola za Marekani millioni 700 kwa ajili ya ufadhili wa miradi ya afya katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Wadau wengine wanaosaidia sekta ya afya ni mashirika ya maendeleo ya kimataifa pamoja na nchi marafiki kama vile Uingereza, Denmark, Canada, Ireland, Palestina, Umoja wa Falme za Kiarabu, Cuba, Misri, Israel, Ujerumani, na Brazil.

### **Nishati na Madini**

**47. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara yangu kwa kutambua umuhimu wa sekta hii katika maendeleo ya uchumi wa nchi imeendelea kuitafutia washirika kutoka nchi marafiki na mashirika ya kimataifa katika miradi yake mbalimbali. Mionganoni mwa wafadhili wakubwa ni Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Dunia. Aidha, kupitia ziara iliyofanywa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Norway hapa nchini mwezi Juni 2017, Serikali ya nchi hiyo imezindua awamu ya pili ya program itakayodumu hadi mwaka 2020, kwa ajili ya kuendeleza sekta ya mafuta nchini. Kupitia programu hiyo, Norway itatoa kiasi cha Dola za Marekani millioni 5.9 kwa ajili ya kuendeleza sekta ya mafuta hapa nchini, na kiasi kingine cha Dola za Marekani milioni 10.5 kwa ajili ya kuendeleza mfumo wa ukusanyaji kodi. Nchi nyingine zinazofadhili miradi kwenye sekta hii kwa kupitia Wizara yangu ni pamoja na Ujerumani, Sweden, Finland na India.

## **Elimu na Mafunzo ya Ufundu**

**48.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu imeendelea kuratibu upatikanaji wa fursa za masomo na mafunzo ya ufundu kutoka nchi marafiki. Ufadhilli huo ni katika mafunzo ya muda mfupi, shahada ya kwanza, uzamili, uzamivu, uboreshaji mafunzo ya ualimu, uboreshaji mitaala na miundombinu ya kufundishia katika vyuo vyetu vya ufundu na teknolojia; vitabu; pamoja na ujenzi wa maktaba ya kisasa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Nachukua fursa hii kuzishukuru nchi zote zinazofadhili miradi katika sekta ya elimu na mafunzo ikiwa ni pamoja na China, Italia, Hungary, Poland, Uhlanzi, Australia, India, Malta, Misri, Korea, Malaysia, Indonesia, Vietnam, Japan, New Zealand, Algeria, Uingereza, Ujerumani, Uswisi, Brunei, Oman, Cuba, Israel, Palestina na Saudi Arabia. Natoa wito kwa Watanzania watumie fursa hizi ipasavyo.

## **Utalii**

**49.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu kupitia Balozi zetu nje imeendelea kushirikiana na wadau wengine wa Serikali kutangaza vivutio vya utalii na kuratibu ujio wa watalii nchini. Nafurahi kutambua ripoti iliyotolewa mwezi Mei 2018 na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na ripoti za balozi zetu zikiainisha kwamba idadi ya watalii nchini sio tu imeongezeka lakini pia pato litokanalo na sekta hiyo limeongezeka. Aidha, ripoti hizo zimebainisha kwamba tofauti na ilivyozoeleka huko nyuma kwa watalii wengi walikuwa wakitoka nchi za Marekani, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia na Hispania, hivi sasa kuna ongezeko kubwa pia la watalii kutoka nchi za China, Australia, Uhlanzi, Uswisi, India na Israel. Ongezeko hilo la idadi ya watalii ni matokeo ya kasi ya kuvitangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini inayofanywa na mamlaka za ndani pamoja na balozi zetu nje ya nchi. Wizara yangu kupitia balozi zetu itaendeleza juhudhi hizi kwa kasi zaidi hasa katika Balozi zetu mpya za Korea Kusini, Uturuki, Qatar na Israel.

**50.** *Mheshimiwa Spika*, katika kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania katika nchi zenye watalii wengi, ubalozi

wa Tanzania Beijing umeendelea kutumia nafasi yake ya kimkakati kwa kutangaza utalii wetu kupitia mitandao ya kijamii ya China kama QQ na WeChat kwa kuweka matangazo ya vivutio kwa lugha za kichina. Aidha, ubalozi kwa kushirikiana na mamlaka za utalii nchini ziliandaa ziara za waigizaji mashuhuri kutoka China ambapo waliandaa makala za kutangaza utalii wa Kisiwapanza-Pemba, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Mbuga ya Selou na Ziwa Eyasi. Makala hizo zilizoandaliwa zimelenga kutangazwa katika runinga zinazoangaliwa na watu wengi zaidi nchini China. Soko la watalii kutoka China ni kubwa kuliko yote kama tukijitangaza vizuri.

**51.** *Mheshimiwa Spika*, kufuatia ziara ya meli ya Sultan wa Oman mwezi Oktoba 2017, Serikali ya Oman imeahidi kukarabati na kuhifadhi Jumba la Maajabu (Beit el Ajab) Zanzibar. Aidha, mwezi Aprili 2018 Tanzania na Oman zilisaini makubaliano ya Ushirikiano katika masuala ya kumbukumbu na nyaraka ili kukuza utalii unaotokana na historia kati ya Oman na Zanzibar.

#### **Msamaha wa madeni ya nje**

**52.** *Mheshimiwa Spika*, moja ya hatua inayofanywa na Wizara yangu kwa kushirikiana na wizara nyingine ni kushawishi nchi marafiki kutufutia madeni, kuyapunguza au kuweka masharti nafuu ya kuyalipa. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa nilipofanya ziara nchini Iran mwezi Oktoba 2017, Serikali ya nchi hiyo iliridhia na kutangaza kusamehe riba ya deni lililokopwa mwaka 1984 ambayo kwa sasa imefikia kiasi cha Dola za Marekani milioni 150. Aidha, mwezi Septemba 2017, Serikali ya Brazil pia ilitoa msamaha wa thamani ya Dola za Marekani milioni 203.6 ambayo ni asilimia 86 ya deni lote tunalodaiwa na nchi hiyo. Misamaha hiyo ni wazi itaipa nafuu nchi yetu katika kulipa madeni. Naomba kutumia nafasi hii kuzishukuru Serikali za Iran na Brazil kwa misamaha hiyo.

**53.** *Mheshimiwa Spika*, pamoja na wajibu wa Serikali kulipa madeni yake nje, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine ndani ya Serikali itaendelea na juhudzi za

kuomba kusamehewa au kupata nafuu ya aina yoyote katika kulipa madeni ya Serikali.

### **MIKUTANOYA TUME ZA PAMOJA ZA KUDUMU ZA USHIRIKIANO**

54. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka huu wa fedha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliratibu na kushiriki katika mukutano wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Misri uliofanyika Cairo, mwezi Januari 2018. Mimi binafsi niliongoza ujumbe wa Tanzania katika mukutano huo ambapo nchi zetu mbili zilikubaliana kushirikiana katika sekta za viwanda, biashara na uwekezaji; maji; kilimo, mifugo na uvuvi; ujenzi, uchukuzi na mawasiliano; afya, nishati, maliasili na utalii; elimu, mambo ya ndani ya nchi na habari. Majadiliano ya utekelezaji wa maazimio mbalimbali yameshaanza na tayari uongozi wa Shirika la ndege la Misri umeshatembelea nchini na kukutana na wataalam wa Idara na Taasisi za Serikali.

### **USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA JUMUIYA ZA KIKANDA NA KIMATAIFA**

#### **Jumuiya za Kikanda**

##### *Jumuiya ya Afrika Mashariki*

##### **Uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Forodha**

55. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuratibu kamati ya kitaifa ya kufuatilia uondoaji wa vikwazo vya kibiashara visivyo vya forodha pamoja na mikutano ya kikanda kwa ajili ya kujadili vikwazo mbalimbali vinavyojitokeza. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2017 hadi Machi 2018, jumla ya vikwazo sita vilivyodumu kwa muda mrefu vimeondolewa na hivyo kufikia jumla ya vikwazo 122 vilivyoondolewa tangu mwaka 2009. Majadiliano ya kuviondoa vikwazo vingine 33 bado yanaendelea. Miongoni mwa vikwazo vilivyoondolewa vinavyoihusu Tanzania ni kupunguzwa kwa vizuizi barabarani katika njia kuu ya kati na kaskazini; kuwianisha muda wa kufanya kazi baina ya mamlaka za mapato za Tanzania na Kenya kwenye ukaguzi

wa mizigo katika bandari kavu mjini Nairobi; kuondoa kodi ya ongezeko la thamani katika huduma za bandari kwa mizigo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi; tozo ya Dola za Marekani 152 kwa mabasi yanayotoka Rwanda na zuio la kuuza bidhaa za chakula kwenda Uganda, pamoja na kurekebisha sheria na kuainisha ubora wa bidhaa mbalimbali tunazouziana.

### **Mapitio ya Wigo wa Pamoja wa Ushuru wa Forodha**

**56.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kuratibu na kusimamia mapitio ya Wigo wa Pamoja wa Ushuru wa Forodha. Kwa sasa nchi za Jumuiya zimeendelea kufanya tafiti katika ngazi ya nchi na kanda kwa lengo la kuwa na taarifa sahihi ya namna ya kupanga viwango vya ushuru wa forodha katika Wigo wa Pamoja wa Ushuru wa Forodha wa Jumuiya. Majumuisho ya awali ya matokeo ya tafiti kutoka kila nchi mwanachama wa Jumuiya yanapendekeza mabadiliko ya viwango vya ushuru wa forodha yazingatie ukuzaji wa viwanda kwa nchi wanachama; kupunguza gharama za uzalishaji; kuongeza biashara mionganii mwa nchi wanachama; na kuwalinda walaji.

### **Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki**

**57.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, Wizara iliratibu majadiliano ya mapitio ya Jedwali la Biashara ya Huduma katika Itifaki ya Soko la Pamoja. Lengo la kufanya mapitio hayo ni kuondoa changamoto zilizokuwa zikikwaza utekelezaji wa Itifaki hiyo katika eneo la huduma. Tayari nchi zote wanachama zimewasilisha maboresho ya jedwali la huduma katika Itifaki ya Soko la Pamoja ambapo changamoto zilizoainishwa zimepatiwa ufumbuzi.

**58.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa elimu kwa umma mijini na vijijini ili kuwawezesha wananchi na hasa vijana kushiriki katika kuchangamkia fursa zilizokoto kwenye soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara kwa

kushirikiana na asasi za kiraia pamoja na vyombo nya habari kupitia makongamano mbalimbali iliendesha programu maalum ya kuhamasisha vijana wa Kitanzania kuzitambua na kuzitumia ipasavyo fursa zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki. Programu hiyo ilipewa jina la Kampeni ya Msafara wa Vijana ya Biashara ya Kuvuka Mpaka. Kampeni hiyo ilifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Manyara na Arusha. Wizara pia kwa kushirikiana na Benki ya Dunia ilitoa elimu kwa umma kwa vijana wa vyuo vikuu juu ya kuchangamkia fursa katika mtangamano.

#### **Utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Fedha ya Afrika Mashariki**

**59.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu imeendelea kuratibu na kushiriki katika uandaaji wa sera, sheria, kanuni na taratibu za kuendeleza sekta ya fedha katika eneo la usimamizi wa bima, huduma ndogo za kifedha (microfinance), pensheni na benki. Aidha, Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2018/19 itaendelea kuratibu na kushiriki majadiliano ya maeneo tajwa hapo juu hadi yatakapokamilika.

**60.** *Mheshimiwa Spika*, ninapenda kularifu Bunge lako Tukufu kuwa, Bunge la Afrika Mashariki liliokaa Dodoma mwezi Aprili 2018, lilipokea na kujadili miswada miwili inayohusiana na utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miswada hiyo ni ya kuanzisha Taasisi ya Fedha na Taasisi ya Takwimu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Muswada wa Kuanzisha Taasisiya Fedha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ulipitishwa na Bunge hilo na hatua inayofuata ni kuidhinishwa na Wakuu wa Nchi Wanachama.

#### **Ushirikiano Bainya ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kanda Nyingine**

**61.** *Mheshimiwa Spika*, Viongozi Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mkuu wao wa 18 uliofanyika Dar es Salaam mwezi Mei 2017 pamoja na mambo mengine, walikubaliana kuwa Mheshimiwa Yoweri Kaguta

Museveni, Rais wa Uganda na mwenyekiti wa Jumuiya, akutane na Rais wa Umoja wa Ulaya, Mhe. Jean-Claude Juncker ili kujadili changamoto za Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi (EPA) baina ya Jumuiya hizo. Kufuatia maamuzi hayo, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika ziara hiyo iliyo fanyika Brussels, Ubelgiji mwezi Septemba 2017. Mwenyekiti aliwasilisha rasmi hoja za Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu changamoto za EPA na mwezi Desemba 2017, Rais wa Umoja wa Ulaya, Mhe. Jean-Claude Juncker aliwasilisha majibu ya hoja hizo.

**62.** *Mheshimiwa Spika*, katika Mkutano wa 19 wa Viongozi Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Kampala mwezi Februari 2018 Rais wa Uganda na Mwenyekiti wa Jumuiya aliwasilisha majibu ya Umoja wa Ulaya kwa Viongozi Wakuu wa Nchi za Jumuiya. Viongozi Wakuu hao hawakuridhishwa na majibu yaliyotolewa na Umoja wa Ulaya hivyo, walimpa mamlaka Mwenyekiti wa Jumuiya kuendelea kuwasiliana na Umoja wa Ulaya kwa lengo la kupata majibu yanayoendana na hoja zilizowasilishwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**63.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/18, Wizara iliendelea kuratibu majadiliano ya maeneo yaliyosalia katika kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA-EAC-SADC pamoja na kuweka katika lugha ya kiuandishi viambatisho vya Mkataba huo. Majadiliano yamekamilika katika Kiambatisho Na. II kinachohusu Usulu hishi wa Migogoro ya Biashara, Kiambatisho Na. IV kinachohusu Sheria ya Utambuzi wa Uasilia wa Bidhaa na Kiambatisho Na. X kinachohusu Utatuzi wa Migogoro. Majadiliano yanaendelea baina ya nchi wanachama kwenye kanuni za utambuzi wa uasilia wa bidhaa pamoja na uondoaji wa ushuru wa forodha.

### **Sekta za Uzalishaji**

**64.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imeratibu maandalizi na ushiriki wa Tanzania katika mikutano ya kuandaa sera na mikakati ya kukuza viwanda katika Jumuiya

ya Afrika Mashariki hususan katika maeneo yaliyoainishwa na Wakuu wa Nchi kuwa ya vipaumbele hasa utengenezaji wa magari, uzalishaji wa dawa na bidhaa za nguo na ngozi. Wizara ilihakikisha vipaumbele vya nchi vinajumuishwa katika sera na mikakati iliyoandalialiwa ikiwemo Mkakati wa Tano wa Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2016/17-2020/21. Ni mategemeo yetu kuwa sera hizi za mtangamano zitasaidia kukuza viwanda na hivyo kuchangia kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

#### **Uendelezaji wa Miundombinu ya Uchumi na Huduma za Jamii**

**65. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa programu na miradi ya kikanda ya uendelezaji wa miundombinu ya uchumi na huduma za jamii kama ifuatavyo:

#### **Maendeleo ya Miundombinu ya Uchukuzi, Nishati na Uwekezaji katika Sekta ya Afya**

**66. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkuiano wa Kazi wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliojadili maendeleo ya sekta ya miundombinu ya uchukuzi, nishati, na uwekezaji katika sekta ya afya uliofanyika Kampala mwezi Februari 2018. Lengo la mkuiano huo lilikuwa ni kubaini kiasi cha fedha kinachohitajika kutekeleza miradi hiyo ambapo imeelezwa kuwa katika miaka 10 ijayo kiasi cha Dola za Marekani bilioni 78 zitahitajika kutekeleza miradi ya miundombinu ya uchukuzi na nishati. Hivyo, miradi 17 ya kipaumbele cha juu ilipitishwa ambapo miradi 10 kati ya hiyo itatekelezwa Tanzania.

**67. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuimarisha sekta ya afya, Wakuu wa Nchi walipitisha vipaumbele tisa. Miongoni mwa vipaumbele hivyo ni kupanua wigo wa huduma za tiba za ubingwa kwa kuimarisha miundombinu, vifaatiba na wataalam; na kupambana na magonjwa ya mlipuko na dharura za kiafya zinazotokana na mwingiliano wa kimataifa. Vilevile, vipaumbele hivyo vimielekezwa katika

kujenga uwezo wa taasisi na vyuo vinavyotoa mafunzo ya afya kwa kuwianisha mitaala ya mafunzo, viwango na miongozo katika sekta ya afya ili kuwa na wataalam wa kutosha na wenye weledi; kupanua wigo wa matumizi na huduma za bima ya afya na hifadhi ya afya ya jamii; na kuendeleza utafiti katika sekta ya afya.

**68.** *Mheshimiwa Spika*, ni matumaini yangu kuwa Wizara za kisekta kwa kadri hali ya bajeti itakavyoruhusu, zitaendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kipaumbele.

### **Usimamizi wa Mazingira Bonde la Ziwa Victoria**

**69.** *Mheshimiwa Spika*, wakati wa kikao kilichopita cha bajeti cha 2017/18, nililifarifu Bunge lako Tukufu kuhusu Awamu ya Pili ya Mradi wa Usimamizi wa Mazingira katika Ziwa Victoria. Naomba kulifarifu Bunge lako kuwa mradi huo umekamilika mwezi Desemba 2017 ambapo faida zilizopatikana ni pamoja na kupunguza magugu maji na kuwapatia maji safi na salama wananchi wanaoishi maeneo ya mradi. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine inaratibu majadiliano ya Awamu ya Tatu ya Mradi huo.

**70.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu upatikanaji wa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kikanda cha Uratibu wa Usalama na Uokozi (Maritime Rescue Coordination Centre - MRCC) katika Ziwa Victoria jijini Mwanza. Tanzania imewasilisha Hati ya Umiliki wa Kiwanja chenye ukubwa wa mita za mraba 13,287 kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ujenzi wa kituo hicho utakuwa na manufaa ya kurahisisha usafirishaji katika Ziwa Victoria na udhibiti, uokozi na usalama.

### **Masuala ya Siasa**

**71.** *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea kuimarishe demokrasia, utawala bora, na kulinda haki za binadamu kwa kushirikiana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa kuzingatia hilo, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye kongamano la Utawala Bora la Jumuiya ya Afrika

Mashariki liliofanyika Arusha mwezi Oktoba 2017. Pamoja na mambo mengine, kongamano hilo liliazimia kwamba Tume za Haki za Binadamu za nchi wanachama zitoe mafunzo kwa vyombo vya usalama. Aidha, nchi wanachama zilitakiwa kuimarisha uwezo wa Tume za Uchaguzi ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa usawa na kwa kuzingatia maadili.

### **Uchaguzi Mkuu Nchini Kenya na Rwanda**

72. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza demokrasia na kulinda amani katika Jumuiya, Tanzania ilikuwa sehemu ya timu ya waangalizi wa uchaguzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika chaguzi zilizofanyika nchini Rwanda na Kenya mwaka 2017. Katika chaguzi hizo, Mheshimiwa Uhuru Kenyatta kutoka muungano wa Jubilee alichaguliwa kuwa Rais Kenya na Mheshimiwa Paul Kagame kutoka chama cha RPF alichaguliwa kuwa Rais Rwanda. Ripoti za usimamizi katika chaguzi hizo zimeeleza kuwa chaguzi zilikuwa huru na haki. Nachukua nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa wananchi wa Kenya na Rwanda kwa kufanya chaguzi kwa amani.

### **Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki**

73. ***Mheshimiwa Spika***, Mkutano wa 35 wa dharura wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya uliofanyika Kampala, mwezi Februari 2018 ulipitisha Rasimu ya Andiko, Hadidu za Rejea, na Mpangokazi wa kuanzisha Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki. Aidha, maandalizi ya rasimu ya Katiba ya Fungamano yanaendelea kwa mujibu wa mpangokazi ulioidhinishwa na zoezi hili linatarajiwakukamilika mwaka 2022.

### **Hati Mpya ya Kusafiria ya Kielektroniki ya Afrika Mashariki**

74. ***Mheshimiwa Spika***, Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wao wa 17 uliofanyika Arusha mwezi Februari 2016 walizindua rasmi hati ya kusafiria ya kielektroniki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kukubaliana kuwa kila nchi mwanachama ianze kuzitumia ifikapo mwezi Januari 2018.

75. *Mheshimiwa Spika*, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa mwezi Januari 2018, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Mugufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua rasmi hati hiyo kwa wananchi wa Tanzania. Wananchi wa Tanzania wataruhusiwa kuendelea kutumia hati walizonazo kwa kipindi cha miaka miwili hadi ifikapo mwezi Desemba 2019. Utoaji wa hati hizi unasimamiwa na mamlaka husika katika kila nchi wanachama kulingana na sheria za nchi yake.

#### **Mapambano Dhidi ya Ugaidi na Uharamia**

76. *Mheshimiwa Spika*, Jumuiya ya Afrika Mashariki inaandaa mpango wa utekelezaji wa mkakatiwa kupambana na ugaidi. Mkutano wa wadau uliofanyika Mwanza, mwezi Oktoba 2017 uliandaa mfumo utakaowezesha vyombo vnavyohusika na mapambano dhidi ya ugaidi kufanya kazi kwa pamoja katika kutekeleza mkakati huo.

77. *Mheshimiwa Spika*, katika kupambana na uharamia kwenye Bahari ya Hindi, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kikanda wa kupambana na uharamia kwa kuratibu makubaliano maalum ya namna ya kubadilishana taarifa za wahalifu. Kufikiwa kwa makubaliano hayo kutasaidia nchi wanachama kubadilishana uzoefu na kubaini mbinu zinazotumiwa na maharamia ili kuimarisha mapambano dhidi ya uharamia katika Bahari ya Hindi. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliratibu zoezi la pamoja la kijeshi la kamandi za kijeshi ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lijulikanalo kama 'EAC CPX USHIRIKIANO IMARA 2017' liiilo fanyika Dar es Salaam mwezi Desemba 2017. Lengo la zoezi hilo lilikuwa ni kujenga uwezo wa majeshi ya nchi wanachama katika kuendesha operesheni za kulinda amani; kupambana na ugaidi; kupambana na uharamia; na kukabiliana na majanga.

#### ***Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)***

78. *Mheshimiwa Spika*, Mkutano wa 37 wa Wakuu wa

Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulifanyika Pretoria mwezi Agosti 2017. Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo uliongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akimwakilisha Mheshimiwa Rais.

**79.** *Mheshimiwa Spika*,.naomba.kuliarifu.Bunge lako Tukufu kuwa Mheshimiwa Makamu wa Rais, kama Mwenyekiti wa Asasi hiyo, aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Asasi ya SADC ya ushirikiano katika siasa, ulinzi na usalama kwa kipindi cha Agosti 2016 hadi Agosti 2017.Taarifa hiyo ilieleza kwa kina tathmini ya hali ya siasa, ulinzi na usalama katika kanda hususan katika Nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Madagascar na Falme ya Lesotho. Tanzania ilipongezwa kwa kusimamia vizuri majukumu ya Asasi hiyo.

**80.** *Mheshimiwa Spika*, Mkutano huo, pamoja na mambo mengine, ulimteua Dkt Stergomena L. Tax, kuendelea na wadhifa wa Katibu Mtendaji wa SADC kwa kipindi cha pili na cha mwisho; uliazimia kuisaidia Serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kufanya uchaguzi tarehe 23 Desemba 2018; na kuridhia ombi la Serikali ya Visiwa vya Comoro kuwa mwanachama wa 16 wa Jumuiya hiyo.

**81.** *Mheshimiwa Spika*, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania ilikabidhi rasmi uenyekiti wa Asasi ya SADC ya Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama kwa Jamhuri ya Angola.

### **Ushirikiano kati ya SADC na Umoja wa Ulaya**

**82.** *Mheshimiwa Spika*, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Umoja wa Ulaya ziliingia makubaliano ya mpango wa ushirikiano wa miaka mitano kuanzia mwaka 2015 hadi 2020. Katika Mpango huo, Umoja wa Ulaya, pamoja na mambo mengine, uliridhia kutoa kiasi cha Euro milioni 31.6 kupitia Awamu ya 11 ya Mfuko wa Maendeleo wa Umoja wa Ulaya, kuzisaidia nchi wanachama wa SADC kutekeleza Itifaki

ya Biashara. Tayari Tanzania imenufaika na mpango huo kwa kupokea kiasi cha Euro 420,000 kati ya Euro milioni 1.4 zilizoahidiwa. Kiasi hicho cha fedha kitatumika kufanya mapitio ya Sera ya viwanda ya Tanzania, kuhamasisha biashara na kuondoa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiushuru.

### **Jumuiya ya Nchi Zinazopakana na Bahari ya Hindi**

**83. *Mheshimiwa Spika***, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na IORA ilifanya warsha ya kuandaa Mkakati wa Kikanda wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Uvuvi katika Ukanda wa Bahari ya Hindi mwezi Oktoba 2017.

**84. *Mheshimiwa Spika***, Serikali ya Tanzania imeanza kunufaika na mtando wa kupeana taarifa za biashara (IORA Trade Repository) ikiwemo mfumo wa kodi, uasili wa bidhaa, taratibu za forodha na upatikanaji wa leseni za uingizaji wa bidhaa kwa kila nchi iliyo ndani ya Jumuiya uliozinduliwa rasmi mwezi Agosti 2017.

### **Umoja wa Afrika**

**85. *Mheshimiwa Spika***, Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 30 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa mwezi Januari 2018. Katika Mkutano huo, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alimuwakilisha Mheshimiwa Rais ambapo pamoja na mambo mengine, mkutano huo ulijadili taarifa ya Mheshimiwa Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda na Mwenyekiti wa Kamati ya Kuhuisha Mifumo ya Kitaasisi ya Umoja wa Afrika. Mkutano huo uliazimia nchi wanachama ziendelee na majadiliano ya namna bora ya kutekeleza mapendekezo ya mabadiliko ya kuhuisha Mifumo ya Kitaasisi ya Umoja wa Afrika ili kufikia muafaka kwa nchi zote. Aidha, mkutano huo ulizindua soko moja la usafiri wa anga Afrika. Hadi sasa nchi wanachama 21 zimesaini Mkataba wa soko hilo unaotarajiwaa kuchochea utalii na kuongeza ajira.

**86.** *Mheshimiwa Spika*, katika Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa mwezi Julai 2017, Tanzania ilipata nafasi ya kuchaguliwa kuwa mionganini mwa wajumbe wanne wa Bodi ya Ushauri ya Umoja wa Afrika kuhusu Masuala ya Rushwa ambapo Bi. Sabina Seja anaiwakilisha Tanzania. Wajumbe wengine kwenye Bodi hiyo ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Algeria na Misri.

**87.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Kigali mwezi Machi 2018. Madhumuni ya mkutano huo yalikuwa kupitia mkataba na itifaki tatu za uanzishwaji wa eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA). Hatua hiyo ni utekelezaji wa maazimio ya Wakuu wa Nchi na Serikali yaliyofikiwa mwaka 2012 kutaka kuanzisha Eneo Huru la Biashara Afrika ambapo majadiliano yake yalizinduliwa rasmi mwaka 2015 na kukamilika mwaka 2017. Katika mkutano huo nchi wanachama 44 zilitia saini mkataba huo na hatua inayofuata ni nchi kuridhia ili utekelezaji wake uanze rasmi.

**88.** *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa mkataba huo utazisaidia nchi za Afrika kukua kiuchumi kwa kushiriki kwenye soko la pamoja ambalo lina watu zaidi ya bilioni moja na pato ghafi linalokadirisha kuwa na jumla ya zaidi ya Dola za Marekani triliioni 3.4. Ni muhimu kwa Tanzania kuongeza uzalishaji na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji wa mitaji ili kutumia vyema fursa ya soko hilo.

#### **Mkutano wa Masuala ya Mipaka ya Nchi za Umoja wa Afrika**

**89.** *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza maazimio ya Umoja wa Afrika yaliyofikiwa Addis Ababa mwezi Juni 2007, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuhakiki na kuimarisha mipaka yake na nchi tunazopakana nazo na tayari tumeanza kuhakiki mipaka kati ya Tanzania na nchi za Kenya na Uganda.

**90.** *Mheshimiwa Spika*, napenda kuliarifu Bunge lako

Tukufu kuwa mbali na utekelezaji wa azimio hilo, zoezi la uhakiki wa mipaka ya nchi yetu ni endelevu, na linalenga kuweka usimamizi mzuri wa maeneo ya mipaka; kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu; kurahisisha ukusanyaji wa mapato mipakani; kudhibiti uhalifu katika maeneo ya mipaka; kuweka mipango ya maendeleo na utoaji wa huduma za msingi za jamii; na kuimarisha mahusiano mazuri yaliyopo baina ya jamii za mipakani.

### **Ushirikiano wa Kimataifa Umoja wa Mataifa**

**91.** *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza jukumu lake la kuratibu masuala ya kimataifa, Wizara yangu iliratibu na kushiriki mikutano mbalimbali. Baadhi ya Mikutano hiyo ni pamoja na: Mkutano wa 72 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa; UN-HABITAT; UNIDO; Mkutano wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa kuhusu Hali ya Wanawake; Mikutano ya Kimataifa inayohusu wakimbizi na uhamiaji; Baraza la Haki za Binadamu; Shirika la Chakula Duniani (FAO); na Mkutano wa 25 wa Wakuu wa Serikali wa Jumuiya ya Madola.

**92.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 72 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliofanyika New York, Marekani kuanzia mwezi Septemba hadi Desemba 2017. Nilipata fursa ya kumwakilisha Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika vikao vya ngazi ya juu viliviyokutanisha Wakuu wa Nchi na Serikali za nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa. Masuala muhimu yaliyojadiliwa wakati wa vikao hivyo yalihusu uhusiano wa kidiplomasia, ajenda ya uendelezaji wa viwanda, biashara, uwekezaji, hali ya usalama na amani duniani na mapambano dhidi ya ugaidi.

**93.** *Mheshimiwa Spika*, pamoja na masuala mengine, Tanzania ilitumia fursa hiyo kuelezea jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano ya kuendelea kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa na Mashirika yake. Vilevile, Tanzania ilieleza hali ya utekelezaji wa ajenda ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030 (Malengo ya Maendeleo Endelevu) na hatua

zinazochukuliwa na Serikali katika kuwaleta maendeleo watu wake ikiwemo mapambano dhidi ya rushwa; dawa za kulevyia; uwindaji haramu; kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuziba mianya ya ukwepajji kodi; na kusimamia uwajibikaji na nidhamu ya utumishi wa umma. Aidha, Tanzania ilitumia fursa hiyo kuomba mashirika ya kimataifa na wadau wengine wa maendeleo kuendelea kutoa misaada ya fedha, teknolojia na utaalam ili kuunga mkono juhudzi za Serikali za kuleta maendeleo endelevu na kuondoa umaskini nchini.

**94. *Mheshimiwa Spika*,** Tanzania kama zilivyo nchi wanachama wengine wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) ilishiriki katika Mkutano Mkuu wa 39 wa Shirika hilo uliofanyika Paris mwezi Oktoba 2017. Ajenda kuu ya Tanzania katika Mkutano huo illikuwa kuwasilisha uamuzi wake wa kutekeleza mradi mkubwa wa umeme wa Stigler's Gorge. Katika kutekeleza azma hii, ujumbe wa Tanzania uliungana na wajumbe wengine wa nchi zinazoendelea kusisitiza umuhimu wa Shirika hilo kuweka uwiano kati ya uhifadhi wa maeneo ya urithi wa dunia na kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo kwenye maeneo husika. Aidha, nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania zilitumia mkutano huo kuomba msaada wa kuimarisha miundombinu katika maeneo hayo.

**95. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara yangu inaendelea kushirkiana na wadau wengine kusukuma ajenda ya kitaifa ya kufikia uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Katika kutekeleza azma ya kukuza viwanda, Wizara iliratibu ujio wa Dkt. Li Yong, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maendeleo ya Viwanda Duniani (UNIDO) mwezi Machi 2018. Moja ya manufaa ya ziara hiyo illikuwa ni kusainiwa kwa tamko la kusudio la kuiingiza Tanzania katika mpango maalum wa ushirikiano wa kuendeleza viwanda unaojulikana kama Program for Country Partnership. Kwa kuwa mpango huu umefanyika kwa mafanikio katika nchi za Ethiopia, Senegal na Peru, Tanzania inaendelea na majadiliano ya karibu na UNIDO ili nayo iingizwe katika mpango huo wenye fursa kubwa katika kusukuma

maendeleo ya viwanda ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya viwanda.

**96.** *Mheshimiwa Spika*, katika ziara hiyo Shirika la UNIDO lilitoa msaada wa vifaa vya kilimo vyenye thamani ya Dola za Marekani 80,000 kwa wakulima wa zao la mwani Zanzibar. Vifaa hivyo vitatumika kwa ajili ya shughuli za kilimo, usafirishaji na usindikaji wa mwani jambo ambalo litasaidia kuongeza thamani ya zao hilo katika soko la dunia.

**97.** *Mheshimiwa Spika*, mwaka jana nililijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuridhia Mkataba wa Paris chini ya mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi ambao Bunge lako Tukufu liliridhia mwezi Aprili 2018. Napenda kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa hatua hiyo na tayari Mheshimiwa Rais alisaini hati ya kuridhla na hivyo kuwezesha nchi yetu kutambuliwa rasmi kama mwanachama wa makubaliano hayo. Naomba kutumia fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine wote ndani na nje ya Serikali kwa ushirikiano mkubwa waliota kuwezesha suala hili kufanikiwa. Ni dhahiri kwamba makubaliano haya yana manufaa kwa nchi yetu na dunia nzima.

### **Kushughulikia Masuala ya Wakimbizi**

**98.** *Mheshimiwa Spika*, moja ya nguzo za Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania ni kulinda utaifa wetu, mipaka ya nchi na uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kusimamia nguzo hii muhimu, mwezi Januari 2018, Serikali ilifanya uamuzi wa kujittoa kwenye mpango maalum wa majaribio wa kuhudumia Wakimbizi ujulikanao kama Comprehensive Refugees Response Framework (CRRF). Mpango huo unalenga kuwanufaisha wakimbizi kwa kupanua wigo wa hifadhi yao na kuwawezesha kujitegemea kwa Serikali kuwapatia ardhi, uhuru wa kutembea mahali popote na vibali vya kufanya kazi popote nchini.

**99.** *Mheshimiwa Spika*, uamuzi wa Serikali kujittoa kwenye

Mpango huo umezingatia maslahi mapana ya Taifa letu hususan masuala ya usalama. Nitumie fursa hii kulihakikishia Bunge Iako Tukufu kuwa pamoja na nia yetu nzuri ya kuwasaidia wakimbizi; usalama, amani na ulinzi wa Taifa letu ndivyo vipaumbele namba moja vya Taifa letu.

**100. *Mheshimiwa Spika*,** pamoja na Serikali kutokua fiki mpango huo bado Tanzania itaendelea kupokea na kuhifadhi wakimbizi pale inapolazimika kwa kuzingatia sheria za nchi na mikataba ya kikanda na kimataifa. Aidha, tunaendelea kutoa wito kwa wakimbizi kurudi makwao kwa hiari pale ambapo hali ya usalama kwenye nchi zao inapotengemaa.

#### **Jumuiya ya Madola**

**101. *Mheshimiwa Spika*,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, alimwakilisha Rais kwenye mkutano wa 25 wa Wakuu wa Serikali wa Jumuiya ya Madola uliofanyika London mwezi Aprili 2018. Mkutano huo, pamoja na mambo mengine, ulipitisha maazimio matano yanayosisitiza kuifanya dunia kuwa mahali penye ustawi na salama zaidi ili kuchochaea maendeleo, kuleta usawa, utunzaji wa mazingira, amani, haki za binadamu na demokrasia. Maazimio hayo pia yameweka msisitizo kwenye mapambano dhidi ya ugaidi, usafirishaji haramu wa binadamu, utumwa, makundi yenye misimamo mikali na uhalifu mwagine wa kimataifa.

**102. *Mheshimiwa Spika*,** Wakuu wa Serikali kwa kauli moja walikubaliana kufanya kila liwezekanaloo kuongeza biashara na uwekezaji mionganoni mwa nchi wanachama. Tanzania ilifanikiwa kuingiza ajenda ya viwanda, nishati ya uhakika na kukuza uchumi kuwa sehemu ya majadiliano na hatimaye kuingia kwenye tamko la mwisho la mkutano huo.

**103. *Mheshimiwa Spika*,** wakati wa mkutano huo, Mheshimiwa Makamu wa Rais alifanya mazungumzo na viongozi wa nchi mbalimbali wakiwemo Rais wa Uganda, Waziri Mkuu wa Australia, Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa wa Uingereza na Mjukuu wa Malkia, Prince William. Katika

mikutano hiyo, viongozi hao waliahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania katika masuala mbalimbali yakiwemo ya elimu, biashara na uwekezaji na mapambano dhidi ya ujangili na biashara haramu ya wanyamapor. Prince William ni mmoja kati ya viongozi wanaounga mkono jitihada za Tanzania katika mapambano dhidi ya ujangili na uwindaji haramu.

**104. *Mheshimiwa Spika*,** akiwa London, Mheshimiwa Makamu wa Rais alikutana na viongozi wa makampuni sita yanayowekeza na yenye nia ya kuwekeza nchini Tanzania. Kwenye mikutano hiyo, Mheshimiwa Makamu wa Rais aliwathibitishia na kuwashakikishia kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji nchini na kukaribisha wawekezaji wengine.

#### **KUSIMAMIA MIKATABA NA MAKUBALIANO YA KIMATAIFA**

**105. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 Wizara iliratibu na kusimamia kusainiwa kwa mikataba, hati.za.makubaliano.na.kumbukumbu za mazungumzo baina ya Tanzania na nchi mbalimbali. Mikataba na makubaliano hayo ni kiashiria kikubwa katika kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi yetu na nchi nyingine, mashirika ya Kikanda na Kimataifa katika kuongeza kasi ya kuvutia uwekezaji, kukuza biashara na kutangaza utalii. Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji wa mikataba hiyo kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu. Orodha ya mikataba na hati za makubaliano zilizosainiwa katika kipindi hicho ni kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho**.

#### **KURATIBU NA KUSIMAMIA MASUALA YA WATANZANIA WAISHIO UGHAIBUNI**

**106. *Mheshimiwa Spika*,** kwa kutambua Watanzania wanaoishi ughaibuni kama wadau muhimu wa maendeleo, Wizara yangu imeendelea kubuni mbinu mbalimbali za kuwashirikisha katika kuchangia maendeleo ya nchi. Moja ya mbinu hizo ni kuandaa makongamano ndani na nje ya nchi ambapo mwezi Agosti 2017, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliandaa Kongamano la Nne

la Diaspora liliowakutanisha Watanzania zaidi ya 200 kutoka nchi mbalimbali na wadau wa maendeleo hapa nchini. Kupitia kongamano hilo, Diaspora walihimizwa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa letu kwa kuhamasisha uwekezaji wa mitaji kutoka nje.

**107. *Mheshimiwa Spika*,** mwezi Aprili 2018 liliifanyika kongamano lingine lillioandaliwa na Diaspora jijini Dallas Marekani, ambalo pamoja na masuala mengine, lilitenga kutangaza vivutio vya utalii nchini pamoja na kuhamasisha wawekezaji kwenye sekta mbalimbali ikiwemo utalii.

**108. *Mheshimiwa Spika*,** mchango wa Diaspora katika maendeleo ya nchi unajidhihirisha katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii. Yafuatayo ni baadhi ya maeneo hayo:

- i. Diaspora imenunua nyumba zenyе thamani ya Shillingi bilioni 29.7 kutoka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa ajili ya nyumba za makazi, ofisi, maeneo ya biashara na viwanja mbalimbali kati ya mwaka 2011 hadi 2017.
- ii. Takwimu za Benki Kuu ya Tanzania zinaonesha kuwa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita 2013-2017, Diaspora kwa ujumla wao walituma nchini kiasi kisichopungua Dola za Marekani bilioni 2.3.
- iii. Timu ya madaktari wa kitanzania waishio Marekani kupitia taasisi.ya afya, elimu na maendeleo (Head Inc.) ilitoa huduma ya afya bila malipo na vifaatiba katika hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar, vyenye thamani ya zaidi ya shillingi bilioni moja;
- iv. Jumuiya ya Watanzania nchini Marekani (DICOTA) ilianda jukwaa la afya mwezi Novemba 2017 ambalo lilihudhuriwa na wataalam wa afya zaidi ya 130 kutoka Tanzania na Marekani ili kubadilishana ujuzi, usoefu na kutathmini njia madhubuti za kuendeleza sekta ya afya nchini Tanzania. Juhudi hizi ziliwezesha kupatikana kwa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi na wafanyakazi zaidi ya 60 kutoka vyuo vikuu na

hospitali nchini ikiwemo Chuo Kikuu cha Tiba KCMC, Hubert Kairuki, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na hospitali ya Bugando.

- v. Aidha, Dkt. Frank Minja mtanzania mtaalam wa Radiolojia wa Chuo Kikuu cha Yale Marekani amesaidia kuimarisha mfumo wa teknolojia ya kisasa ya radiolojia katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

**109.** *Mheshimiwa Spika*, wakati ambapo kipaumbele cha kitaifa ni viwanda, tunahitaji kufikiria ujuzi maalum walionao Watanzania wanaoishi katika Diaspora, na vile vile mchango wa kifedha ambao wanaweza kuchangia kutoka kwenye vyanzo vyao binafsi au kwa kushirikiana na raia wa nje, mabenki na taasisi nyingine za nje. Ili kuwezesha viwanda vyetu kuza nje, tunahitaji kutambua, kupima na kupenya katika masoko mbalimbali ya kigeni. Watanzania walioishi nchi za kigeni na watoto wao wanaweza kuchangia zaidi kutockana na ujuzi wao kwa kupata masoko kwa kutumia ujuzi wao wa lugha za kigeni.

**110.** *Mheshimiwa Spika*, watanzania wengi walio Diaspora wanachangia sana maendeleo ya kijamii na uchumi wa familia zao na Tanzania kwa ujumla, na wako tayari kushiriki katika jukumu kubwa la kujenga uchumi wa Taifa hili. Pengine tunahitaji kuwa na mfumo wa kisheria na sera ya kutoa huduma hiyo kwa uhalali na uhakika.

## **TATHMINI YA HALI YA DUNIA**

### **Hali ya usalama**

**111.** *Mheshimiwa Spika*, hali ya usalama duniani imeendelea kuimarika pamoja na kwamba changamoto kadhaa zimeendelea kuwepo katika baadhi ya maeneo. Changamoto hizo ni pamoja na migogoro ya kisiasa katika baadhi ya nchi, matukio ya kigaidi na kuongezeka makundi yenye itikadi kali na athari za kiusalama zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Tanzania imeendelea kuunga mkono

jitihada za kikanda na za Umoja wa Mataifa za kuimarisha amani na usalama duniani.

**112.** *Mheshimiwa Spika*, kuhusu migogoro ya kisiasa katika baadhi ya nchi, naomba nitumie fursa hii kuizungumzia kama ifuatavyo:

#### **Lesotho**

**113.** *Mheshimiwa Spika*, hali ya siasa, ulinzi na usalama nchini Lesotho bado hairidhishi. SADC ilituma misheni maalum ya ulinzi wa amani ili kusaidia nchi hiyo kutekeleza maazimio ya kurejesha amani. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kuwa misheni hiyo ilizinduliwa rasmi tarehe 2 Desemba 2017 na ina jumla ya maafisa 269. Serikali ya Lesotho imetakiwa kutekeleza maazimio yanayohusu maboresho ya mifumo ya Serikali kwa kipindi cha mwaka mmoja.

#### **Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo**

**114.** *Mheshimiwa Spika*, hali ya ulinzi na usalama nchini DRC hairidhishi. Hivi sasa Serikali ya nchi hiyo inaendelea na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ambaa umepangwa kufanyika tarehe 23 Desemba 2018. Maandalizi ya uchaguzi huu yanaendelea vizuri ikiwa ni pamoja na kukamilika kwa zoezi la kuandikisha wapiga kura na kuitisha sheria mpya ya uchaguzi. Natoa rai kwa wadau wa ndani na nje kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa utulivu kama ulivyopangwa. Hata hivyo, DRC inahitaji kusaidiwa kwa hali na mali katika kuandaa uchaguzi huo hususan ikizingatiwa kuwa nchi hiyo ni kuliko nchi yoyote Barani Afrika.

#### **Madagascar**

**115.** *Mheshimiwa Spika*, hali ya siasa nchini Madagascar hairidhishi na SADC imetuma ujumbe wa Baraza la ushauri la masuala ya uchaguzi nchini humo ili kufanya tathmini ya utayari wa nchi hiyo kufanya uchaguzi mkuu Novemba 2018. Aidha, SADC ilimtuma Mheshimiwa Joaquim Chissano, Rais Mstaafu wa Msumbiji na mjumbe maalum wa SADC tarehe 8 hadi 13

Mei 2018 kwa lengo la kusaidia kuweka mazingira ya amani kabla ya uchaguzi mkuu.

### **Sudan Kusini**

**116.** *Mheshimiwa Spika*, hali ya usalama nchini Sudan Kusini imeendelea kuwa ya wasiwasi kutokana na uhasama kati ya Serikali na upinzani. Aidha, hatua ya waliokuwa viongozi wa juu wa jeshi la nchi hiyo kuamua kuunda vikundi vya uasi imezidi kuchochea mgogoro huo. Hadi sasa mgogoro huo umesababisha zaidi ya watu milioni mbili kukimbilia nchi jirani na wengine zaidi ya 230,000 kulazimika kuyakimbia makazi yao na kuhifadhiwa kwenye makambi ya Umoja wa Mataifa nchini humo.

**117.** *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa mkataba wa mwezi Agosti 2015 wa kugawana madaraka umeendelea kusuasua licha ya jitihada za Jumuiya ya Maendeleo ya IGAD za mwaka 2017 za kufufua utekelezaji wa makubaliano hayo. Jumuiya ya Afrika Mashariki, Umoja wa Mataifa na Umoja wa Ulaya zinaendelea kutafuta suluhu ya kudumu ya mgogoro huo. Tanzania inaunga mkono jitihada zote zinazofanywa kutafuta suluhu ya kudumu nchini humo.

### **Somalia**

**118.** *Mheshimiwa Spika*, hali ya usalama na siasa nchini Somalia inaendelea kuimarka baada ya kuwa na Katiba mpya na uchaguzi wa Bunge kufanyika. Kwa kuititia jitihada kubwa za Jeshi la Serikali ya Somalia kwa kushirikiana na AMISOM, Serikali imerezesa zaidi ya asilimia 80 ya maeneo yaliyokuwa yanashikiliwa na kikundi cha kigaidi cha al-Shabaab. Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo kikundi hicho kimeendelea kuwa ni kikwazo cha kuleta amani nchini humo.

**119.** *Mheshimiwa Spika*, kwa upande mwingine majeshi ya AMISOM yameanza kuondoa askari wake na kuhamasisha Jeshi la Somalia kuanza kuchukua jukumu la kuliinda usalama wa nchi yake. Katika kipindi cha mwezi Oktoba na Desemba

2017, jumla ya askari 1,000 wa AMISOM waliondolewa na kurudishwa katika nchi zao. Tanzania inaitakia Serikali ya Somalia na watu wake mafanikio katika mipango ya kurejesha na kuimarisha amani na usalama nchini humo.

### **Libya**

**120.** *Mheshimiwa Spika*, hali ya amani na usalama nchini Libya ni tete. Hali hiyo imechangiwa na Dola kukosa udhibiti wa nchi, kuongezeka kwa makundi yanayokinzana na kukwama kwa mazungumzo ya amani. Tanzania inaunga mkono juhudzi za kimataifa zinazoendelea kupitia Umoja wa Afrika za kuupatia ufumbuzi mgogoro huo.

**121.** *Mheshimiwa Spika*, siku za hivi karibuni, imeripotiwa kuibuka kwa biashara haramu ya binadamu na utumwa katika baadhi ya maeneo nchini Libya. Tanzania inalaani kwa nguvu zote kuwepo kwa biashara hiyo na kuitaka jumuiya ya kimataifa kuchukua hatua stahiki kwa wale waliohusika.

### **Burundi**

**122.** *Mheshimiwa Spika*, kuhusu mgogoro wa kisiasa nchini Burundi napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba jitihada kubwa zinazofanywa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, chini ya usuluhishi wa Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Uganda akisaidiwa na Mwezeshaji Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimesaidia kurejesha hali ya amani na utulivu nchini Burundi tofauti na ilivyokuwa mwaka 2015 mgogoro huo ulipoibuka.

**123.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu na kushiriki katika mazungumzo ya kutatua mgogoro wa kisiasa nchini Burundi uliofanyika Arusha, mwezi Novemba 2017. Mazungumzo hayo yalijumuisha.Serikali.ya.Jamhuri ya Burundi na makundi yanayohusika na mgogoro huo wakiwemo wanasiasa, Marais wastaafu, viongozi wa dini, vyama vyasiasa na vyama vyasakiraia.

## Syria

**124.** *Mheshimiwa Spika*, mgogoro wa Syria bado unaendelea kuwa moja kati ya ajenda muhimu kwenye jumuiya ya kimataifa. Mgogoro huo unazidi kuwa mgumu kutokana na mvutano wa mataifa makubwa. Tunayasihi mataifa yanayohusika na mgogoro huo kushirikiana ili kurejesha amani nchini humo kwa njia ya mazungumzo. Hii inatokana na ukweli kwamba vita vinavyoendelea baina ya makundi mbalimbali yanayoungwa mkono na nchi za kigeni huzidisha uhasama na kusababisha hasara kubwa kwa maisha ya binadamu wasio na hatia pamoja na uharibifu wa miundombinu ya nchi hiyo.

## Yemen

**125.** *Mheshimiwa Spika*, Tanzania ina imani kwamba wananchi wa Yemen wana haki ya kujiamulia mustakabali wa nchi yao. Kutokana na mgogoro huo idadi ya vifo, raia wanaokimbia nchi yao na wanaopoteza makazi inazidi kuongezeka. Tanzania inaamini kuwa mgogoro huu unaweza kupatiwa suluhu kwa pande zinazohasimiana kukaa pamoja na inaunga mkono juhudzi za usuluhisho wa mgogoro huo, kupitia jumuiya za kimataifa.

## Iran

**126.** *Mheshimiwa Spika*, mwaka 2015 nchi wanachama wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na Ujerumanzi ziliingia makubaliano na Iran kuhusu mpango wake wa nyuklia ili kuondolewa vikwazo vyia kiuchumi. Mkataba huo ulitoa matumaini ya ushirikiano wa kimataifa katika juhudzi za kuondokana na silaha za nyuklia. Hata hivyo mwanzoni mwa mwezi Mei 2018, mmojawapo wa wadau wakuu ametangaza kujitua katika mkataba huo. Tanzania inazisihi pande zote zinazohusika kuendelea kuheshimu mkataba huo na kama kuna dosari katika mkataba huo zitatuliwe kwa njia ya mazungumzo.

## Rasi ya Korea

**127.** *Mheshimiwa Spika*, Rasi ya Korea ni miongoni mwa maeneo yenye historia ya mgogoro wa muda mrefu na kutishia hali ya amani na usalama duniani. Hata hivyo, hali hiyo imeanza kubadilika kufuatia tukio la kihistoria lililosuhudiwa mwezi Aprili 2018 wakati Marais wa Korea Kaskazini na Korea Kusini walipokutana katika eneo la mpaka wa nchi hizo (Demilitarized Zone) baada ya zaidi ya miaka 50 ya uhasama. Marais hao walikutana kujadili namna ya kumaliza tofauti zao na kushirikiana. Aidha, mukutano huo umefanyika baada ya miaka 10 tangu viongozi watangulizi wa nchi hizo mbili, Rais Kim Jong Il na Rais Roh Moo-hyun kukutana mwaka 2007.

**128.** *Mheshimiwa Spika*, baada ya Rais wa Jamhuri ya Korea Moon Jae-in kuingia madarakani mwaka 2017, moja ya agenda za serikali yake ilikuwa ni kukaa katika meza ya majadiliano na Korea ya Kaskazini ili kutafuta suhuu. Nia hiyo njema ya kiongozi huyo iliimarishwa na hotuba ya Rais wa Korea Kaskazini ya mwaka mpya 2018, ambapo alimtakia heri na mafanikio Rais wa Korea Kusini katika kuwa mwenyeji wa mashindano ya olimpiki ya majira ya baridi ya Februari 2018. Baada ya salamu hizo Rais wa Korea Kusini alimwalikia mwenzake kushiriki ufunguzi pamoja na kutuma timu kushiriki katika mashindano hayo. Mwanzo huo mzuri ulizaa matunda na dunia iliendelea kushuhudia mazungumzo mbalimbali katika ngazi za juu za Maofisa wa usalama wa nchi hizo mbili na hatimaye mukutano huu wa kihistoria.

**129.** *Mheshimiwa Spika*, Tanzania kama nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa, ambayo imekuwa ikichangia sana katika harakati za kuimarisha amani na usalama duniani, na kusimamia suluhu ya migogoro kupitia mazungumzo inapongeza kwa dhati hatua hii ambayo imeonesha umuhimu wa diplomasia katika kutatua migogoro kwa njia ya mazungumzo. Dunia inasubiri kwa hamu matokeo ya mazungumzo kati ya Rais Donald Trump wa Marekani na rais Kim Jong-un wa Korea ya Kaskazini yatakayofanyika baadae mwaka huu.

## Bahari ya Kusini ya China (South China Sea)

**130.** *Mheshimiwa Spika*, Tanzania imekuwa ikifuatilia kwa makini hali ya usalama katika Bahari ya Kusini ya China na visiwa vyake. Tunaunga mkono msimamo wa China unaotaka pawe na mazungumzo baina ya nchi zinazohusika katika kutatua mgogoro na kuondoa tofauti zilizopo kati ya nchi hizo kwa mazungumzo ili kufikia suluhu kwa njia ya amani.

## Nchi za Ghuba

**131.** *Mheshimiwa Spika*, Tanzania inafuatilia kwa makini mwelekeo wa siasa na tofauti zilizopo katika nchi za ghuba, hususan Saudi Arabia, Falme za Kiarabu, Bahrain na Misri kwa upande moja na Qatar kwa upande mwingine, nchi zote hizi zina uhusiano mzuri na Tanzania. Nchi hizi zina rasilimali kubwa ya mafuta na gesi ambayo ni muhimu kwa uchumi wao na dunia kwa ujumla. Tanzania inazisihi nchi hizi ambazo ni muhimu kwa amani na uchumi wa dunia kuzungumza na kufikia muafaka wa tofauti zao kwa amani.

## Hali ya Uchumi

**132.** *Mheshimiwa Spika*, uchumi wa dunia umeendelea kuimarika ambapo kwa sasa unakadiriwa kukua kwa asilimia 3 ikilinganishwa na asilimia 2.4 mwaka 2016. Ukuaji huo umechangiwa zaidi na kuimarika kwa uchumi wa mataifa yaliyoendelea, uwekezaji wa mitaji kwenye nchi zinazoibukia kiuchumi, pamoja na kupanda kwa bei za bidhaa. Hali hii inatoa matumaini ya kuimarika kwa biashara ya bidhaa hususan kutoka nchi zinazoendelea.

**133.** *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Afrika, shughuli za kiuchumi zimeendelea kuimarika zikisaidiwa kwa kiasi kikubwa na kuimarika kwa uchumi wa mataifa yaliyoendelea pamoja na masoko yanayoibukia. Uchumi wa Afrika unakadiriwa kukua kwa asilimia 3.1 mwaka 2018 kutoka asilimia 1.5 mwaka 2016. Ukuaji huu unatarajiwa kuendelea kutokana na kuimarika kwa hali ya soko la fedha la nje (external

financial market conditions). Hali hii itasaidia kuongezeka kwa uwekezaji katika miundombinu ya kimkakati kama vile reli, bandari na barabara. Hata hivyo, ukuaji wa uchumi katika Afrika unatarajija kuwa na viwango tofauti ambapo nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatarajija kuendelea kuimarika zaidi. Aidha, Tanzania inatarajija kuendelea kuwa kinara katika ukuaji wa uchumi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na hata katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

**134. *Mheshimiwa Spika*,** hali hii nzuri ya ukuaji kiuchumi kwa ujumla wake, unaweza kuathiriwa na baadhi ya matatizo ya kimfumo hususan kwenye sekta ya fedha na kodi. Jumuiya ya kimataifa inapaswa kuweka mfumo mahsus wa ushirikiano wa masuala ya kodi kwa ajili ya kuondoa ushindani wa kukusanya kodi na kuyalazimisha makampuni ya kimataifa kulipa kodi stahiki kwenye nchi yanapowekeza. Aidha, Tanzania inahamasisha ushirikiano madhubuti wa kimataifa kwa ajili ya kukabiliana na uhamishwaji haramu wa fedha ili kupambana na vitendo vya rushwa vya kimataifa. Kwa sasa thamani ya fedha zinazohamishwa kutoka nchi zinazoendelea kwenda nchi tajiri ni kubwa kuliko thamani ya misaada ya maendeleo inayotolewa kwa nchi zinazoendelea hivyo ni muhimu kuwa na mkakati wa pamoja kudhibiti uhalifu huu unaokwamisha jitihada za maendeleo Afrika na kwingineko. Changamoto hizi zinahitaji ushirikiano wa kimataifa kuzitatua na kuimarisha mifumo ya kisiasa na kiusalama ili kuweka mazingira mazuri ya kujenga uchumi imara kwa watu wote.

**135. *Mheshimiwa Spika*,** tangu kuanzishwa kwake Shirika la Biashara Duniani (WTO), limekuwa muhimili mkubwa katika kuhakikisha biashara duniani zinaendeshwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizojadiliwa na kukubalika na nchi zote wanachama. Kama leo hii pasingekuwepo na WTO ili kusimamia uendeshaji wa biashara na hasa kulinda maslahi ya nchi zinazoendelea kama Tanzania, dunia ingekuwa siyo mahali salama pakufanya biashara. Migogoro na mivutano ya kibiasahara ingekuwa mingei na ingezorotesha maendeleo.

**136.** *Mheshimiwa Spika*, hivi sasa Shirika hili linapitia changamoto zinazotishia uwepo wake na ustawi wa biashara duniani tangu kuanzishwa kwake miaka zaidi ya 20 iliyopita. Hali hii inasababishwa na kuongezeka kwa maamuzi ya nchi moja moja (unilateralism) badala ya kuzingatia misingi ya kuamua kwa pamoja (multilateralism) iliyojengwa na WTO. Nchi zinazoendelea zikiruhusu hili, zitakuwa za kwanza kuangamia. Natoa wito kwa nchi zote hususan zilizoendelea kuhestimu na kulinda misingi ya ushirikiano wa kimataifa katika kufanya maamuzi ya biashara duniani. Pale panapotokea sintofahamu, ni vizuri kufuata taratibu za usuluhishi za kimataifa zinazokubalika.

**137.** *Mheshimiwa Spika*, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania itaendelea kusimamia na kutetea misingi ya ushirikiano wa kimataifa katika kufikia maamuzi yanayohusu mustakabali wa dunia kwenye nyanja zote.

### **TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA**

**138.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara inasimamia taasisi tatu ambazo ni Chuo cha Diplomasia, Taasisi ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha, ambacho pia kinasimamia Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kilichopo Dar es Salaam. Naomba nichukue fursa hii kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo kama ifuatavyo:

#### **Chuo cha Diplomasia**

**139.** *Mheshimiwa Spika*, Chuo kimeendelea kutekeleza majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kushauri Wizara katika masuala ya diplomasia na uhusiano wa kimataifa. Mafunzo yanayotolewa chuongi hapo yamejikita zaidi katika programu ya diplomasia ya uchumi ili kwenda sambamba na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kufanya mageuzi ya uchumi wa Tanzania kuwa wa viwanda.

**140.** *Mheshimiwa Spika*, katika kujiimarisha, Chuo

kinaktekeleza mradi wa upanuzi na uboreshaji wa miundombinu yake ili kuongeza udahili wa wanafunzi. Madhumuni ya hatua hizi ni kutoa nafasi zaidi ya elimu kwa umma na kukiongezea chuo mapato na hatimaye kupunguza utegemezi wa fedha za uendeshaji kutoka Serikalini. Katika kufanikisha hilo, Wizara inaendelea kutenga fedha zaidi kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya chuo hicho.

### **Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha**

**141.** *Mheshimiwa Spika*, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) kimeendelea kuwa kitovu cha diplomasia ya mikutano hapa nchini na kuchangia katika kukuza uchumi. Hadi kufikia mwezi Machi 2018 Kituo kilikuwa mwenyeji wa mikutano **257** ambapo kati ya hiyo, mikutano **57** ni ya kimataifa na **200** ya kitaifa ambayo imeingiza jumla ya **Shilingi 2,036,218,423**.

**142.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi.cha.mwaka wa fedha 2018/19, Kituo.kimepanga.kuingiza.mapato ya **Shilingi 16,743,620,893**. Kati ya fedha hizo, Shilingi 15,587,877,637 nikutoka vyanzo mbalimbali vya ndani; na **Shilingi 1,155,743,256** zitatokana na mkopo. Aidha, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) kinategemewa kuingiza kiasi cha **Shilingi 3,338,800,000**.

**143.** *Mheshimiwa Spika*, Kituo cha AICC kinategemea kukopa **Shilingi 1,155,000,000** kwa ajili ya mradi wa upanuzi wa Hospitali ya AICC. Aidha, kituo kinaendelea kufanya taratibu za kuwezesha ujenzi wa kituo mahsusini cha mikutano kitakachoitwa Mt. Kilimanjaro International Convention Centre (MK-ICC). Kituo hicho ndicho kitakachokuwa suluhisho la utekelezaji wa diplomasia ya mikutano ya kimataifa na maonesho hapa nchini. Vilevile, Kituo kimeiomba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupatiwa eneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mikutano jijini Dodoma.

## **Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika (APRM)**

**144.** *Mheshimiwa Spika*, APRM ni mpango wa nchi za Afrika wa kujitathmini katika masuala ya utawala bora. Tanzania ilijunga na Mpango huo mwaka 2004, na uliridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2005. Lengo la APRM ni kuziwezesha nchi za Afrika kuimarisha utawala bora kwa kushirikisha wananchi wake kubainisha changamoto na kuzigeuza kuwa fursa za maendeleo ili kubaini mambo mazuri ya kuendelezwa kwa faida ya nchi yenye na hata kuwa mfano wa kuigwa na nchi nyingine.

**145.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, APRM Tanzania illendelea kutekeleza shughuli zilizopangwa kwenye mpangokazi kama ifuatavyo:

- (i) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi wa APRM kwa ufadhili wa jumla ya Dola za Marekani 100,000 kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) Tanzania;
- (ii) Kusimamia uzinduzi wa Ripoti ya nchi uliofanywa tarehe 19 Julai 2017 na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (iii) Kufanya warsha ya kuwajengea uwezo watendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuunganisha mipango ya maendeleo ya nchi pamoja na mpangokazi wa APRM;
- (iv) Kushiriki mikutano ya APRM kulingana na Mkataba wa Makubaliano wa kuijunga na APRM; na
- (v) Kuendelea kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu utekelezaji wa shughuli za APRM.

**146.** *Mheshimiwa Spika*, kwa kutambua.umuhimu wa misingi ya utawala bora, Wizara yangu itaendelea kuiwezesha APRM kutekeleza majukumu yake.

### **UTAWALA NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU**

**147.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara ina jumla ya watumishi 456 wa kada mbalimbali. Kati ya hao, 347 wapo Makao Makuu ya Wizara na 109 wapo katika Balozi zetu nje ya nchi.

#### **Ajira Mpya**

**148.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/18, Wizara ilipata kibali cha kuajiri watumishi 10 wa kada mbalimbali ambapo hadi sasa watumishi 5 tayari wameripoti kazini na watumishi 5 taratibu za ajira zao zinaendelea.

#### **Upandishaji vyeo watumishi**

**149.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/18, Wizara imepata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora cha kuwapandisha vyeo watumishi 97. Taratibu za kuwapandisha vyeo watumishi hao zinaendelea kukamilishwa.

#### **Uteuzi**

**150.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/18, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa mabalozi watano ambapo kati yao watatu wamepangia vituo na wawili taratibu za kuwapangia vituo zinaendelea.

#### **Mafunzo**

**151.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo Watumishi kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi. Watumishi 31 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi 9 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya Uzamili. Aidha, Wizara ilipokea nafasi 5,220 za mafunzo kutoka nchi 27

wahisani na marafiki. Kati ya nafasi hizo mafunzo ya muda mfupi ni 4,650 na ya muda mrefu ni 570. Wizara iliratibu fursa hizo kwa kuzitangaza kwa umma wa watanzania kupitia vyombo vya habari, tovuti ya wizara, mitandao ya kijamii na nyingine ziliwasilishwa moja kwa moja kwenye Wizara na Idara za kisekta ili watanzania wenyewe sifa waweze kuomba nafasi hizo.

**152. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara iliandaa Semina Elekezi kwa Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki iliyofanyika mwezi Januari, 2018, Jijini Dar es Salaam. Lengo la Semina hiyo lilikuwa ni kuwajengea uelewa Waheshimiwa Wabunge hao katika masuala yatakayowawezesha kutekeleza majukumu yao, wakihakikisha kuwa wanawasilisha na kutetea hoja zenye manufaa na maslahi mapana kwa ustawi wa nchi yetu wakati wa mijadala ndani ya Bunge hilo.

**153. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 Wizara yangu imekabiliana na changamoto mbalimbali za kimfumo wa dunia, pamoja na zile za kiutendaji. Hata hivyo, pamoja na changamoto hizo Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi mkubwa kwa kuendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wote wa ndani na nje kuhakikisha kwamba malengo ya Serikali kwenye ushirikiano wa kimataifa yanatimia bila kujali uwepo wa changamoto hizo. Napenda kutumia fursa hii kuhimiza wadau kuendelea kushirikiana na Wizara yangu ili kwa pamoja tuweze kutimiza azma ya Serikali ya kukuza uchumi na kuboresha maisha ya wananchi wote.

## **SHUKRANI**

**154. *Mheshimiwa Spika*,** kwa namna ya pekee naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Mabalozi, Wawakilishi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa na Mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kupitia nchi na mashirika yao kufanikisha mipango mbalimbali ya maendeleo inayotekelizwa na Serikali.

**155.** *Mheshimiwa Spika*, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kupata mafanikio makubwa kutokana na mchango wa wadau na washirika wa maendeleo kutoka nchi na asasi mbalimbali za kitaifa, kikanda, kimataifa pamoja na sekta binafsi. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi za Afrika Kusini, Algeria, Australia, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Denmark, Finland, Hungary, India, Italia, Ireland, Israel, Iran, Japan, Korea Kusini, Kuwait, Malaysia, Marekani, Malta, Misri, Morocco, New Zealand, Norway, Oman, Pakistan, Palestina, Poland, Qatar, Saudi Arabia, Sweden, Singapore, Sri-Lanka, Thailand, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Uingereza, Ujeruman, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ureno, Urusi, Usvisi, Uturuki na Vietnam kwa kuchangia mafanikio hayo muhimu kwa Taifa.

**156.** *Mheshimiwa Spika*, shukrani ziwaendee pia Umoja wa Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *African Capacity Building Facility*, Benki ya Dunia, IAEA, Shirika la Fedha Duniani (IMF), *Investment Climate Facility for Africa*, UNDP na Mashirika mengine yote ya Umoja wa Mataifa, *TradeMark East Africa*, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika (BADEA), *The Association of European Parliamentarians with Africa*, WWF, *The Belinda and Bill gates Foundation*, *Global Fund*, *International Committee of the Red Cross*, *International Federation of the Red Cross and Red Crescent Societies*, *Medecins Sans Frontieres* pamoja na Mifuko na Mashirika mbalimbali ya Misaada. Ni dhahiri kuwa mafanikio tuliyoyapata yamechangiwa kwa misaada na ushirikiano wenu.

## **MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19**

**157.** *Mheshimiwa Spika*, kwa muhtasari mionganoni mwa malengo yaliyopangwa kutekelezwa na Wizara yangu katika mwaka wa Fedha 2018/19 ni pamoja na:

- i. Kuendelea kulinda na kutetea misingi ya Taifa;
- ii. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ikiweka msisitizo kwenye diplomasia ya uchumi kuelekea Tanzania ya viwanda;

- iii. Kuendelea kuvutia fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali, biashara pamoja na kutangaza vivutio vyatyalii;
- iv. Kuratibu Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano (JPC);
- v. Kufuatilia mwelekeo wa siasa na uchumi duniani na kutathmini matokeo yake kwa siasa ya mambo ya nje ya Tanzania;
- vi. Kuendelea kuratibu utekelezaji wa makubaliano ya kikanda na kimataifa ikiwemo agenda ya Umoja wa Afrika ya 2063; na agenda ya Umoja wa Mataifa ya 2030;
- vii. Kufuatilia fursa mbalimbali zinazotokana na ushiriki wa Tanzania katika mtangamano wa kikanda na mashirika ya kimataifa;
- viii. Kuendelea kuongeza uwakilishi wa Tanzania nje kwa kufungua Balozi mpya, Konseli Kuu, kutumia Konseli za Heshima sambamba na kuongeza umiliki wa nyumba za makazi ya watumishi na ofisi balozini;
- ix. Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa;
- x. Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa mikataba mbalimbali iliyosainiwa kati ya nchi yetu na nchi nyingine na kufuatilia ahadi mbalimbali zilizotolewa kwa nchi yetu na nchi wahisani na mashirika ya kimataifa;
- xi. Kuongeza mshikamano na jumuiya za watanzania wanaoishi ughaibuni na kuweka utaratibu madhubuti utakaowawezesha kuchangia kwenye maendeleo ya Taifa;
- xii. Kuendelea kushirikiana na Wizara, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na vyombo vyatyalii katika kuelimisha umma juu ya fursa mbalimbali

- zitokanazo na ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za kikanda na kimataifa;
- xiii. Kuendelea kutafuta nafasi za masomo, misaada na kushawishi nchi na mashirika kutufutia madeni; na
- xiv. Kuendelea kujenga uwezo wa watumishi Wizarani.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19**

**158.** *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka wa fedha 2018/19, Wizara yangu imetengewa bajeti ya kiasi cha **Shilingi 177,006,232,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 154,810,812,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 11,795,420,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 10,400,000,000** ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

**159.** *Mheshimiwa Spika*, katika bajeti ya matumizi mengineyo, **Shilingi 116,010,729,689** ni kwa ajili ya matumizi ya vifungu vya Balozini, **Shilingi 35,324,806,566** ni kwa ajili ya vifungu vya makao makuu ya Wizara, **Shilingi 1,077,362,234** ni kwa ajili ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala bora Tanzania, **Shilingi 1,000,000,000** ni kwa ajili ya fedha za matumizi mengineyo ya Chuo cha Diplomasia, **Shilingi 1,239,633,751** ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na **Shilingi 158,279,760** ni kwa ajili ya Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika.

**160.** *Mheshimiwa Spika*, katika fedha za bajeti ya maendeleo, kiasi cha **Shillingi 10,400,000,000** zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2018/19, kiasi cha **Shilingi 6,180,676,000** zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi ya ubalozi wa Tanzania Muscat, Oman; **Shilingi 1,819,324,000** ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi yaliyopo ubalozi wa Tanzania Khartoum, Sudan; na **Shilingi 2,400,000,000** ni kwa ajili ya upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya chuo cha diplomasia.

**161.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2018/19, Wizara kuitia balozi zake, inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi **28,564,158,100** ikiwa ni maduhuli ya Serikali.

## HITIMISHO

**162.** *Mheshimiwa Spika*, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 177,006,232,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 166,606,232,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 10,400,000,000** ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

**163.** *Mheshimiwa Spika*, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na waheshimiwa wabunge kwa kunisikiliza.

**164.** *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa niaba yake Mheshimiwa Mboni Mohamed Mhita. (*Makofii*)

**MHE. MBONI M. MHITA (K.n.y. MHE. MUSSA A. ZUNGU - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba taarifa hii iingie katika *Hansard* kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mchango wake wa dhati, kutupigania vijana wake na kuweza kushinda uchaguzi huu. Namshukuru vilevile Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu wa Bunge, *staff* wa Bunge na Wabunge wote kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki,

Mabalozi, timu nzima ya Wabunge wenzangu ambao ni wawakilishi wa Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2017/2018; pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019; na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(3) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Wizara hili ni mojawapo ya Wizara inayosimamiwa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimezipa jukumu Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 23 na 26 Machi, 2018. Katika kikao hicho, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama inavyoelekeza Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa lengo la kulinganisha na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii, kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019, taarifa ninayo iwasilisha inatoa maelezo kuhusu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, mapitio ya taarifa ya Wizara kuhusu uzingatiaji wa maoni yaliyotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, uchambuzi wa ukusanyaji wa maduhuli ikilinganishwa na lengo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018;

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, mapitio ya taarifa ya Wizara kuhusu upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge pamoja na utekelezaji wa majukumu na malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018;

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, uchambuzi wa majukumu na malengo yanayowekwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019;

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2018/2019; na

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, mapitio ya malengo ya bajeti na makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kulinganisha na makadirio ya fedha za matumizi yaliyowasilishwa na mtoa hoja mapema leo Bungeni ili liweze kujadili na kuamua kuhusu maombi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, ilihusu maeneo makuu mawili. Maeneo hayo ni uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati na mapitio ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Naomba kulijulisha Bunge lako hili kuwa, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina mambo yote mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakumbuka kuwa Bunge hili lilipokuwa linajadili hoja ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ilitoa ushauri katika jumla ya mambo makuu kumi na tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufuatilia uzingatiaji wa ushauri huo, tarehe 23 Machi, 2018 Waziri wa Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki alijulisha Kamati kuhusu utekelezaji wa ushauri huo. Naomba kulijulisha Bunge lako kwamba upo ushauri uliozingatiwa, upo unaoendelea kuzingatiwa na upo ushauri uliopewa uzito kidogo katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganoni mwa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu ufunguzi wa ofisi za Ubalozi au Balozi za Heshima katika nchi zenye uhusiano mkubwa wa kibiashara na Tanzania kama vile Lubumbashi *DRC*, Cuba na Guangzhou – China. Maelezo ya Waziri yalionesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga Sh.9,329,800,000 kwa ajili ya kufungua ubalozi mpya Cuba na Konseli (*Consular*) Kuu katika miji ya Lubumbashi – Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Guangzhou nchini China. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo inayoweza kuinufaisha nchi yetu kutohana na fursa mpya za kiuchumi na kibiashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri unaoendelea kufanyiwa kazi na ambao utekelezaji wake haujaanza ni pamoa na ujenzi wa ofisi ya Wizara kwa upande wa Zanzibar. Naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa, tarehe 31 Mei, 2017 wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii, Kamati ilishauri kwamba Serikali ifanye matengenezo makubwa au kujenga jengo jipya la ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki huko Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 23 Machi, 2018, Kamati ilipochambua taarifa ya Wizara hii, hakuna ukarabati wa jengo hilo au ujenzi wa jengo jipya kwa madhumuni hayo, uliokuwa umepangwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Waziri ilionesha kuwa bado mazungumzo yanaendelea baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu umiliki wa jengo linalotumiwa hivi sasa na Idara ya Mambo ya Nje ya Zanzibar. Ahadi iliyotolewa ni kwamba, mazungumzo yatakapokamilika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikipatiwa umiliki wa jengo husika, ukarabati utaanza mara moja. Ni maoni ya Kamati kuwa kasi ya kufanikisha mazungumzo hayo inapaswa kuongezwa na njia ya kujenga jengo lingine inaweza kutumika iwapo mazungumzo hayo hayatafanikisha azma ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla ushauri wa Kamati umefanyiwa kazi na uzingatiaji upo katika hatua mbalimbali. Hata hivyo, Kamati inasitisiza kuwa, kwa mambo ambayo uzingatiaji wake haujafikia hatua kubwa, ushauri wa Kamati unapaswa kupewa uzito stahiki. Kwa mfano, suala la kukamilisha Sera mpya ya Mambo ya Nje, inayopaswa kutoa dira na mwelekeo unaoendana na hali ya kisasa ya diplomasia ya uchumi duniani linapaswa kupewa uzito mkubwa zaidi kuliko ilivyo sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujulisha Bunge lako Tukufu kuwa taarifa iliyotolewa kwenye Kamati inaonesha kuwa hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa Rasimu ya Sera. Aidha, hatua inayofuata na ambayo haijaanza ni kuandaa mkakati wa utekelezaji wa sera iwapo itapitishwa ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, imepita takribani miaka 17 sasa tangu sera iliyopo ilipotungwa. Wakati huo Wizara haikuwa na jukumu la kushughulikia au kuratibu masuala ya mtangamano wa Afrika Mashariki. Kamati ina maoni kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza kasi ya kukamilisha mchakato wa sera hii na mkakati wake ili kuikamilisha kabla ya mwaka wa fedha 2019/2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa kuchambua hali ya ukusanyaji wa

mapato hadi mwezi Februari 2018 pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi tarehe 20 Machi, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara hii ilikuwa na lengo la kukusanya maduhuli ya Serikali kiasi cha shilingi bilioni ishirini na tano milioni mia saba sabini na tatu. Hata hivyo, Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Wizara ilikusanya jumla ya Sh.18,665,000,000/=, sawa na asilimia 72 ya lengo la ukusanyaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya ulinganisho wa hali ya ukusanyaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 hadi kufikia Februari, 2017. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Februari, 2017 makusanyo yalifikia asilimia 60.7 tofauti na asilimia 72.4 ya lengo kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018. Kamati ina maoni kwamba mwenendo huu wa ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa wa kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipochambua taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa 2017/2018 ilibaini kuwa hadi kufikia tarehe 20 Machi, 2018 Wizara ilipokea Sh.98,617,000,000/=, sawa na asilimia 65.38 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hali hiyo ni tofauti na Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Wizara ilipokea Sh.87,201,000,000/=, sawa na asilimia 56 ya bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha zilizopokelewa katika mwaka wa fedha 2017/2018, Sh.88,228,000,000/= zilikuwa za matumizi mengineyo, sawa na asilimia 66 ya Sh.133,424,000,000/= zilitengwa. Sh.7,468,000,000/= kwa ajili ya mishahara, sawa na asilimia 79 ya Sh.9,421,000,000/= zilitengwa na Sh.2,920,000,000/= zilikuwa za miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 36.5 ya Sh.8,000,000,000/= zilitengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kuwa asilimia kubwa ya fedha zilizopatikana kutoka Hazina

zilitumika kugharamia uendeshaji wa ofisi za balozi zetu nje ya nchi; safari za viongozi wa kitaifa nje ya nchi, ukarabati wa majengo ya Balozi zetu zilizopo Kampala, Kinshasa, Lilongwe na Brussels pamoja na utekelezaji wa majukumu mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo huu wa matumizi hautofautiani sana na mwelekeo ulivyokuwa kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017. Hata hivyo, bado kuna umuhimu mkubwa kwa Wizara kuititia vipaumbele vyake kabla ya kuanza matumizi ya fedha zinazopokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kueleza uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, napenda kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilielezwa miongozo 12 iliyozingatiwa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganoni mwa miongozo hiyo, ni Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, ambayo ina umri wa takribani miaka 17. Miongozo mingine ni pamoja na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021) na Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuia ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa zaidi kuwa Wizara imepanga malengo makuu 12 ya kibajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Mfano wa malengo hayo ni kuandaa Sera ya Taifa ya *Diaspora* itakayotoa mwongozo wa namna ya kuwashirikisha *Diaspora* wa Tanzania katika kuchangia maendeleo ya nchi yao. Lengo lingine ni kuratibu na kusimamia majadiliano ya Rasimu ya Andiko la Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki (*East Africa Political Federation*).

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba hakuna lengo mahsusila ukamilishaji wa mapitio ya Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje kwa wakati huu, ambapo Wizara itaratibu majadiliano kuhusu Andiko la Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki. Ni maoni

ya Kamati kuwa jambo hili linapaswa kupewa umuhimu kwa kiwango stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii, Kamati ilichambua makadirio ya ukusanyaji wa mapato yanayopendekezwa kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 na kubaini kuwa makadirio hayo yanatofautiana kidogo na lengo lilitilowekwa kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018. Katika mwaka wa fedha unaoisha, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya Sh.25,773,000,000/=, wakati kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara inalenga kukusanya kiasi cha Sh.28,564,000,000/=. Lengo hili la makusanyo limeongezeka kwa kiasi cha Sh.2,790,000,000/= sawa na asilimia 10.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi zaidi ulionesha kuwa ongezeko hilo lipo katika lengo la makusanyo ya balozi zetu za nje ya nchi ambapo zilitikuwa na lengo la kukusanya jumla ya Sh.25,672,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2017/2018; lakini kwa mwaka wa fedha 2018/2019 zinapewa lengo la kukusanya jumla ya Sh.28,448,000,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ililinganisha lengo la kukusanya mapato kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na mwenendo halisi wa ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ili kutathmini lengo la maduhuli linalopangwa kwa mwaka wa fedha unaofuata. Tathmini imeonesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2018, ni kiasi cha Sh.18,665,000,000/=, sawa na asilimia 72.7 kilikuwa kimekusanywa. Kwa mwenendo huo, kiasi cha lengo kilichobaki ni Sh.7,113,000,000/= sawa na asilimia 27.3 ambacho kinaweza kukusanywa kwa kipindi cha mwezi Machi hadi Juni, 2018. Kwa mwenendo huu, Kamati inaridhika kuwa lengo la mapato linalowekwa linaendana na hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijulishwa kuwa Wizara hii inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Sh.177,000,000,000/= ambapo Sh.154,000,000,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (*OC*) Sh. 11,795,000,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh.10,400,000,000 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa maombi hayo na kuona kuwa asilimia 87.5 ya makadirio hayo ni kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli, asilimia 6.7 ni kwa ajili ya mishahara na asilimia 5.1 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo kama inavyoonekana katika jedwali Na. 01 na *graph* Na. 01 na Na. 02 katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya ulinganisho katika Bajeti ya Mwaka 2017/2018 na Mwaka 2018/2019 kama inavyoolekeza Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika ulinganisho huo, Kamati ilibaini kuwa fedha zinazoombwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 zimeongezeka kwa asilimia 17.3 kutoka shilingi bilioni 150.8 zilizoidhinishwa mwaka 2017/2018 hadi shilingi bilioni 177 zinazoombwa kuidhinishwa na Bunge leo kama ilivyobainishwa katika Jedwali Namba 01.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipochambua zaidi ilibaini kuwa bajeti ya mishahara, bajeti ya matumizi mengineyo na bajeti ya miradi ya maendeleo imeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2017/2018. Bajeti ya mishahara imeongezeka kwa asilimia 25.2, bajeti ya matumizi mengineyo imeongezeka kwa asilimia 16 na bajeti ya maendeleo kwa asilimia 30. Pamoja na hivyo, sura ya uwiano wa bajeti iliyotengwa kwa vipengele hivyo vitatu kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019 haitofautiani sana kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01 na *Graph* Na. 01 pamoja na *Graph* Na. 02.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kuwa mwenendo huu wa uwiano wa bajeti utaendelezwa na hata kuboreshwa zaidi. Ni imani ya Kamati kuwa hata baada ya kuidhinisha makadirio haya, upatikanaji wa fedha utakuwa mzuri na unaozingatia namna Bunge linavyoidhinisha makadirio haya ya mapato na matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia dhamira ya Wizara ya kusimamia na kutekeleza diplomasia ambayo itachangia katika shughuli za kiuchumi na kuwezesha

mageuzi ya haraka na maendeleo endelevu ya Tanzania, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuataao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe fedha zote kiasi cha Sh.9,329,000,000/= ambazo zimetengwa kwa ajili ya kufungua ubalozi mpya huko Cuba na Konseli (*consular*) Kuu katika Miji ya Lubumbashi – Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo na Guangzhou ambayo ipo Nchini China, zinatolewa kwa wakati na kutumika kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini pesa hizo zikitolewa kwa ukamilifu zitawezesha ufunguzi wa ubalozi huo na Konseli kuu hizo na hatimaye nchi yetu kunufaika na fursa za kiuchumi na kibashara. Aidha, Serikali iweke mikakati zaidi ya kufungua Balozi au Balozi za Heshima katika nchi nyingine zinazoendelea kukua kwa kasi kiuchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kiwango cha fedha za bajeti zinazotolewa kwa Wizara kimekuwa hakiendani na mtiririko wa fedha uliopangwa, jambo ambalo linasababisha Wizara na balozi zake kutotekeliza ipasavyo majukumu yake ya msingi hususana Sera ya Mambo ya Nje inayoweka msisitizo wa diplomasia ya uchumi, Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazotengwa zinatolewa kwa kuzingatia mtiririko uliopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kiwanja kilichotolewa na Serikali ya Oman kwa ajili ya kujenga Ubalozi wa Tanzania Jijini Muscat hakijaendelezwa tangu kilipowekewa jiwe la msingi na Rais Mstaa fu wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2012, na kwa kuwa upo uwezekano wa kiwanja hicho kutwaliwa na Serikali ya nchi hiyo endapo kitaendelea kukaa bila kuendelezw, Serikali itoe shilingi bilioni moja milioni mia nane tisini na nne zilizokuwa zimetengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ubalozi kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Serikali itoe fedha za maendeleo

zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Ubalozi wetu wa Cairo, ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia, Dar es Salaam na ujenzi wa makazi ya Balozi, Addis Ababa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Serikali ilijiwekea mkakati wa miaka 15 (2001 - 2003 – 2016/2017) wa kuendeleza viwanja, kukarabati na kununua majengo ya ofisi na makazi ya watumishi balozini, mkakati huo haujatekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutoa kipaumbele katika kuendeleza viwanja 12 ambavyo baadhi yake ni vya muda mrefu (kama vile viwanja vilivyopo huko Maputo, London, Addis Ababa, Nairobi na Muscat); na kuboresha majengo ya ofisi na makazi ya watumishi katika Balozi zetu ikibidi kwa kutumia mikopo ya muda mrefu lakini yenyе riba nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia Serikali kuokoa fedha nyingi za walipa kodi zinazotumika kwa ajili ya kukodi majengo ya ofisi na makazi katika Balozi zetu nje ya nchi; ambapo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Sh. 21,667,000,000/ = zimetengwa kwa ajili hiyo. Sambamba na hilo, hii itawezesha Serikali kujenga majengo ya kisasa ya balozi zetu ambayo yakikamilika yataingiza fedha nyingi za kuendesha Balozi hizo na kusitisha utaratibu wa kupanga ofisi na nyumba za watumishi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati imebaini kuwa utaratibu huo ni wenye tija na mafanikio makubwa kama vile inavyoonekana katika Ubalozi wa Maputo – Msumbiji ambako kwa mwaka ujao wa fedha wa 2018/2019 hawatahitaji na hawakupangiwa fedha za pango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara imekubaliana na ushauri wa Kamati wa kupanga miradi michache itakayoweza kutekelezwa kwa mwaka na hatimaye kuweka miradi mitatu tu ya maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha 2018/2019, Serikali ihakikishe kuwa inaipatia fedha miradi hiyo, hususan ule wa ujenzi wa Ofisi

ya Ubalozi wa Muscat, Oman ambako Serikali inaweza kukusanya fedha nyingi za maduhuli kwa miaka ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga; Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Susan Alphonse Kolumba; Katibu Mkuu, Profesa Mkenda; Naibu Katibu Mkuu, Balozi Ramadhan Muombwa; pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakin si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru sana Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi bi. Angelina Sanga; na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhan Abdallah na bi. Grace Bidya wakisaidiwa na bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA  
NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI  
YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA  
AFRIKA MASHARIKI (FUNGU 34) KWA MWAKA WA FEDHA  
2017/2018; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA  
HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## **SEHEMU YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, [Kanuni za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, na kuliomba Bunge lako tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Bunge, Wizara hii ni mojawapo ya Wizara inayosimamiwa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimezipa jukumu Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 23 na 26 Machi, 2018.

**Mheshimiwa Spika**, katika kikao hicho, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa

Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama inavyoelekeza Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge kwa lengo la kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Taarifa ninayoiwasilisha inatoa maelezo kuhusu:-

- i) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu uzingatiaji wa maoni yaliyotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
- ii) Uchambuzi wa ukusanyaji wa maduhuli ikilinganishwa na lengo liliowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
- iii) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge pamoja na utekelezaji wa majukumu na malengo ya bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
- iv) Uchambuzi wa majukumu na malengo yanayowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
- v) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na
- vi) Mapitio ya Malengo ya bajeti na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, lengo ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kulinganisha na Makadirio ya fedha za matumizi yaliyowasilishwa na mtoa hoja mapema leo ili Bunge liweze kujadili na kuamua kuhusu Maombi ya Wizara hii.

## **SEHEMU YA PILI**

### **MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ilihusu maeneo makuu mawili. Maeneo hayo ni Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati na Mapitio ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Naomba kulijulisha Bunge hili kuwa, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina mambo yote mawili kama ifuatavyo:-

#### **Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, tutakumbuka kuwa Bunge hili lilipokuwa linajadili hoja ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Kamati ilitoa ushauri katika jumla ya mambo makuu kumi na tano katika kufuatilia uzingatiaji wa ushauri huo, tarehe 23 Machi, 2018 Waziri wa Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki alijulisha Kamati kuhusu utekelezaji wa ushauri huo. Naomba kulijulisha Bunge kwamba upo ushauri uliozingatiwa, upo unaoendelea kuzingatiwa na upo ushauri uliopewa uzito kidogo katika utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, mionganini mwa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu ufunguzi wa Ofisi za ubalozi au Balozi za heshima katika nchi zenyehusiano mkubwa wa kibashara na Tanzania kama vile Lubumbashi DRC, Cuba

na Guangzhou – China. Maelezo ya Waziri yalionesha kuwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Serikali imetenga shilingi 9,329,800,000/= kwa ajili ya kufungua ubalozi mpya Cuba na Konseli kuu katika miji ya Lubumbashi – Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Guangzhou – China. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo inayoweza kuinuifaisha nchi yetu kutohana na fursa mpya za kiuchumi na kibiashara.

**Mheshimiwa Spika**, ushauri unaoendelea kufanyiwa kazi na ambao utekelezaji wake haujaanza ni pamoja na ujenzi wa Ofisi ya Wizara kwa upande wa Zanzibar. Naomba kulikumbusha Bunge lako tukufu kuwa, tarehe 31 Mei, 2017 wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii, Kamati ilishauri kwamba Serikali ifanye matengenezo makubwa au kujenga jengo jipya la Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki huko Zanzibar. Hadi kufikia tarehe 23 Machi, 2018 wakati Kamati ilipochambua Taarifa ya Wizara hii, hakuna ukarabati wa jengo hilo au ujenzi wa jengo jipya kwa madhumuni hayo, uliokuwa umepangwa.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Waziri ilionesha kuwa bado mazungumzo yanaendelea baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu umiliki wa jengo linalotumiwa hivi sasa na Idara ya Mambo ya Nje Zanzibar. Ahadi iliyotolewa ni kwamba, mazungumzo yatakapokamilika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikipatiwa umiliki wa jengo husika, ukarabati utaanza mara moja. Ni maoni ya Kamati kuwa kasi ya kufanikisha mazungumzo hayo inapaswa kuongezwa na njia ya kujenga jengo lingine inaweza kutumika iwapo mazungumzo hayo hayatafanikisha azma ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla ushauri wa Kamati umefanyiwa kazi na uzingatiaji upo katika hatua mbalimbali. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa, kwa mambo ambayo uzingatiaji wake haujafikia hatua kubwa, ushauri wa Kamati unapaswa kupewa uzito stahiki. Kwa mfano, suala la kukamilisha Sera mpya ya Mambo ya Nje, inayopaswa kutoa

dira na mwelekeo unaoendana na hali ya kisasa ya Diplomasia ya Uchumi duniani, linapaswa kupewa uzito mkubwa zaidi kuliko ilivyo sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Taarifa iliyotolewa kwenye Kamati inaonesha kuwa hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa Rasimu ya Sera. Aidha, hatua inayofuata na ambayo haijaanza ni kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera iwapo itapitishwa ndani ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, imepita takribani miaka kumi na saba sasa tangu Sera iliyopo ilipotungwa. Wakati huo Wizara haikuwa na jukumu la kushughulikia au kuratibu masuala ya mtangamano wa Afrika Mashariki. Kamati ina maoni kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza kasi ya kukamilisha mchakato wa Sera hii na mkakati wake ili kuikamilisha kabla ya Mwaka wa Fedha 2019/2020.

### **Uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa kuchambua hali ya ukusanyaji wa mapato hadi mwezi Februari 2018 pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi tarehe 20 Machi, 2018.

#### **Ukusanyaji wa maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara hii ilikuwa na lengo la kukusanya maduhuli ya Serikali kiasi cha shilingi **25,773,820,000/=**. Hata hivyo, Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Wizara ilikusanya Jumla ya shilingi **18,665,002,685.57/=** sawa na **asilimia 72.4** ya lengo la ukusanyaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ulinganisho wa hali ya ukusanyaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 hadi

kufikia Februari, 2017. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa katika kipindi cha Julai 2016 hadi Februari, 2017 makusanyo yalifkia **asilimia 60.7** tofauti na **asilimia 72.4** ya lengo kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Februari, 2018. Kamati ina maoni kwamba mwenendo huu wa ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa wa kuridhisha.

### **Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipochambua Taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2017/2018 ilibaini kuwa hadi kufikia tarehe 20 Machi, 2018 Wizara ilipokea **Shilingi 98,617,704,687.20** sawa na **asilimia 65.38** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu. Hali hiyo ni tofauti na Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Wizara ilipokea **Shilingi 87,201,012,183.00** sawa na **asilimia 56** ya Bajeti illyokuwa imeidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha zilizopokelewa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, **Shilingi 88,228,634,384.20** zilikuwa za Matumizi Mengineyo sawa na **asilimia 66** ya **Shilingi 133,424,290,000.00** zilizotengwa, **Shilingi 7,468,874,648.00** kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 79** ya Shilingi **9,421,129,000.00** zilizotengwa, na **Shilingi 2,920,195,655.00** zilikuwa za Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 36.5** ya **Shilingi 8,000,000.00** zilizotengwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa asilimia kubwa ya fedha zilizopatikana kutoka Hazina ilitumika kugharamia uendeshaji wa Ofisi za Balozi zetu nje ya nchi; safari za Viongozi wa Kitaifa nje ya nchi; ukarabati wa majengo ya Balozi zetu zilizopo Kampala, Kinshasa, Lilongwe na Brussels; pamoja na utekelezaji wa majukumu mengine.

**Mheshimiwa Spika**, Mwelekeo huu wa matumizi hautofautiani sana na mwelekeo ulivyokuwa kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017. Hata hivyo, bado kuna umuhimu mkubwa kwa Wizara kuititia vipaumbele vyake kabla ya kuanza matumizi ya fedha zinazopokelewa.

## SURA YA TATU

### UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

#### **Uchambuzi wa Malengo ya Bajeti**

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kueleza uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, napenda kutoa Taarifa kwa Bunge lako tukufu kuwa, Kamati ilielezwa Miongozo Kumi na Mbili iliyozingatiwa wakati wa maandalizi ya Bajeti ya Wizara hili.

**Mheshimiwa Spika**, Mionganini mwa miongozo hiyo, ni Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001, ambayo ina umri wa takribani miaka kumi na saba. Miongozo mingine ni pamoja na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/21) na Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa zaidi kuwa Wizara imepanga Malengo Makuu Kumi na Mbili ya Kibajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Mfano wa Malengo hayo ni kuandaa Sera ya Taifa ya Diaspora itakayotoa mwongozo wa namna ya kuwashirikisha Diaspora wa Tanzania katika kuchangia maendeleo ya nchi yao. Lengo lingine ni kuratibu na kusimamia majadiliano ya Rasimu ya Andiko la Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki (*East Africa Political Federation*).

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba hakuna lengo mahsusili la ukamilishaji wa Mapitio ya Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje kwa wakati huu, ambapo Wizara itaratibu majadiliano kuhusu Andiko la Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki. Ni maoni ya Kamati kuwa jambo hili linapaswa kupewa umuhimu kwa kiwango stahiki.

### **Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii, Kamati ilichambua Makadirio ya ukusanyaji wa Mapato yanayopendekezwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kubaini kuwa Makadirio hayo yanatofautiana kidogo na lengo lililowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Katika Mwaka wa Fedha unaoisha, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya shilingi **25,773,882,820/-** wakati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara inalenga kukusanya kiasi cha Shilingi **28,564,154,100/-**. Lengo hili la Makusanyo limeongezeka kwa kiasi cha shilingi **2,790,271,280/-** sawa na **asilimia 10.8.**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa ongezeko hilo lipo katika lengo la Makusanyo ya Balozi zetu nje ya nchi ambapo zilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya shilingi **25,672,638,700/-** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 lakini kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 zinapewa lengo la kukusanya jumla ya shilingi **28,448,635,288/-**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ililinganisha lengo la kukusanya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na mwenendo halisi wa ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ili kutathmini lengo la maduhuli linalopangwa kwa Mwaka wa Fedha unaofuata.

Tathmini imeonesha kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2018 ni kiasi cha Shilingi **18,665,002,685.57 sawa na asilimia 72.70** kilikuwa kimekusanya. Kwa mwenendo huo, kiasi cha lengo kilichobaki ni shilingi **7,113,591,658.32 sawa na asilimia 27.30** ambacho kinaweza kukusanya kwa kipindi cha mwezi Machi hadi Juni, 2018. Kwa mwenendo huu, Kamati inaridhika kuwa lengo la Mapato linalowekwa linaendana na hali halisi.

### **Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa Wizara hii inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **177,006,232,000/=** ambapo shilingi **154,810,812,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC), shilingi **11,795,420,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi **10,400,000,000/=** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.


**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya Uchambuzi wa maombi hayo na kuona kuwa **87.5%** ya Makadirio hayo ni kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli, **6.7%** ni kwa ajili ya Mishahara na **5.1%** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1 na Grafu Na 1 na Na. 2 katika Taarifa hii.

Jedwali Na. 01: Uwiano wa aina za Bajeti ya Matumizi na ulinganisho wake kwa mwaka 2017/2018 na 2018/2019

MWAKA	2017/2018		2018/2019		% ONGEZEO
	AINA YA MATUMIZI	KIASI ASILIMIA	KIASI	ASILIMIA	
<i>MISHAHARA (PE)</i>	9,421,129,000.00	6.2	11,795,400,000.00	6.7	25.2
<i>MATUMIZI MENGINEYO (OC)</i>	133,424,290,000.00	88.5	154,810,812,000.00	87.5	16.
<i>MIRADI YA MAENDELEO</i>	8,000,000,000.00	5.3	10,400,000,000.00	5.9	30
<b>JUMLA</b>	<b>150,845,419,000.00</b>	<b>100</b>	<b>177,006,212,000.00</b>	<b>100</b>	<b>17.3</b>

Chanzo: Randama ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Uk. 10 na Uk. 74, Mwezi, Machi, 2018


### Grafu Na. 1: Ulinganisho kwa mwaka 2017/2018



Chanzo: Takwimu katika Jedwali Na. 1.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ulinganisho kati ya Bajeti ya mwaka 2017/2018 na mwaka 2018/2019 kama inavyoelekeza Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge. Katika ulinganisho huo, Kamati ilibaini kuwa fedha zinazoombwwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 zimeongezeka kwa **asilimia 17.3** kutoka shilingi **150,845,419,000/=** zilizoidhinishwa Mwaka 2017/2018 hadi shilingi **177,006,212,000/=** zinazoombwwa kuidhinishwa na Bunge leo kama ilivyobainishwa katika Jedwali Namba 1.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipochambua zaidi ilibaini kuwa Bajeti ya Mishahara, Bajeti ya Matumizi Mengineyo na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo imeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2017/2018. Bajeti ya Mishahara imeongezeka kwa **asilimia 25.2**, Bajeti ya Matumizi Mengineyo imeongezeka kwa **asilimia 16** na Bajeti ya Maendeleo kwa **asilimia 30**. Pamoja na hivyo, sura ya uwiano wa Bajeti iliyotengwa kwa vipengele hivyo vitatu kwa Mwaka 2017/2018 na Mwaka 2018/2019 haitofautiani sana kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1 na Grafu Na. 1 pamoja na Grafu Na. 2.



**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa mwenendo huu wa uwiano wa Bajeti utaendelezwa na hata

kuboreshwa zaidi. Ni imani ya Kamati kuwa hata baada ya kuidhinisha Makadirio haya, upatikanaji wa fedha utakuwa mzuri na unaozingatia namna Bunge linavyoidhinisha Makadirio haya ya Mapato na Matumizi.

**SURA YA NNE  
MAONI NA USHAURI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Dhamira ya Wizara ya kusimamia na kutekeleza diplomasia ambayo itachangia katika shughuli za kiuchumi na kuwezesha mageuzi ya haraka na maendeleo endelevu ya Tanzania, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

i) Serikali ihakikishe fedha zote kiasi cha Shilingi 9,329,800,000.00 ambazo zimetengwa kwa ajili ya kufungua Balozi mpya huko Cuba na Konseli Kuu katika miji ya Lubumbashi- Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Guangzhou- China zinatolewa kwa wakati na kutumika kama ilivyokusudiwa. Kamati inaamini pesa hizo zikitolewa kwa ukamilifu zitawezesha ufunguzi wa Ubalozi huo na Konseli kuu hizo na hatimaye nchi yetu kunufaika na fursa za kiuchumi na kibashara. Aidha, Serikali iweke mikakati zaidi ya kufungua Balozi au Balozi za Heshima katika nchi nyingine zinazoendelea kukua kwa kasi kiuchumi.

ii) Kwa kuwa kiwango cha fedha za bajeti zinazotolewa kwa Wizara kimekuwa hakiendani na mtiririko wa Fedha uliopangwa jambo ambalo linasababisha Wizara na Balozi zake kutotekeleza ipasavyo majukumu yake ya msingi hususana Sera ya Mambo ya Nje inayoweka msisitizo wa Diplomasia ya Uchumi, Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazotengwa zinatolewa kwa kuzingatia mtiririko uliopangwa.

iii) Kwa kuwa Kiwanja kilichotolewa na Serikali ya Oman kwa ajili ya kujenga Ubalozi wa Tanzania jijini Muscat hakijaendelezwa tangu kilipowekewa jiwe la Msingi na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Mwaka 2012, na kwa kuwa upo uwezekano wa

Kiwanja hicho kutwaliwa na Serikali ya Nchi hiyo endapo kitaendelea kukaa bila kuendelezwa, Serikali itoe Shilingi 1,894,056,560.00 zilizokuwa zimetengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ubalozi kabla ya Mwaka huu wa Fedha kuisha.

Sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Serikali itoe fedha za Maendeleo zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Ubalozi wetu wa Cairo, Ukarabati wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia, Dar es Salaam na Ujenzi wa Makazi ya Balozi, Addis Ababa.

iv) Pamoja na kwamba Serikali ilijiwekea Mkakati wa miaka kumi na tano (2001/2003-2016/2017) wa kuendeleza viwanja, kukarabati na kununua majengo ya Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini, Mkakati huo haujatekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutoa kipaumbele katika kuendeleza viwanja 12 ambavyo baadhi yake ni vya muda mrefu (Kama vile Viwanja vilivyopo Maputo, London, Adis Ababa, Nairobi, Muscat) na kuboresha majengo ya Ofisi na Makazi ya Watumishi katika Balozi zetu ikibidi kwa kutumia mikopo ya muda mrefu lakini yenyé riba nafuu.

Hii itasaidia Serikali kuokoa fedha nyingi za walipa kodi zinazotumika kwa ajili ya kukodi majengo ya Ofisi na Makazi katika Balozi zetu nje ya Nchi ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Shilingi **21,667,174,191.00** zimetengwa kwa ajili hiyo. Sambamba na hilo, hii itawezesha Serikali kujenga majengo ya kisasa ya Balozi zetu ambayo yakimalizika yataingiza fedha nyingi za kuendesha Balozi hizo na kusitisha utaratibu wa kupanga Ofisi na nyumba za watumishi.

Aidha, Kamati imebaini utaratibu huo ni wenye tija na mafanikio makubwa kama vile inavyoonekana katika Ubalozi wa Maputo – Msumbiji ambako kwa Mwaka ujao wa Fedha wa 2018/2019 hawatahitaji na hawakupangiwa fedha za pango;

v) Kwa kuwa Wizara imekubaliana na ushauri wa Kamati wa kupanga Miradi michache itakayoweza kutekelezwa kwa mwaka na hatimae kuweka Miradi mitatu ya Maendeleo kwa Mwaka ujao wa Fedha 2018/2019, Serikali ihakikishe kuwa inaipatia fedha Miradi hiyo hususan ule wa ujenzi wa Ofisi ya Ubalozi wa Muscat – Oman ambako Serikali inaweza kukusanya fedha nyingi za maduhuli kwa miaka ijayo;

vi) Kamati inatambua nia njema ya Serikali katika kuondoa suala la *retention* kwa Wizara zake zote. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu maalum utakaoruhusu Balozi zetu nje ya Nchi kubaki na angalau asilimia 40 ya makusanyo yao ili yawawezeshe katika kutekeleza majukumu yao hususan kukarabati majengo ambayo mengi yao yamekaa muda mrefu bila kufanyiwa ukarabati. Aidha, Serikali ione umuhimu wa kuweka utaratibu maalum wa kuziwesha baadhi ya Balozi kutuma fedha za makusanyo moja kwa moja Serikalini badala ya kuititia katika Ubalozi mwingine ili kuepukana na changamoto ya *exchange losses* ambayo inaathiri kiwango cha mapato yanayokusanya.

vii) Kwa kuwa baadhi ya Balozi zetu zinakabiliwa na changamoto ya kuwa na watumishi wachache kutoekana na baadhi ya watumishi kustaafu na wengine kurejea nyumbani baada ya kumaliza muda wa kufanya kazi Balozini, Serikali ione umuhimu wa kupeleka watumishi zaidi katika Balozi zenyetuhitaji ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, kwa kuwa baadhi ya wataalam katika Balozi zetu hawana weledi wa Diplomasia ya Uchumi, Serikali ihakikishe watumishi wanaopelekwa katika Ofisi zetu za Ubalozi wana utaalami, ujuzi na uzoefu "Professionals" kuhusu masuala yanayohusu Diplomasia ya Uchumi, ili kuondoa changamoto za uwajibikaji na utekelezaji wa kazi za Kibalozi zilizojitokeza huko nyuma.

viii) Kwa kuwa ni dhahiri Utalii wa Mikutano na matukio (business tourism) ni muhimu katika kuchangia na

kukuza pato la Taifa kuititia Sekta ya Utalii, na kwa kuwa Vituo vyetu Vya Mikutano ya Kimataifa hususan kituo cha Arusha (AICC) havina Chombo Mahsus (National Convention Bureau) cha kuitangaza Nchi na kuvutia Mikutano na maonesho ya Kitaifa kufanyika nchini, Serikali ione umuhimu wa kuanzisha Chombo hicho ili kuvutia Mikutano na Maonesho mengi ya Kimataifa kufanyika nchini na hatimaye kuongeza Pato la Taifa.

ix) Sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, ili kuimarisha Sekta ya Utalii nchini na kukuza pato la Taifa, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kuititia Balozi zake, iendelee kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kutangaza utalii nje ya nchi ili watalii wengi zaidi watembelee Tanzania.

x) Kwa kuwa Serikali imekuwa na kasi ndogo ya ubadilishaji wa Sheria za Nchi ili kuendana na matakwa ya Itifaki ya Soko la pamoja la Afrika Mashariki, Serikali pamoja na Idara na Taasisi zake iongeze kasi ya ubadilishaji wa Sheria za Nchi zilizoainishwa ili ziendane na matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja. Hii itawezesha Watanzania kunufaika ipasavyo na fursa za Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na Jumuiya nyingine za Kikanda.

xi) Kwa kuwa ni dhahiri kuwa kuna uelewa mdogo mionganoni mwa wananchi kuhusu masuala ya Mtangamano na faida zake, Serikali iendelee kutoa elimu kwa Umma kuhusu fursa zitokanazo na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa ambazo Tanzania ni Mwanachama.

xii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza kasi ya kuandaa Sera maalum kuhusu mtangamano wa Afrika Mashariki ili kuiwezesha Serikali kuwa na mwongozo wa kisera inapotekeleza masuala mbalimbali ya kijumuiya. Ushauri huu umekuwa ukitolewa mara kwa mara lakini haujazingatiwa kikamilifu.

xiii) Kwa mara nyingine tena, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kukamilisha haraka upatikanaji wa Sera

Mpya ya Mambo ya Nje. Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara kuhusu upatikanaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje itakayoendana na hali ya sasa ya Diplomasia ya Uchumi lakini utekelezaji wake umeendelea kuchukua muda mrefu.

xiv) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine ijenge Chuo kipyä cha Diplomasia cha kisasa Jijini Dodoma kitakachohamasisha nchi nyngine za Afrika na Duniani kwa ujumla kuleta wanafunzi wao na hatimaye kuongeza pato la Taifa kutokana na mapato yatokanayo na udahili wa wanafunzi hao. Aidha, ili kuvutia wanafunzi wengi zaidi, Chuo hiki kwa sasa kianze kufundisha lugha ya Kiswahili.

xv) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kulipa michango yote ya Kimataifa na Mashirika yake ambayo nchi yetu inadaiwa hadi muda huu hususan ya "International Conference on the Great Lakes Region – ICGLR" ili kuendelea kujenga heshima ya muda mrefu ya nchi yetu mbele ya Jumuiya ya Kimataifa. Ushauri huu umekuwa ukitolewa mara kwa mara lakini haujazingatiwa kikamilifu;

xvi) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kuharakisha mchakato wa kupatikana kwa jengo la kisasa la Kurugenzi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirkiano wa Afrika Mashariki kwa upande wa Zanzibar;

xvii) Kamati imebaini kuwa bado vitendo vya unyanyasaji wa wafanyakazi wa majumbani kwa baadhi ya nchi za nje vinaendelea, hivyo Serikali iweke utaratibu utakaohakikisha kuwa panakuwepo na usalama wa Watanzania wanaofanya kazi mbalimbali nje ya nchi kabla na baada ya kuondoka nchini Tanzania;

xviii) Serikali iweke utaratibu mahsus wa kufuatilia utekelezaji wa mikataba yenye tija kwa Taifa ambayo tumeingia na Serikali nyngine za Nchi za Nje. Hii itawezesha Tanzania kunufaika na faida zitokanazo na mikataba hiyo ambayo baadhi yake imekuwa haitekelezwi kwa kasi inayostahili;

**SURA YA TANO  
HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambaao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

- 1Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb, **Mwenyekiti**
- 2.Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb, **M/Mwenyekiti**
- 3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
- 4.Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
- 5.Mhe. Prosper J. Mbena, Mb
- 6.Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb
- 7.Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
- 8.Mhe. Cosato David Chumi, Mb
- 9.Mhe. Bonnah Mosses Kaluwa, Mb
- 10.Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb
- 11.Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
- 12.Mhe. Gerson Hosea Lwenge, Mb
- 13.Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
- 14.Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb
- 15.Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
- 16.Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb
- 17.Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb
- 18.Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb
- 19.Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb
- 20.Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
- 21.Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
- 22.Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb
- 23.Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb
- 24.Mhe. Augostino Manyanda Masele, Mb
- 25.Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga, (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Dkt.

Susan Alphonse Kolimba (Mb), Katibu Mkuu Prof. Adolf F. Mkenda, Naibu Katibu Mkuu Balozi Ramadhan Muombwa pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumanu Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama yalivyowasilishwa na mtoha hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mussa Azzan Zungu, Mb  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE,**  
**ULINZI NA USALAMA**  
23 Mei, 2018

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumemsikia Mheshimiwa Waziri, pia ushauri wa Kamati. Tutaendelea na utaratibu wetu; nimeletewa majina ya kuchangia hapa, lakini kabla sijaanza kuita wachangiaji, wako wageni ambao hawakutangazwa asubuhi, nitawatangaza sasa kabla hatujaendelea.

Nianze na Mheshimiwa Roberto Mengoni ambaye ni Balozi wa Italia; tunaye pia Mheshimiwa Theresia Samaria ambaye ni Balozi wa Namibia; vile vile yupo Mheshimiwa Monica Patricio Clemente Mussa ambaye ni Balozi wa Msumbiji; karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Tunao pia wanafunzi 49 wa Chuo cha Diplomasia, pengine wameshatoka lakini majina haya yamekuja baadaye. Karibuni sana wageni wetu Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza na ninayo majina hapa kwa mujibu wa uwiano wetu tulionao; tutaanza na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim ajiandae.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza naomba niwashukuru sana Wanambeya wenzangu kwa kusimama na mimi nilipofungwa kisiasa kwenye Gereza Kuu la Luanda, Mbeya, pia nawapa pole kwa wao kufungwa kisaikolojia. Nawashukuru pia Watanzania wote ndani na nje ya Tanzania kwa kulaani kufungwa kwangu kiholela. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Wabunge wote hasa wa Upinzani, kwa *support* kubwa waliyotoa, lakini pia hata upande wa CCM, japo kuwa mliogopa kuja kuniangalia lakini salamu zenu nilizipata; na *source* ya hofu yenu wote tunaelewa, lakini nimshukuru mzee, Profesa Mark Mwандосya, aliwawakilisha upande wa CCM kwa kuja kunitembelea jela. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami niwapongeze Mheshimiwa Stephen Masele na Mheshimiwa Mboni Mhita kwa nafasi walizochaguliwa kwenye Bunge la Afrika. Bunge letu limejiunga kwenye Vyama vya Kibunge vya kimataifa kama *CPA, PAP, ACPEU, IPU* na kadhalika, lakini wote tunafahamu ni kwamba hatushiriki vyema na tatizo sijajua ni nini. Hata hivyo, kama hatujui umuhimu mbona tunafurahia matunda ya ushindi wa

Mheshimiwa Masele na Mheshimiwa Mboni Mhita wakati wote tunajua hata kwenda huko walijigharamia wenyewe? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja, na nitaanza na masuala ya sera za mambo ya nje (*foreign policy*). Mheshimiwa Waziri wakati anaanza kuchangia alisitisiza sana kwamba mwelekeo wetu wa *foreign policy* hatutakubali kungiliwa wala kuchaguliwa marafiki. Naomba nimhakikishie na kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, najua ana weledi katika nyanja za kimataifa, kwamba sisi kama Tanzania hatujawahi kuburuzwa wala kuchaguliwa marafiki tangu enzi ya Mwalimu Nyerere na ndijo maana tulikuwa *member* wa nchi zisizofungamana na upande wowote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ile *Non-Aligned Organization (movement)* sisi tulikuwa ni *member* muhimu sana na tulitambulika kimataifa. Tanzania ilikuwa inaheshimika kimataifa kwa mambo kadhaa. Kwanza na muhimu tulikuwa na sera ya kutetea wanaokandamizwa duniani; mfano South Africa, Mozambique, tuliwasaidia sana mpaka kufikia kujiondoa katika makucha ya *apartheid* na wale Mozambique kupata uhuru wao kutoka kwa Wareno.

Mheshimiwa Naibu Spika, sera hizo hizo tulizokuwa nazo dhidi ya South Afrika na Mozambique ndizo tulisimamia Sera yetu ya Mambo ya Nje kwa Palestina na Sahara ya Magharibi. Mwalimu Nyerere alifuta uhusiano wa kibalozi na Israel kwa *ku-support struggle* ya Wapalestina kudai uhuru. Sasa tujiulize leo hii tunaenda kufungua Ubalozi Israel, je, ile *course* ya Mwalimu *ku-support* uhuru wa Palestina imefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu ukiangalia ni kwamba hali imezidi kuwa mbaya Wapalestina ndani ya Gaza na maeneo mengine yanayokaliwa kimabavu wanazidi kuuawa kila siku kadri Israel inavyoongeza uwezo wake wa kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika Mwalimu Nyerere na sisi kama Taifa tulifuta uhusiano na Morocco kwa *ku-support* kudai haki kwa Sahara ya Magharibi chini ya *POLISARIO*. Sasa leo tumeacha sera zetu dhidi ya Morocco kwa ahadi ya kujengewa uwanja wa mpire *stadium*, tunajivunja heshima kwa ahadi ya kujengewa uwanja wa mpire ambao Mheshimiwa Mkapa amejenga pale Dar es Salam uwanja wa mpire kwa *support* ya Wachina bila kuuza nchi wala bila kukiuka misimamo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina uhakika Mheshimiwa Waziri na Bunge hili Mwalimu Nyerere Baba wa Taifa huko alikolala kaburini Mwitongo anageuka geuka kwa jinsi Taifa hili linavyokwenda sasa hivi katika sera ya mambo ya nchi za nje. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *diaspora*; naomba sana Mheshimiwa Waziri tuache siasi kwenye maisha ya Watanzania wenzetu. Ni lini Serikali itatambua Watanzania wanaoishi nje ya nchi (*diaspora*)? tuache kutoa ahadi kila tena nasikia mwakilishi yuko hapa, *I hope* amekuja ile *straight* hakuja kisiasa kwa sababu wenzake anaowawakilisha wanalia sana kule, sisi tumekaa kule, tuna mawasiliano kule, tunajua kilio chao, hata hapa kwenye simu nina mawasiliano ya kutoka *diaspora* baada ya wao kujua kwamba leo kinaenda kuzungumzwa nini, wametoa nao changamoto zao wanataka tuzizungumze humu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachotaka watu wa *diaspora* ni kuruhusiwa uraia pacha, kama ambavyo uraia pacha uko katika nchi nyingine. Wapewe uraia pacha ili waweze kushiriki kujenga uchumi na si tu makongamano mara kuwaalika Zanzibar, mara kuwaalika wapi. Wakati umefika turuhusu sasa uraia pacha ili watu hawa waweze kushiriki katika uchumi wa nchi. Hawa watu wa *diaspora* sasa wanaanzisha kitu kinachoitwa *Tanzania Global Diaspora Council (TGDC)*. Sasa tusije sisi na mawazo yetu tunataka kuwasaidia vipi sijui kuwashirikisha vipi, wale wana *exposure* wamefunguka, wanajua wanachokitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa itakiwa tutambue na Serikali iniambie imejipangaje kufanya kazi hiki chombo cha *diaspora* cha *Tanzania Global Diaspora Council* ambacho kinaenda kuanzishwa na hawa Watanzania wenzetu katika kusaidia kuji-integrate kwenye masuala ya nchi yao ambayo wanaipenda. Kwa sababu, *otherwise* mtu kama ameshapata uraia wa wapi anaweza akaamua kuendelea na maisha na kusaidia kuleta maendeleo kwenye yale maeneo wakati tungewapa fursa wangeweza kafanya hivyo katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna ajenda ya pamoja kwa *diaspora*. Mheshimiwa Mzee Kikwete alipokuwa anaenda nje aliwashawishi *experts* wa Tanzania huko nje warudi kujenga nchi yao; lakini utawala huu uliofuata ukawageuka na kuanza kuwanyanyasa mfano ni yule mama Julieth Kairuki wa *TIC*. Mheshimiwa Dkt. Kikwete alikwenda kumshawishi South Afrika ameacha kazi yake nzuri, ameacha kila kitu kilicho kizuri kinachoendana na weledi wake amekuja nyumbani kusaidia kujenga nchi, lakini leo unamwambia kwamba hatuwezi kukulipa huo mshahara mkubwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi alikuja kwa makubaliano gani kutoka South Afrika anakuja hapa tunakuja tunawageuka? Wengine waliambiwa warudi kujenga nyumbani na kuwekeza wakaanza kurudi kwa wingi wakajenga majumba, wakafungua biashara. Leo hii Waziri wa Ardhi hawa si raia halali, kwa hiyo mali zao zitataifishwa tunawatia woga Watanzania wezetu hawa wakati walikuwa wangeweza kushiriki vizuri sana katika masuala yetu ya uchumi na kujenga nchi.

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi kengele ya kwanza imegonga, lakini kuna taarifa kule nyuma, naomba ukae Mheshimiwa upokee taarifa.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** (*Aliongea bila kutumia kipaza sauti*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi naomba ukae kuna taarifa.

*(Hapa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi aliendelea kuongea bila utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbilinyi kama ni hayo yaliyokuleta humu ndani unajua kitakachokupata, Mheshimiwa Mollel kule nyuma.

**MHE. DKT. GODWIN O MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe rafiki yangu taarifa kwamba kwa sisi kufungua Ubalozi Israel hatujapingana na Mheshimiwa Rais aliyekuwa Baba yetu wa Taifa; kwa sababu moja; ni kwamba kama ni watu wa kwanza kupingana na Mheshimiwa Rais ni wao kwa sababu tuliwaona sehemu wakifanya kikao na wale watu ambao Rais alienda kuwashtaki Umoja wa Mataifa lakini wao sasa ndio watetezi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunajua kwamba wamezunguka sehemu nyingi dunia kuhakikisha kwamba taifa hili linasusiwa na mataifa. Jinsi Rais Dkt. Magufuli alivyo mzuri wao wakizunguka kwa viranja, Rais ameenda kwa Mwalimu Mkuu amefungua na nyumba ya kuishi kule, kwa hiyo wamechanganyikiwa hawawezi kutimiza azma yao, kwa hiyo tunacho...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, Mheshimiwa Mbilinyi unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH. O MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei taarifa ya Dkt. Shika. Nimpe tu utaalam mdogo; tulikuwa na Ubalozi wetu Egypt ambao ulikuwa ni ubalozi *neutral*...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa kuangalia muda tulio baki nao sitaruhusu taarifa tena sasa hivi, Mheshimiwa Mbilinyi.

**MHE. JOSEPH. O MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ilifaa kabisa kubakisha ubalozi wetu pale Cairo, Egypt, kwa sababu ule ubalozi ulikuwa *neutral* na ulikuwa unaweza ku-*harmonize* pande zote yaani Palestina na Israel mpaka mambo yao yatakapokaa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ni *top diplomat* wa nchi, suala la kusafiri bado ni muhimu, labda kama ana tatizo la kiafya. Tena anapokwenda nje anaweza kutumia lugha ya Kiswahili kwa sababu Rais wa Xi Jinping wa China kila anakokwenda anaongea Kichina japokuwa ni msomi aliyesomea Marekani. Yeye amesomea chuo kikuu na elimu zake za juu Marekani anazungumza Kiingereza vizuri, lakini kila anapokwenda anazungumza lugha ya Kichina; kwa hiyo tena tutakuwa tunaitangaza na lugha yetu ya Kiswahili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama tatizo ni gharama mbona anatumia *delegations*? Mara Makamu wa Rais, mara Waziri Mkuu nao wanatumia gharama kwa sababu hawaendi kule kwa miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hatuendi *UN*, hatuendi Davos, hatuendi *Common Wealth*. *Common Wealth* ni Mkutano wa Wakuu wa Nchi (*Head of States*), lakini sisi tunatuma wawakilishi wakati kule kuna fursa za kiuchumi na biashara. Rais Uhuru Kenyatta ametumia vizuri sana fursa za kiuchumi na kibiashara kwa nchi alipokwenda *Common Wealth*, hali kadhalika Rais Ramaphosa wa South Afrika pia alitumia huo kukutana na *investors* wa kutosha aka-*archive* miradi ya takribani *Rand* triliioni 1.2 kwa ajili ya nchi yake; ndizo faida ya majukwaa haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Rais kusafiri haiepukiki, ni muhimu na kama alivyonukuliwa mzee Kikwete Rais aliyepita kwamba kusafiri kulimsaidia sana, mkaa bure si sawasawa na mtembea bure; hii alisema wazi. Kwa hiyo kusafiri ni muhimu sana, kwa sababu Mabalozi tunaowachagua huko hawatusaidii kwa sababu

tunachagua Mabalozi wetu kisiasa bila kuangalia weledi. Aidha, tunawapa ubalozi watu kama zawadi au kuwa-control.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Slaa tumempa zawadi kwa kazi aliyoifanya 2015 katika uchaguzi, tumempa ubalozi, lakini Dkt. Emmanuel Nchimbi tumempa ubalozi Brazil kum-control ili awe mbali kudhibiti ushawishi wake ndani ya Chama cha Mapinduzi. Haya ni mambo ambayo yako wazi na yanaelewaka kabisa. Sasa hawa ni shida sana kusimamia diplomasia ya uchumi, watakuwa wanaleta siasa pekeyake na iko hivi...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Sekunde 30 maliza muda wako kengele imeshagonga.

**MHE. JOSEPH. O MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimamishwa kidogo. Diplomasia ya uchumi bila *stability* ni shida. Tunawatisha wawekezaji, tunapiga risasi Wabunge, tunafunga ovyo Wabunge. Wawekezaji wa nje walifuatilia haya mambo. Wakifuatilia haya mambo inakuwa wanasiita sasa kuja kuwekeza kwa sababu hakuna mwekezaji anayetaka kuweka kwenye nchi ambayo haiko *stable*, haina amani na usalama. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge nilimtaja Mheshimiwa Cosato David Chumi atafuatiwa na Mheshimiwa Masuod Abdalla Salim, Mheshimiwa Fakharia Shomar ajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa na mimi kuchangia Wizara hii na kwa haraka kabisa napenda kuipongeza Wizara kuanzia Mheshimiwa Waziri, Naibu, Makatibu Wakuu pamoja na Mabalozi ambao ni Wakurugenzi wanaoongoza idara mbalimbali katika Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizi haziwezi kwenda tu hivi hivi zitaendana na ukurasa wa 25 ambaao unaelezea misamaha ya madeni ya nje. Hii yote ni jitihada za kazi nzuri ambaao Wizara pamoja na Wakurugenzi na Mabalozi kote waliko wanaifanya na ndiyo maana tumeweza kusamehewa baadhi ya madeni katika Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia na mimi nichukue nafasi hii kuwapongeza wenzangu Mheshimiwa Masele na Mheshimiwa Mboni Mhita kwa nafasi walizochaguliwa. Hii inaendelea kuthibitisha kwamba Taifa bado linaendelea *to maintain* heshima yake katika nyanja za kidiplomasia Afrika na dunia kwa ujumla. Kwa hiyo tuendelee kusonga mbele na kuchapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa sababu si haba niseme kidogo, sina nia ya kumjibu ndugu yangu Mheshimiwa Mbilinyi lakini niseme tu kwamba, katika nyanja za kidiplomasia nchi kama Algeria nitawapa mfano ndiye *supporter* mkubwa wa *POLISARIO* Chama cha Ukombozi wa Sahara. Hata hivyo, Algeria hii ambaao *POLISARIO* Makao yake Makuu yako Algeria ina mahusiano (*bilateral*) na Morocco. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kum-*support* mtu fulani haikuzuii wewe kufanya mahusiano na yule mtu mwingine *as far as you have interest in that particular* mahusiano. Kwa hiyo si jambo geni, hata South Afrika ni *supporter* mkubwa wa *POLISARIO*, ndio wanaao *finance* *POLISARIO*, lakini wana mahusiano *bilateraly* na Morocco. Kwa hiyo, unaangalia wewe una *interest* gani na misimamo yako inabaki vile vile; niliona ni muhimu kulisema hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nipende pia kupongeza kwa kufunguliwa hizi balozi zetu nyingine, sita na Mheshimiwa Waziri amesema mabalozi wamesha kwenda. Pia kama ambavyo Kamati ilikuwa imeshauri kuwa

na umuhimu wa kufungua zile tunaita *General Consulate* katika Miji ya Lubumbashi na Guangzhou. Nimeona kwamba Serikali imezingatia ushauri wa Kamati na Wabunge kwa ujumla na kwamba sasa tunakwenda kufungua *General Consulate* katika hiyo miji ambayo iko *strategically* kibashara kwa Taifa letu, kama hiyo Lubumbashi na Guangzhou.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mambo ambayo ya kupongeza na yanaonesha kwamba Serikali inachukua mawazo yetu Wabunge na kuyafanya kazi. Kwa hiyo niwasih tu kama Serikali twende kwa haraka katika kulitekeleza kwa vitendo jambo hili ambalo mmelichukua kutokana na ushauri wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie; Mheshimiwa Waziri amekuwa kwenye nyanja hii ya diplomasia, atakuwa anafahamu kwamba sasa hivi kuna reforminaendelea *UN Security Council*, kwamba na sisi kama Afrika tungependa tupate nafasi katika sehemu ile ya zile kura tano za *veto*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama Taifa nimwombe Mheshimiwa Waziri tujipange vizuri na hatua mojawapo ya kujipanga ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunapeleka maafisa katika vituo vyetu vya ubalozi. Tukiwa na maafisa wa kutosha maana yake ni kwamba ushiriki wetu utakuwa ni madhubuti. Kuna vituo ambavyo ni *multilateral stations*, Mheshimiwa Waziri anafahamu, kama New York, anafahamu pale kuna Kamati sita ambazo kila Kamati inapaswa iwe na afisa kwa ajili ya kutetea maslahi mbalimbali ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano wa Kamati ya tano, Mheshimiwa Waziri anafahamu kabisa kwamba baada ya kufunga *ICTR* tuko kwenye *transition* kuititia ile *Mechanism For International Criminal Tribunal*. Katika bajeti ya 2018/2019 mapendekezo yalikuwa kwamba tupate nadhani dola milioni mia mbili kumi na tano. Hata hivyo,

kutokana na kukosa ushawishi wa kutosha, Waziri anafahamu mataifa makubwa yamepunguza tumepata dola milioni 88.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jitihada za baadhi ya mataifa kuhakikisha kwamba hata ikiwezekana ile iliyokuwa *ICTR* ifungwe ihamie The Hague. Sasa jambo hili likifanyika ni hasara kwa Taifa letu kwa sababu, *imagine* kama mahakama ile inapangiwa dola milioni 215 maana yake ni kwamba hata kiuchumi zitaongoza mzunguko katika Taifa letu, siyo tu pale Arusha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Nanibu Spika, pia jitihada hizi inabidi tujipange kikamilifu kuweka kukabiliana nazo; kwa nini; kwa sababu wa uwepo wa *ICTR* pale Arusha ni *legacy* kubwa kwa Taifa letu katika dunia. Sasa jitihada hizi kama hatutahakikisha tunapeleka watumishi wa kutosha katika balozi zetu, maana yake ni kwamba hata ushiriki wetu katika vyombo mbalimbali *especial* hizi Kamati utakuwa ni *minimum*. Kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Waziri tu *speed up* hii process ya kupeleka maafisa kwani umuhimu wake uko wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama vile haitoshi, kwa nini mimi nasema nasema masuala haya, watu wengi tunapozungumza masuala ya *peace keeping* wanazungumzia *chapter six* na *chapter seven*; lakini ukweli *UN* imeendelea kupunguza fedha za kulinda amani katika maeneo ya migogoro Afrika. Hii ni kwa sababu ama tunapunguziwa ushawishi kutoka labda na *understaffing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimwmbe Mheshimiwa Waziri kwa sababu yeye ni nguli katika nyanja hii, katika hii *reform* inayoendelea ya *UN Security Council* hebu sisi kama watu ambao tunaaminika kiplomasia na kimataifa, kwamba tuna ushawishi mkubwa Kusini mwa Afrika, tuna ushawishi mkubwa katika bara la Afrika, tuna ushawishi mpaka katika South East Asia, hebu tu-*play role* yetu ili kusudi ushawishi kama Taifa katika Umoja wa Mataifa uendelee kuwa

mkubwa ili kusudi hata yanapokuja masuala ya bajeti kwa mfano za *peace keeping* tuweze kushawishi pesa itengwe ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu madhara yake ni nini, tumeona tumeopoteza wanajeshi pale Congo. Ingekuwa *UN* inapeleka bajeti ya kutosha ya *peace keeping*; maana tumeambiwa mapigano yalidumu masaa 14, maana kama vingekuwa vifaa nya kisasa, tuna ndege za *rescure* maana yake tungeweza kuokoa wanajeshi wetu wale. Haya yote hayafanyiki kwa sababu ndani ya mfumo wa *UN* wakubwa wa dunia wanajitahidi kuhakikisha ile keki inapelekwa katika mambo ambayo wao wanaona yatakuwa yanawasaidia lakini sisi hayatusaidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niishauri Serikali kwamba tuendelee kuthibitisha kwa vitendo kwamba sisi ni taifa kubwa katika ushawishi wa diplomasia kimataifa Afrika na duniani kwa ujumla; na ushiriki huu utathibishwa kwa sisi kuendelea kuwa na *staff* wa kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia sitakuwa nimetenda haki kama sitawashukuru Wizara katika ujumla wake. Nimeona hapa wametuletea kijitabu kinasema *find about us*; ndani yake kina anuani za Balozi zetu. Maana yake ni kwamba sisi hapa ama tuna ndugu zetu ama tuna watu wanaenda katika matibabu au watu wanaenda kutafuta fursa za kibashara au kuna wanafunzi. Sasa kijitabu hiki kitaraphisha yale mawasiliano ya kidiplomasia kujua nchi gani balozi ni nani na anuani yake ni ipi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi wametupa pia kijitabu ambacho kinaonesha anuani za Balozi za nje ambazo ziko hapa nchini. Vile vile wametupa kijitabu hiki kinachoonesha diplomasia ya Tanzania ambapo ndani yake wametuonesha picha, wameandika na *caption* ya utekelezaji mbalimbali wa Diplomasia Tanzania kuelekea uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli niwashukuru sana na naamini Mheshimiwa Masoud, Mzee wangu wa Matambile pale atakuwa leo amefurahi na atacheka mpaka jino la mwisho kwa sababu ni kitu ambacho tumekuwa pia tukizungumza katika Kamati na Serikali imeweza kuthibitisha. Niongeze tu wakati ujao wanaweza kutuboreshea pia kwa kutuletea kijitabu ambacho kinaeleza kila nchi ina fursa gani na watu wanaweza kuzipata fursa zile kwa namna gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, napende kushukuru na naunga mkono hoja. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika. Ahsante sana (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Masoud kwa maneno hayo bado unachangia? Nilifikiri umeahirisha! Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis na Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe ajiandae kwa dakika tano.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* aliyetujalia uzima na afya njema katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, tuwatakie sote tunaofunga Mwenyezi Mungu *a-taqabbal*funga zetu, atulipe ujira mwema, na *Insha Allah bi-idhinillah* malipo ya kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mhehimiwa Waziri muhusika, tatizo la mahujaji waliosota, waliokaa muda mrefu wakati wanakwenda Hija mwaka uliopita tatizo hili lisirejee tena. Ilikuwa ni aibu kubwa, tatizo kubwa, liliteta taswira mbaya mionganoni mwa watu mbalimbali. Wizara husika ni Wizara hii hii. Kwa watu wote wanaoshughulika na kwenda nje kwa vyovoyote iwayyo bado Wizara ya Mambo ya Nje inahusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu wazi wazi; tumekuwa tukipiga kelele kwamba wameiandikia BAKWATA tena kuwapa Mamlaka na madaraka ya kuwapeleka watu Mahujaji hawa kwenda kuhijji, tafadhali sana BAKWATA kama

Taasisi nyingine kwa hiyo msiwape mamlaka, yakinoteka mambo mengine hasa tutasema kwamba BAKWATA ni sehemu ya Serikali na ndivyo inavyonekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachosema ni kwamba waachenii taasisi nyingine za kidini ziandae utaratibu wake wa kupeleka mahujaji Makka, ndiyo nikasema sasa ni vyema tujitathmini na hili. Upungufu huu wa kupeleka Mahujaji Makka dosari hii isitokee tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *APRM (African Peer Review Mechanism)*, mpango wa kujitathmini wenyewe kiutawala bora, kisiasa, kiuchumi na mambo mengine. Nashukuru kwamba wameongeza fedha. Hata hivyo, nataka Mheshimiwa Waziri aniambie kisiasa wamejitathmini kiasi gani kwa wakati huu pale ambapo mwendelezo au wanakaa mahabusu muda mrefu Mahakamani, unaambiwa upelelezi haujakamilika. Masheikh wa Uamsho wamekaa muda mrefu, juzi tu Mheshimiwa Waziri alisema kwamba ushahidi umepatikana, wanasubiri *e-mail* kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi watu wanakaa mahabusu miaka minne, miaka mitano hili hawalioni, wanataka tafsiri nyingine zije tafsiri za aina gani? Masheikh wa Uamisho wamekaa muda mrefu sana. Kwa hiyo wanajitathmini kiasi gani? Amesema Mheshimiwa Bwege mpaka akatoka machozi. Watu wamepigwa risasi Msikitini kule Chumo, damu imemwagwa msikitini Chumo. Tafadhali sana, hakuna kitu kibaya katika mambo haya ya hisia za dini. Waliopigwa risasi kule Chumo msikitini liwe jambo la mwisho tafadhalini sana. Mheshimiwa Mahiga anifahamu na walionifahamu wanifahamu, wale Taasisi za Serikali za kiulinzi wanifahamu, risasi msikitini isilie tena maisha, tafadhalini sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina suala lingine ambalo ni juu ya mahusiano yetu ya mambo ya nje na Mataifa mbalimbali uko vizuri. Nafahamu uhusiano mzuri tulionao sisi na Msumbiji, nafahamu jinsi Tanzania ilivyoshiriki katika ukombozi ule wa Msumbiji, nafahamu mambo mengi mazuri

yetu sisi na Msumbiji na mimi naunga mkono. Kuna Watanzania ambao wako gerezani kule Msumbiji katika Gereza la Beyo kule eneo la Pemba ambao wako gerezani hasa kwa muda wa miezi sita. Hawa ni wapiga kura na kwa mahusiano mazuri sisi na Msumbiji na nadhani nampongeza sana Balozi wetu Monica hapa leo yupo hongera, sana nampongeza sana Balozi Monica. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa naomba sana niwataje kwa majina wapo Beyo hapo Msumbiji kwenye Gereza hilo. Kwanza kutoka Jimbo la Kiwani na Mtambile Jimboni kwangu na hawa wamefanya makosa madogo madogo tu, hawana yale makosa makubwa ukasema makosa yale labda ya madawa ya kulevyia; nao ni

Shahali Makame Omary wa Chole-Kiwani; Fadhili Khamisi Makame, Chole-Kiwani; Khamisi Fadhili Khamisi, Chole-Kiwani; Mussa Rare Mussa, Chole-Kiwani; Ally Zidini Ngali, Chole-Kiwani; Zahoro Ngwali Ally, Chole-Kiwani; Zaharani Fadhili Khamisi, Chole-Kiwani; Silima Yakoub Ally, Chole-Kiwani; Ally Shahali Makame, Chole-Kiwani; Mbarouk Hijja Silima, Chole-Kiwani; na Juma Tabu Mussa, Chole-Kiwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo la Ziwanii kuna Abdallah Khalfani, wa Wesha; na Hamza Fikira Sharif, wa Wesha. Kuna Jimbo la Mkoani nako kuna Makame Burhani Kombo, wa Chokocho; na Faki Shahali, wa Chokocho. Donge-Unguja yuko Mselem Khalfani Mohamed na Chumu Mshenga, hawa wako kwenye gereza la Beyo huko Pemba-Msumbiji. Tafadhalii sana, kwa ujirani tulionao na ubora wa Balozi wetu Monica ninavyomwona yuko vizuri sana, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili jambo walichukue, utaratibu wa nchi nyingine wanakuwa wanafahamiana, utaratibu wa kuwarudisha mahabusu au wafungwa kutoka nchi hizo sembuse hapo jirani tu. Naombeni sana hawa watu waandae mazingira mazuri waweze kuwarejesha. Nina imani kwa ujumbe huo Mheshimiwa

ataweza kufanya jambo lolote la msingi la kuweza kufanya shughuli zinazohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye jambo lingine la tatu ambalo ni miradi ya maendeleo. Mara nyingi tunasema kwamba baadhi ya miradi ya maendeleo inataka itekelezwe kwa wakati wake. Kuna miradi inayopaswa kutekelezwa katika Visiwa vya Unguja na Pemba yaani Zanzibar. Mpiga duru yupo katika mikakati, naomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie suala la mpiga duru.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka kadhaa wamekuwa wakisema kwamba wana mpango mkakati wa kuboresha uwanja wa ndege Pemba, lakini kila mara wanataja, wanataja katika mipango yao hii ya kiujumla katika bajeti hii ya Afrika mashariki. Ni kwa nini na ni sababu zippi za msingi zillizopelekea uwanja wa Ndege, Pemba haupewi kipaumbele ukapewa nafasi yake ili ile dhana ya uchumi unaohitajika ukaendelea, tatizo ni nini? Pemba ipo Tanzania nataka wafahamu haiko sehemu nyingine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Mkoani walisema muda mrefu kwamba nayo wataboresha, watakwenda vizuri lakini hadi leo inaonekana bado ni danganya toto. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aniambie habari ya mpiga duru, aniambie habari ya uwanja wa Ndege wa Pemba, anipe habari rasmi ya Bandari ya Mkoani na Bandari ya Wete. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, atumishi ambao wako katika Balozi inafika wakati Maafisa huwa hawapeleki kwa wakati na ile dhana ya diplomasia ya kiuchumi inakuwa inasusua. Naomba waniambie sasa kwamba kwa nini wanakuwa na kigugumizi cha kupeleka Maafisa kwenye Balozi kwa haraka haraka pale ambapo wengine wameshamaliza muda wao. Anipe habari, nataka kujua kule Ankara, Uturuki, anipe habari ya Korea, Doha-Qatar, Brussels ambapo kuna vikao vingi ya *European Union* nako sasa hawapo au ni kidogo sana. Addis Ababa napo ni tatizo, New York nako vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili tatizo ni lini wataweza kulisawazisha kwamba tunasema tuna *economic diplomacy* (diplomasia ya kiuchumi) lakini Maafisa wale wa Ubalozi ambao wanahitajika kwenda kule hawako, sasa hili nalo ni tatizo. Sasa Mheshimiwa Waziri aniambie jambo hili ni lini litakaa vizuri.

Mheshimiwa naibu Spika, la mwisho, tuepukane na aibu kubwa ambayo tunaipata kwenye vile viwanja ambavyo haviendelezwi. Majengo ambayo wanataka kuyakarabati hapa yapo, lakini kila wakati tunaweka bajeti tu lakini fedha zile hazipelekwi. Kwa hiyo atuambie sasa mkakati wa kuepukana na aibu ni upi. Leo tunaambiwa kwamba Tanzaia itashtakiwa katika nchi husika kwamba majengo yale ni machakavu, mabovu na viwanja haviendelezwi. Nimwambie Mheshimiwa Waziri, hii ni aibu kwa Taifa kama letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa tujifunze, tuepukane na aibu kwa nchi za nje, tunajitia aibu sisi wenyewe kwa sababu hatupeleki zile fedha. Kama ingekuwa tunaona kwamba kuepuka aibu Mataifa ya wenzetu wasiweze kututafsiri vinginevyo, basi majengo hayo tungeyakarabati, tungepeleka fedha na vile viwanja ambavyo vilitaka kuchukuliwa ambavyo vimekuwa ni pori na tunataka kushtakiwa ile aibu sisi tungkuwa hatunayo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Serikali ni moja waandae mazingira kuona kwamba majengo yetu yanakarabatiwa, fedha zinapelekwa na vile viwanja ambavyo vinatia aibu, aibu hiyo inaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie la mwisho, ni hati za utambulisho (*Present Credential*), wamepanga mara kadhaa Mheshimiwa Naibu Waziri, hizi hati za utambulisho katika maeneo ambayo tumepanga basi tufanye kweli. Ukiangalia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Namalizia sekunde 30.

**NAIBU SPIKA:** Ameshasikia hati za utambulisho, ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe dakika tano na Mheshimiwa Machano Othman Said dakika tano.

**MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, sina budi kumpongeza Wizara kwa hatua nzuri wanayofikia katika majukumu yao Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Kurugenzi yake yote kwa utendaji wao mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, sina budi kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwasamehe wafungwa na kuwa huru kwa mujibu wa Katiba na ndani yake ndiyo Mheshimiwa Mbilinyi na yeye kapata msamaha leo tunaye hapa Bungeni na tunaweza kuwa naye na kuchangia naye katika Bunge letu hili Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia diplomasia ya uchumi; diplomasia ya uchumi inasaidia kwa Wizara na nchi nzima kuweza kujua jinsi Mabalozi wetu wanavyokwenda nje nini majukumu yao ya kufanya. Hata hivyo, ilivyo Wizara bado haijajipanga kuweza kupatikana sera mpya yao ya Wizara ikaungana na hii ya diplomasia ya uchumi ikaenda pamoja, vikawa vitu viwili sambamba tukaweza kufanikiwa katika majukumu ya utendaji wetu wa kazi na Wizara mpaka leo sijui inasubiri nini na kushindwa kutoa sera mpya ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje. Mheshimiwa Waziri naomba atakapokuja atuambie wanakwama nini hata wanashindwa kutoa sera mpya itakayoendana na sera ya uchumi ya diplomasia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sera hiyo ya diplomasia ya uchumi itasaidia kutupatia masoko, kutuletea watalii tena siyo wale wa makundi tunataka waliokuwa na hadhi za juu, itaweza kutuletea wawekezaji maana tuna sera ya viwanda,

tunataka kuanzisha viwanda Tanzania ili tuweze kutanua uchumi wa Watanzania. Zanzibar kuna fukwe nzuri za watalii, Bara kuna Kilimanjaro nzuri kwa watalii, tuna mbuga za wanyama, kuna bahari au bustani ndani ya bahari ambavyo hivyo vyote ni vivutio kwa utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwa Mheshimiwa Waziri, kama inavyozungumzwa, anavyopeleka watendaji katika Balozi zetu, apeleke watendaji ambaeo wanaendana na diplomasia ya uchumi ili waweze kutusaidia katika majukumu yetu tunayotaka kuyaanzisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwa upande wa Zanzibar, Zanzibar tunataka au tungependa tuwe na jengo letu kama Ofisi ya Wizara ya Muungano, kama walivyo Mambo ya Ndani, kama walivyo Wizara nydingi za Muungano zina Ofisi zao wenyewe wamejenga. Sasa tunashangaa Mambo ya Nje mpaka leo kuanzia 1964 hadi leo hamna jengo, wana jengo lile ambapo wanasesma wapo kwenye mazungumzo na mazungumzo hayo hajulikani yatamalizika lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba viwanja Zanzibar kwa kujenga Ofisi vipo. Waache mazungumzo, waombe viwanja waweze kujenga lakini wakisubiri wanazungumza hii kama inabidi wanavuta muda na wakati, wakati muda wa kujenga hawajakuwa nao na wala hawajakuwa na tamaa ya kujenga. Mheshimiwa Waziri naona Kamati imemwambia kwamba tunataka Kurugenzi za Zanzibar na wao wafanye kazi katika jengo linaloridhisha na linaloitwa kwamba ni jengo la Ofisi siyo nyumba imegeuzwa jengo wanasesma ni Ofisi, hiyo haitowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi ya Ofisi za Ubalozi wetu wa nje pamoja na Ofisi zao hayaridhishi na kwa nini hayaridhishi? Kwa sababu kuanzia sasa pesa nydingi tunapoteza kulipa katika majengo. Ikifika mwaka lazima tutenje bajeti ili tulipe pesa za Ofisi. Kwa mwaka huu tayari Wizara imeshatenga bilioni 21.6. Pesa hizi ni za kodi za walalahoi tunazokwenda kulipa, kwa nini tunashindwa

kujenga? Tungejenga ili kunusuru pesa za walipa kodi wetu tena maskini wa Tanzania walalahoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, hili wazidi kuliangalia maana hizi pesa zitatoka nyingi na pesa hizi kama wangekuwa wanatoa kidogo kidogo huku wanaanza kujenga Ofisi zetu za Ubalozi tungekuwa tayari tuko mbali na tungeweza kupata mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, Ubalozi wa Oman umetoa kiwanja Muscat. Tayari Mheshimiwa Rais Mstaafu Dkt. Jakaya Kikwete amekwenda kuweka jiwe la msingi. Hata hivyo, toka mwaka 2012 hadi hii leo hakuna kinachoendelea na wako tayari wenyeewe kuchukua sehemu yao kwa sababu wameshatuona hatuna maendeleo ya kuyafanya. Ingawa aliomba 1.8 *billion* lakini mpaka leo hajapewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naiomba Wizara ya Fedha wangefanya kila mbinu, hizi pesa zikatoka angalau tukaonekana na sisi tunajhangisha kuleta maendeleo. Ikiwa watu wamesema ukibebwa na wewe jikaze, wametupa kiwanja, wako tayari kutusaidia ina maana sisi kuijendeleza tunashindwa? Mheshimiwa Waziri akishirikiana na Wizara ya Fedha, naomba hili waliangalie na liweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unyanyasaji wa wafanyakazi wa majumbani nje. Unyanyasaji huu umekuwa mkubwa na vijana wetu wengi wanaondoka kinyemela, Wizara au Serikali inakuwa haijui, Balozi kule za nje hawajui kama vijana wetu wapo. Sasa hili walitilie mkazo na waweze kujua mbinu wanazopita na waweze kujua Ma-agent wanaosimamia ili hili jukumu liweze kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoto ye yote anauma, lakini akiwa wa mwenziwe, mtu anajifanya punguani anamuona haumi, lakini mtoto anauma na hasa akiwa katika nchi yako akaondoka, akaenda nchi nyingine na nchi yenyeewe ina ubalozi na akafika akateseka bila Wizara kujua au ubalozi kujua na hiyo yote inaelekea kwamba

wanaondoka hawajui, watafute mbinu wanapita vipi, inakuwaje mpaka wanafika waweze kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba bado Wizara ya Fedha kwa bajeti hii ingawa safari hii imepanda kidogo kwa *17 percent* basi waweze kusimamia hii bajeti itoke kwani ikitoka ndiyo manufaa kwa Tanzania. Tunamwona Mheshimiwa Waziri anavyohangaika, anavyokwenda safari zote ndani na nje ili kuisaidia Tanzania na hali tunaiona Tanzania tunavyopiga hatua. Naomba Mheshimiwa Waziri hizi pesa zitoke, Balozi zetu zipate pesa, waweze kufanya kazi na tufaidike. Haitofaidika Balozi itafaidika Tanzania nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe Ruyagwa dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Machano Othman Said dakika tano, Mheshimiwa Salum Rehani ajiandae dakika tano.

**MHE. ZITTO R. Z. KABWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na kutokana na muda nimewasilisha kwa Mheshimiwa Waziri maelezo ya mchango wangu katika maeneo mbalimbali ambayo nachangia ili tuweze kupata majibu ya Serikali. Kwa hiyo, nitachangia maeneo machache tu kutokana na muda ambao umepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, nchi yetu ilijenga heshima kubwa duniani siyo kwa sababu ya utajiri, siyo kwa sababu ya idadi ya watalii ambaao tunao bali ni kwa sababu ya kupigania utu mahali popote pale duniani. Mwaka 1961 wakati tunapata uhuru, usiku wa kuamkia siku ya uhuru tuliweka Mwenge juu ya Mlima Kilimanjaro na Mwalimu Nyerere alitamka maneno yafuatayo:- (*Makofi*)

*'Tunataka kuwasha Mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro, umulike hata nje ya mipaka yetu, ulete*

*matumaini pale ambapo hakuna matumaini, upendo pale palipo na chuki, heshima pale palipojaa dharau.' (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndio umekuwa msingi wa sera yetu ya mambo ya nje miaka nenda miaka rudi. Ndio mambo ambayo Waziri Mahiga, amekuwa akifundisha, ametumikia nchi yetu, amekuwa Balozi wa Umoja wa Mataifa lakini leo mambo ambayo yanatekelezwa tunashindwa kuelewa kabisa kama ni Mheshimiwa Dkt. Mahiga huyu tunayemjua au kuna Mheshimiwa Dkt. Mahiga mpya baada ya kuwa Waziri wa Mambo ya Nje. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetazama kura zote *UN Security Council*, wakati Waziri Dkt. Mahiga anaiwakilisha nchi yetu. Kura zote zilizokuja kupigania wanyonge tulikuwa pamoja na wanyonge, lakini toka mwaka 2016 kura zote tunazopiga kwenye majukwaa ya kimataifa uanzie *UNESCO Parish*, mwezi Oktoba, 2017 na mpaka hivi majuzi ama tuna abstain tunaona aibu kusimama na wanyonge au tunapiga na watu ambao wanawakandamiza watu wengine. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mtu anayekataza nchi yetu kuwa na mahusiano ya kibalozi na Israel. Hata Mwalimu Nyerere hakukataza kuwa na mahusiano na Israel lakini Mwalimu Nyerere alisema kwamba mahusiano hayo yasitufanye tuache kusimamia wanyonge. Mheshimiwa Waziri alikuwa Israel juzi, amekwenda Israel *at the time*, ambayo ndio inawaumiza Wapalestina kuliko wakati mwingine wowote miaka 70 ya Taifa la Israel. Amekwenda kutembelea miji ambayo inapakana na Gaza, kulikuwa na *massacre*. Nchi yetu leo inaona aibu kulaani mauaji ya watu wanyonge wanaokandamizwa, walionyang'anya ardhi yao. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma maelezo ya Wizara ukurasa wa nane mpaka wa tisa, *propaganda* kutaka kuridhisha watu ambao bado wanaamini misimamo ya Mwalimu Nyerere kwamba bado tuna misimamo hiyo, lakini ukitaka kujua hasa nini misimamo ya Serikali kwenye mambo ya kimataifa nenda angalia ukurasa wa 51 mpaka 60 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *No mention of Palestina, no*

mention of POLISARIO, Ame-mention kwenye preamble huku ili kuturidhisha kwamba misimamo yetu haijabadilika, lakini huko amekuja kuzungumzia mpaka mambo ya North Korea huko, *nothing about* watu ambao tumekuwa tukiwapigania.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi watu ambao tumewakomboa South Africa, baada ya *massacre* ya Gaza, wamemwondoa balozi wao, Waziri wetu anakunywa mvinyo na Netanyahu, *the butchery* ya Wapalestina. Anaenda kwenye *television* za Israel, *television* za Taifa anapongeza Israel, anashindwa kutoa neno moja la kulia na watu ambao, sasa mambo yote aliyokuwa anafundisha Mheshimiwa Dkt. Mahiga siku zote ya *foreign* yanaenda wapi? At this age anavunja heshima yake yote ya huku nyuma. Kwa sababu ya nini misaada ya Israel? *POLISARIO, its true, amezungumza rafiki yangu Mheshimiwa Cosato kwamba Algeria wana ubalozi wana... mwisho. (Makof)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Machano Othman Said dakika tano, atafuatiliwa na Mheshimiwa Salum Rehan dakika tano na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma ajandae dakika kumi.

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuchangia mchana huu wa leo. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu na weledi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia Mheshimiwa Masele na Mheshimiwa Mboni kwa nafasi ambazo wamezipata katika Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka nizungumzie baadhi ya majukumu ya Wizara hii na umuhimu wake. Wakati wa bajeti ya Wizara ya Maji Mheshimiwa Waziri wa Maji alizungumzia pia kuhusu mradi wa maji ambao

tunataraja kutoka India. Sasa mradi huu karibu ni mwaka wa tatu naomba Wizara hii nayo itusaidie kutupa maelezo ya ziada kuhusu hatima ya mradi huu wa maji ambao pia na Zanzibar ipo katika mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje katika ofisi za Zanzibar. Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na Kamati naipongeza sana wamezungumzia umuhimu wa kufanywa matengenezo ya jengo la Zanzibar au kujenga jengo jipyä. Kwanza nikiri kwamba lile eneo ni nzuri na liko katika sehemu nzuri na niiombe Wizara ijenge au ifanye matengenezo makubwa kwa jengo lile lakini pia na vitendea kazi kwa ofisi ya Zanzibar. Pamoja na watenda kazi wenyewe bado ni tatizo kwa upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, natarajia Mheshimiwa Waziri hili nalo atalitilia mkazo na kutuletea majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze uamuzi wa Wizara wa Serikali wa kufungua ofisi ndogo au *Council* katika Mji wa Guangzhou na Lubumbashi. Vile vile pia niipongeze sana Serikali kwa kuamua kufungua ubalozi mjini Havana, Cuba kwa masilahi ya Tanzania. Cuba ndio nchi ya kwanza kutambua Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 64, kwa hivyo kwa Cuba, Tanzania ni rafiki wao wa kudumu kwa hivyo nimefurahi nawashukuru na kuwapongeza Wizara kwamba mwaka huu pengine tunaweza tukafungua Ubalozi nchini Cuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine suala la Mahujaji, Mheshimiwa Masoud alizungumza lakini mimi kidogo na tofautiana naye. Ni kweli tunazo fursa na uhuru wa makundi kupeleka mahujaji Makka, lakini mwaka jana kupitia makundi haya haya mahujaji wa Tanzania walipata tabu sana nchini Saudi Arabia. Wengine walitapeliwa na imefikia hatua Serikali ya Saudia kuagiza mahujaji wa Tanzania mwaka huu walipiwe mwanzo kabla ya wakati wa Hija ili kuepusha tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ambalo limewasababisha baadhi ya mahujaji kuwa katika wakati

mgumu kwa sababu kwa utaratibu Mahujaji wanachanga fedha kidogo kidogo ili wawayi nao kutekeleza ibada. Sasa kwa uamuzi huu imekuwa kazi kubwa sana na ngumu. Nimwombe Waziri pia kwa sababu masuala haya ya dini pamoja na kwamba ni Tanzania lakini yanashughulikiwa sehemu mbalimbali, kulikuwa na wazo kwa mahujaji wa Zanzibar kufunguliwa akaunti yao peke yao na mahujaji kutoka Bara wawe na akaunti yao. Sasa sijui Serikali ya Jamhuri ya Muungano imefikia wapi katika suala hili la kuweka sawa ili kupunguza hili suala la utapeli kwa mahujaji wetu na kuweza kupata huduma nzuri katika mji wa Maka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Ubalozi wetu Msumbiji. Msumbiji ukiacha lile jengo kubwa ambalo tumejenga la ghorofa tisa liko kwenye sehemu nzuri lakini pla tunayo majengo mengine yasiyopungua mawill mpaka matatu. Maeneo ambayo tumepewa Msumbiji ni mazuri na wenyewe Msumbiji wanaona wametuheshimu sana kutupa maeneo yale, lakini kwa bahati mbaya tumeshindwa kuyaendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara kama ingwezekana wangebadilisha matumizi ya lile jengo jipya badala ya kulitumia kwa Ofisi ya Ubalozi, tungelitumia kwa kituo cha biashara na yale majengo mengine tukayajenga na tukatumia kwa shughuli za kibalozi ambayo yanatosha sana. Yaani pale fedha nyingi tumetumia lakini tuna maeneo mazuri tunaweza tukawa vizuri zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata wao Msumbiji Tanzania yapo maeneo bado wanadai kwamba walipewa na wamenyang'anywa katika utaratibu ambao hauko wazi. Ukiacha chuo cha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wao umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. KHAMIS YAHAYA MACHANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salum Rehani dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma dakika kumi.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Vilevile niungane na wenzangu wale ambao walimpongeza ndugu yetu Sugu kwa kuweza kurudi hapa Bungeni, baada ya kutoka kifungoni kule Mbeya. Pia tumshukuru Raís kwa kuliona hilo na kuweza kuleta tafifu ya kumrudisha hapa na leo tunaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kusema kwa haraka haraka kulingana na muda suala la kwanza, Tanzania ndani ya tasinia ya Afrika mashariki. Kila tunapokwenda bado hakujawa na mikakati chanya ya kuweza kukabiliana na ushindani iwe wa uchumi, elimu, hata utamaduni. Tunahitaji Wizara ileze kwa undani ni mikakati gani ambayo itaweze kutufanya sisi kama nchi kuweza kukabiliana na tasinia ya ushindani ndani ya *East Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona wenzetu kila siku wanafungua fursa nyingi za kiuchumi katika maeneo yao, lakini bado pamoja na harakati ya miradi ambayo iliyoko ndani ya nchi ya Tanzania haionyeshi *competitive advantage* ya kuweza kushindana na wenzetu ambao wako katika maeneo yetu wakati sisi tuna rasilimali nyingi ambazo zinaweza kutupaisha haraka zaidi kuliko wao. Kwa hiyo, nimwombe Waziri aje atupe maelezo hapa mkakati gani tunao ndani ya utengamano huu wa *East Africa*, kukabiliana na ushindani wa kibashara, ushindani wa kielimu lakini vilevile na kiutamaduni baina ya nchi zetu hizi sita zilizo katika mtengamano huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumza ni suala zima la Balozi zetu zilizo nchi za nje. Bado uwezo wa Mabalozi kuona *output* katika nchi hii ni mdogo. Tegemeo la kupewa *post* hizi hawa Mabalozi tunategemea waitangaze hii nchi kwa vivutio mbalimbali

vya kiuchumi, kiutamaduni na teknolojia vilivyoko ndani ya nchi hii. Hata hivyo, tumeona tu wenzetu Wafaransa juzi balozi amechangamka na kuweza kuleta *delegation* hapa ya Wafaransa kuja kuangalia fursa za uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, na sisi Tanzania tunahitaji kuona tunatoa *delegation* mbalimbali zinakwenda katika nchi mbalimbali kuangalia fursa. Siyo hao tu wafanyabiashara hata nao Wabunge pia wapewe fursa za kwenda nje kuangalia fursa mbalimbali za kiuchumi, kiutamaduni na teknolojia ili waweze kuisemea nchi hii na kuleta matunda ambayo yataweza kuisaidia hii nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vitu vingi ambavyo tunaweza kufanya uwekezaji, lakini tuna miradi mingi ya kimkakati ambayo inaweza kuitoa nchi hii, lakini tunasema miradi hii tumeifungasha sisi wenyewe tu. Wazo langu tuitoe, tuitangaze kama tunaanzisha mradi mkubwa wa *Stiegler's Gorge*, tuitangaze duniani utapata *support*, watu wanahitaji kuuona na kuujua, ziletwe ripoti za hii miradi ili tuweze kuona miradi hii inapata ufadhili, lakini vilevile inapata...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma atachangia kwa huo muda uliobaki.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa kupitia Bunge hili Tukufu naomba nitoe shukurani za dhati kwa Mheshimiwa David Silinde, Mbunge wa Mombasa mwanatimu ya mapambano kwa mashirikiano na juhudzi zake amefanya kazi kwa moyo wa kijasiri na kwa kujitolea mpaka kuhakikisha ushindi wa Mheshimiwa Mboni Mhita, Rais wa *Caucus* ya

vijana, Mheshimiwa Stephen Masele, Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika wamepata ushindi na kulletea nchi yetu heshima kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa taarifa yako kamanda wa jeshi hilo la ushindi si mwininge isipokuwa ni mimi mwenyewe Asha Mshuwa na nampelekea salamu Mheshimiwa Dkt. Magufuli japokuwa mimi hakunialika mimi na Mheshimiwa Silinde lakini sisi ndio tuliofanya mapambano ya *infantryna ya air wing*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la heshima kwa viongozi hawa wawili tulioweza kupata ni vile wameahidi kwamba watatumia lugha ya Kiswahili katika kuendesha shughuli katika Bunge la Afrika. Hii ni turufu kubwa na heshima kwa Tanzania yetu. Tanzania hoyee.

**WABUNGE FULANI:** Hoyeeee!

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo linakuwa na uzito sana...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mshua inabidi tulifute maana wewe umewafanya Wabunge wazungumze bila kuruhusiwa na mimi. Endelea Mheshimiwa Mshuwa.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nakubali. Katika hotuba Waziri amezungumza sana kuhusu *diaspora* na vile wanavyoweza kuchangia. Ni kweli wana-*diaspora* wameongezeka na uchumi wao huko waliko ni mzuri, hivyo wana nafasi kubwa kuchangia hapa kwetu. Sasa Serikali irahishe mazingira ya wao kuweza kuwekeza hapa nchini Tanzania, kwa hili bado halijawa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko mifano kadhaa ya nchi ambazo zimeweza kuwatumia *diaspora* na kuendeleza na kunyanya uchumi wa nchi hizo na kipato cha familia zao. Hasa kwa kuzingatia kama watu hawa wana uchumi mzuri na wanapata *experience* na *exposure* za kutoka katika nchi zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo linanikereketa na naomba Serikali inisaidie na tuweze kupata ufumbuzi ni hili suala la uraia pacha (*dual citizenship*). Suala hili tuiombe Serikali ilifanyie tafakari upya na kulipatia utekelezaji japo kwa masharti. Ikiwezekana basi kama wasiwasi wa kiusalama basi tuweke vipengele ambavyo vitazuia watu hawa wasiingie katika mistari ya kupiga kura au kuhtarisha usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nafikiria na napendekeza kwamba, basi tutazame uwezekano wa kufanya kama ule mfano ambaao wanatumia India. India wao hawana *duals citizenship* lakini wanao utaratibu unaotiya *Person of India Origin*, Wahindi hao wanapewa utambuzi ambaao unawapa haki sawa isipokuwa hawawezi kupata uraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jambo kama hili kwa kutumia watalaam wao watafute namna kama kuwa na timu kabambe kama zile za makinikia ili tuweze kuwasaidia hawa vijana wetu ambaao wako nje huko na wanapoteza nguvu kazi nyingi sana, ambaao wana nia hasa ya kuendeleza rasilimali katika Tanzania yetu na hasa hivi tunavyotaka Tanzania ya viwanda hawa watu naamini wanao uwezo sana wa kutengeneza viwanda hata vidogo vidogo. Mbona hamnipigii makofi, hamtaki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ombi hilo la kuiomba Serikali, sasa naomba tena suala la *pass* ya *diplomatic. Diplomatic Pass* imetoka agizo kwamba wasipewe wenza. Sasa naomba Serikali ifikirie jambo hilo kwa sababu inakuwa haipendezi unasafiri na mkeo au na mumeo japo mimi sina mume lakinina wasemea wenzangu wenyewe waume. Wewe mke unakwenda huku, mume anakwenda kwingine inakuwa haipendezi na hajengi heshima ya nchi. Hata hivyo, tutazame kwa wale watu ambaao wanaongeza wake wengi waliozidi, waliozidi wanne au ishirini, basi waambiwe awekewe wake

zake wawili tu. Kwa sababu tukisema apewe mke mmoja hapa nitaingilia utaratibu hata Mzee Ally Hassan nitakuwa nimemwingilia kwa hivyo atakuwa haweze kuwachukulia wake zake wote wawili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha naomba ukae kidogo.

Waheshimiwa Wabunge kwa Mujibu wa Kanuni ya 28(2) nakusudia kuongeza nusu saa ili tuweze kumaliza shughuli iliyoko mbele yetu, lakini fasili hii inataka niwahoji, hivyo nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaokubaliana na hoja ya kuongeza nusu saa ili tumalize shughuli iliyoko mbele yetu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda. Mheshimiwa Asha Abdallah, endelea. *(Makofii)*

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sasa nasema kwa sababu ukisema apewe mke mmoja tu au mume mmoja inaweza kuleta tatizo kwa sababu mzee wetu wa heshima baba yetu Rais wetu Ali Hassan anao wake wawili. Sasa utakuwa upendeleo ukisema mmoja aende. Kwa hivyo wakae watazame namna gani wata-sort out jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu viwanja vya ubalozi. Nchi yetu tulipata heshima kubwa na viwanja vingi tulipata kwa heshima ya mwenyewe hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, lakini viwanja vingi mpaka hivi sasa hivi bado havijaendelezwa. Sasa tubadilike tutafute namna hata kushirikiana na *investors* wengine sio tu haya majengo yawe kwa ajili ya ubalozi lakini tuweze kufanya shughuli nyingine kwenye majumba yale kujenga ofisi, kupangisha na kufanya ubalozi. Maana yake hiyo tunu tuliyopewa mwisho itapotea, nyota ile tuliondoka nayo itapotea, majengo yetu mengi hayako katika hali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutumie hii nafasi ya kidemokrasia ya kiuchumi kushawishi ili tuweze kuviendeleza viwanja hivyo, lazima kuwe na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa fedha zilitengwa kwa mfano wa kujenga jengo la Oman lakini hazikuweza kupatikana. Sasa nataka nishauri kwa vile Oman ni rafiki zetu sana na nimeona hapa kwenye hili ripoti wanasaidia kukarabati Bete la Jaibu basi tutafute namna kwa kushirikiana kwa mazungumzo kama vile wafalme wengine wanaweza kuja kutujengea uwanja au kama marehemu Gadafi alivyojijengea misikiti na hao watusaidie kujenga hili jengo la ubalozi pale Oman itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kumuuliza Mheshimiwa Waziri...

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili tayari Mheshimiwa.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Muda wangu umeisha?  
*Astaghfiru-Allah!* Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Suzan Kolimba na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendelea kuiweka Tanzania katika ramani ya dunia kwa masuala ya uhusiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napenda kuendelea kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Rais wetu mpewda Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa kazi nzuri na kubwa ya kujenga Tanzania ya viwanda na maendeleo ya uchumi wa kati.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi naomba sasa nichangie hoja ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ipatie kipaumbele haja ya kurekebisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuruhusu raia wake kuweza kuwa na uraia pacha (*Dual Citizenship*). Nionavyo kuna faida kubwa kuliko hasara kama Watanzania wanaopenda kuwa na uraia wa nchi mbili watahalalishwa kufanya hivyo, kwani kwa kufanya hivyo, tunajiongezea fursa za kiuchumi na kijamii, hasa kwa Watanzania wenzetu wanaoishi na kufanya kazi nchi za nje (*The Diaspora Community*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika ya Mashariki. Ingawa hotuba ya Waziri inatamka bayana katika ukurasa wa 28, aya ya mwisho kuwa, wananchi na hasa vijana washiriki katika kuchangamkia fursa zilizoko kwenye soko la Jumuia ya Afrika Mashariki, hali ilivyo sasa kwa wasafiri wanaotumia Hati za Dharura za kusafiria siyo rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani Hati za Dharura za Kusafiria zilikuwa zinatolewa kwa kuruhusu kutumika kwa *multiple entries* kwa muda wa mwaka mmoja, lakini kwa sasa na kwa sababu ambazo wananchi wanaosafiri mara kwa mara kwenda na kurudi katika nchi jirani zetu Afrika Mashariki hupewa hati za dharura ambazo zinaruhusu *single entry visa* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kumaanisha kuwa, mara msafiri anapopita kwenda nchi ya jirani, mfano Kenya, kwa wajasiriamali wa mpaka wa Kenya na Tanzania, Namanga, ambao hufanya biashara katika masoko ya nchi jirani kila wiki hulazimika kukata hati mpya ya dharura ya kusafiria kila *trip* hata kama atasafiri kwenda na kurudi kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili siyo rafiki kwa uchumi wa wananchi na vijana wanyonge ambao Itifaki ya

Soko la Pamoja illenga kuwasaidia. Gharama ya hati kwa kila safari ni wastani wa Sh.20,000/= na kama msafiri atahitaji kwenda Kenya mara tano kwa mwezi, kwa mfano, atalazimika kutumia hadi Sh.100,000/= kwa hati ya kusafiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri na kuiomba Serikali watengeneze mazingira rafiki ya ama kurejesha Hati za Dharura ambazo ni *valid for multiple entries for one year* au utoaji wa Pasi za Afrika Mashariki urahisishwe na kuwezekana kutolewa mpakani tofauti na sasa ambapo ni mpaka maombi yapelekwe Dar-es-Salaam na kuchukua zaidi ya miezi sita mpaka msafiri apate pasi hiyo, au ikubalike sasa kuwa, Watanzania waruhusiwe kusafiri nchi za Jumuiya yetu kwa kutumia vitambulisho vyao vya Kitaifa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu na Watendaji wote walioko katika Wizara hii. Pamoja na pongezi nina machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itenye fedha za kutosha kwa Balozi ambazo zinatumika nchi tatu mpaka tano ili Balozi aweze kuzitembelea na kutafuta fursa za kiuchumi kama utalii, viwanda na usalama na uwakilishi uwe wenyе manufaa katika nchi hizo. Ofisi za Ubalozi zitengewe fedha za ukarabati wa ofisi za ubalozi na nyumba za watumishi katika Balozi husika ili ziendane na hadhi ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vya Ubalozi ambavyo havijajengwa vitengewe fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Ubalozi na makazi ya Balozi zetu na watumishi wake. Kwa mfano, kiwanja cha Ubalozi Jijini London kimetelekezwa na kimejaa magugu na mbwa mwitu. Kila ofisi za Ubalozi wetu nje ya nchi ziwe na wataalam wa fani ambazo zitasaidia kuiuza nchi yetu kiutalii, kiutamaduni, lugha ya Kiswahili, kuvutia wawekezaji kuja Tanzania kujenga viwanda, Kujenga hospitali za kitalii kwenye website ya kila

Ubalozi kuwe na vivutio vyote vilivyoko katika nchi yetu ili kila mtalii aamue ni eneo gani anapenda kwenda kutalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, kuna mazoea ya kuona vivutio vichache tu Serengeti *National Park*, Mlima Kilimanjaro, Ngorongoro Crater, Zanzibar lakini ukiangalia nchi yetu ina vivutio vingi sana kama, Kitulo *National Park*, Ruaha *National Park*, Manyara *National Park*, Mahale *National Park*, Maporomoko ya Kalambo (Rukwa), Gombe *National Park*, Saa Nane *Island*, Arusha *National Park*, Tarangire *National Park*, Udzungwa *National Park*, Kilimanjaro *National Park*, Serengeti National Park, Selou *National Park*, Majengo ya Kale Kilwa, Mafia, Bagamoyo, Olduvai George, Nyagoza Mtu wa Kale, Mapango ya Amboni Tanga, Kaburi la Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere – Butiama, Fukwe za Bahari, Utalii wa *Water Sports* (Bahari na Maziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa - Matema Beach). Maeneo ya kale Mtwara Mikindani na Utamaduni wa Ngoma za asili na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vivutio hivyo vyote na vingine ambavyo sikuvitaja viwekwe kwenye matangazo mbalimbali duniani na hasa ziwekwe kwenye *website* za kila Balozi zetu nje ya nchi. Balozi ziandae maonesho kwa lengo la kuitangaza nchi yetu ya Tanzania, katika sekta za utalii, kiutamaduni na kutumia fursa ya kijiografia ya nchi yetu kupakana na nchi zaidi ya tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. FATMA H. TOFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa ya kuchangia kwa maandishi. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kuwa ofisi za Ubalozi zimepewa jukumu la kutoa *Visa* kwa wageni mbalimbali wanaotaka kufika nchini kwa shughuli mbalimbali, suala la *Visa* rejea. Katika utoaji wa *Visa* rejea kumekuwa na ucheleweshaji sana kuwapata waombaji

wanaotoka katika zile nchi ambazo nchi yetu inawapatia *Visa* hizo. Kuna nyakati *Visa* rejea hutolewa baada ya miezi mitatu na wakati mwingine waombaji hawapati majibu kabisa. Hii inaleta adha kwa wale wageni wanaotoka kuja pamoja na Maafisa Balozi. Hali ya kuchelewa au kutopata *Visa* rejea, husababisha Serikali kukosa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kulipitia upya sharti la *Visa* rejea ili kwenda na wakati kwa kufungua milango ili wageni waweze kuingia. Mfano watalii, wawekezaji, wafanyakashara na wageni wengine ambao huja kwa shughuli za mikutano na ziara za utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya ada ya *Visa* kuwa juu na kwa dola. Kuna baadhi ya mawakala wamekuwa wakitoa pesa juu sana kwa ajili ya *Visa* mfano baadhi ya mawakala wa Saudi Arabia wamekuwa wakitoza ada si chini ya dola 600, sambamba na hilo kuna baadhi ya mawakala hawana ofisi maalum, ni budi Wizara kufanya uhakiki wa mawakala wote ili kuwaondolea adha Watanzania kulanguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 66 ajira mpya, pamoja na kupata kibali cha kuajiri watumishi 10 bado ofisi nyingi za Ubalozi zina upungufu wa wafanyakazi wanadiplomasia. Hebu Serikali ifanyile kazi ili wapatikane na kutosheleza ili kuleta ufanisi katika utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi za kazi nje ya nchi. Tanzania imekuwa ikisisitiza umuhimu wa Watanzania wana *diaspora* waishio nje kuchangia uchumi wa Taifa letu kwa kuleta mapato wapatayo huko ughaibuni. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha jambo hili linaenda sawa na kuleta tija kwa nchi? Mkakati upoje ili Watanzania wote waishio ughaibuni wafahamike wapo nchi zipi na wanafanya kazi au shughuli zipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia kwa maandishi na naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi si Tanzania ya Nyerere, ni Tanzania mpya, Tanzania mbaya inayokalia kimya mauaji ya kinyama ya Wapalestina na kuunga mkono waonevu.

(i) Msimamo wa Tanzania kuhusu Palestine (aya 18 ya Hotuba ya Waziri), maelezo ya Serikali hayaendani na matendo. Tanzania imewatupa mkono wanyonge wa Palestine.

(ii) Msimamo wa Tanzania kuhusu Sahara Magharibi (aya 19 ya Hotuba ya Waziri), kuna dalili zote kuwa Serikali inataka kuwafukuza *POLISARIO* baada ya kuikumbatia Morocco.

(iii) Unafanyaje diplomasia bila wanadiplomasia? Vituo vingi nje havina *FSOs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Tanzania kuhusu mgogoro wa Israel na Palestina unaelezwa vizuri sana na nukuu hii ya Mwalimu Nyerere alioitoa mwaka 1967 na ndiyo umekuwa msingi wa Sera yetu ya Mambo ya Nje kwa miaka mingi kabla ya utawala wa sasa wa CCM mpya.

*"....Tanzania's position. We recognize Israel and wish to be friendly with her as well as with the Arab Nations. But we cannot condone aggression on any pretext, nor accept victory in war as a justification for the exploitation of other lands, or Government over other peoples."*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba Tanzania inaitambua Israel na inapenda kuwa na urafiki nayo pamoja na urafiki na mataifa mengine ya kiarabu, lakini hatuwezi kukalia kimya uvamizi kwa namna yoyote ile, pia ushindi vitani hauhalalishi unyonyaji dhidi ya ardhi ya wengine au dhidi ya Serikali za watu wengine. Msingi huu unaendana kabisa na dhamira ya sasa ya Sera ya Mambo ya Nje. Hata hivyo, hali ni tofauti kabisa. Mambo tunayoyayafanya kwenye Sera yetu ya Mambo ya Nje yanamfanya Mwalimu Nyerere ageuke huko kaburini kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaeleza kwa mifano, 26 Oktoba, 2016 kulikuwa na kikao cha Wajumbe wa Nchi 21 zinazounda ‘Kamati ya Urithi wa Dunia’ ya UNESCO-Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni kupiga kura ya kuitisha makubaliano ya kuridhia kuupa hadhi ya urithi wa Dunia Mji wa Jerusalemu pamoja na moja ya majengo ya Mji huo (*Temple Mount*) na kufungamanishwa na uasili wake na si hali ya sasa inayotokana na uvamizi wa Israel juu ya eneo hilo lilioloko Jerusalemu Mashariki (liliolovamiwa mwaka 1967 na mpaka leo kutambuliwa na UN kama eneo la Palestina, ambao wanauona ndiyo Mji Mkuu wa nchi ya Palestina iwapo makubaliano ya ‘*Two States Solution*’ yatafikiwa).

Mheshimiwa Naibu Spika, ACTWazalendo tulihoji juu ya jambo hili linalokwenda kinyume na Sera ya Nje ya nchi yetu. Msimamo wa Tanzania ni kukubaliana na UN kupinga uvamizi wa eneo hilo uliofanywa na Israel. Serikali ilitoa majibu mepesi tu, tena pembeni kuwa upigaji wa kura ule haukuwa msimamo rasmi wa nchi yetu ni ukiukwaji wa sera yetu ya Mambo ya Nje na kuwa ni jambo ambalo Afisa wetu kwenye mkutano ule wa UNESCO alilifanya kwa makosa na hivyo hatua zingechukuliwa dhidi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri hayo yalikuwa ni ghiliba tu, matukio ya karibuni yameonesha kwa uwazi sura mpya ya Taifa letu pamoja na msimamo mpya wa Sera yetu ya Mambo ya Nje. Kwenye diplomasia matendo ya nchi huwa na maana zaidi kuliko maneno ya wanadiplomasia wake, matendo yetu yafuatayo ya karibuni yameonesha kuwa Tanzania hatuiungi mkono tena Palestina.

(1) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwaangusha Wapalestina kule Paris kwenye Mkutano wa UNESCO, Serikali iliahidi kuwa ingemchukulia hatua Afisa yule wa Wizara ya Mambo ya Nje aliyekwenda kinyume na Sera yetu ya Mambo ya Nje, hatujafanya hilo zaidi tumempandisha cheo na kumteua kuwa Balozi Elizabeth Kiondo apige kura namna ile kule UNESCO na sasa tumempa cheo zaidi kwa kazi njema aliyoifanya. Jambo hili linaonesha kuwa kwa sasa

tunawaunga mkono Waisrael na hatuko tena na Wapalestina.

(2) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tumeamua kufungua Ubalozi wetu Israel, Tel Aviv, kuongeza uchungu kwenye kidonda, tukachagua wakati huu wa maadhimisho ya miaka 70 ya uvamizi wa Israel ardhi ya Taifa la Palestina kuzindua ubalozi wetu huo. Jambo hili linafanyika kukiwa na tuhuma kuwa hata huo ubalozi unagharamiwa na Israel yenye, ndio maana tumepangiwa hata kipindi cha kuufungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kidiplomasia kuufungua ubalozi wetu katika wakati huu ni kuadhimisha uvamizi wa Israel katika ardhi ya Palestina. Maana tulikuwa na uwezo wa kuchagua wakati mwingine wowote kufanya uzinduzi wa ubalozi wetu, lakini kwa kuwa aliyegharamia uwepo wa Ubalozi huo (Israel) alitaka tuufungue wakati huu wa maadhimisho ya miaka 70 ya uvamizi wa Israel kwa Palestina, ilitubidi tufanye hivyo. Jambo hili limeonesha kuwa kwa sasa hatuungi mkono tena utu (Palestina) bali tunamtumikia kila mwenye kitu (Israel).

(3) Mheshimiwa Naibu Spika, wakati akiwa ziarani Israel, Balozi Dkt. Mahinga alifika sehemu ya miji inayokaliwa kimabavu na Israel ambayo inapakanu na ukanda wa Gaza, na baadaye alihojiwa na Televisheni ya Taifa ya Israel ambako alionesha tu masikitiko yake kwa Waisrael wanaokaa maeneo hayo kwa kusumbuliwa na mashambulizi ya Hamas, lakini hakulaani kabisa uendelezaji wa Israel kujenga makazi kwenye maeneo hayo ya uvamizi kama wanadiplomasia wengine wa nchi zenye msimamo wa '*Two States Solution*' kama sisi wanavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi Dkt. Mahinga mwanadiplomasia mzoefu na mbobezi, kutokulaani kwake makazi yale haramu ni jambo la makusudi kabisa, si bahati mbaya. Ni kitendo cha kutuma salamu kwa Wapalestina kuwa tunaunga mkono uendelezaji makazi wa Israel katika maeneo hayo iliyoavamia.

(4) Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imetajwa na vituo mbalimbali vya habari vya Kimataifa kuwa ni katika nchi 33 ambazo zilihudhuria ufunguzi wa Ubalozi wa Marekani Mjini Jerusalemu, Mei 14 kilele cha maadhimisho ya miaka 70 tangu uvamizi wa Israel katika maeneo ya Wapalestina. Chanzo cha taarifa ya Tanzania kuhudhuria ni Serikali ya Israel, ikitaja nchi ilizozialika na zilizohudhuria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu inasema inapinga uwepo wa Ubalozi wa Marekani Mjini Jerusalemu, lakini hapo hapo inatajwa kuhudhuria uzinduzi huo. Picha tunayoitoa hapa kwa Wapalestina ni kuwa tunaunga mkono jambo hili la ufunguzi wa Ubalozi wa Marekani Mjini Jerusalemu.

(5) Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya uzinduzi huo wa ubalozi wa nchi ya Marekani Mjini Jerusalemu, Jeshi la Israel liliwua kwa risasi zaidi ya watu 54 wa Palestina, waklwemo wanawake, watoto, walemavu na hata wanahabari. Nchi mbalimbali duniani zimelaani mauaji hayo. Nchi ya Afrika ya Kusini imekwenda mbali zaidi kwa kumrudisha nyumbani Balozi wake aliyeko Israel. Tanzania tulivoikombwa Afrika ya Kusini tumekaa kimya, tumeshindwa hata kutoa kauli ya kulaani mauaji hayo. Kuhudhuria kwetu ufunguzi wa ubalozi na kukaa kimya juu ya mauaji hayo kunaonesha tumewaacha rasmi Wapalestina.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo hayo matano yanaonesha kuwa sisi si tena ile Tanzania ya Mwalimu Julius Nyerere, sisi kwa sasa ni Tanzania mpya (kama yasemavyo matangazo ya lkulu yetu) – Tanzania mpya inayosimama na waonevu wa dunia, wauaji na wavunja haki za wanyonge. Sisi si tena Tanzania ya kusimama na wanyonge, bali ni Tanzania ya kusimama na wanyongaji kwa sababu ya maslahi ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, si ile Tanzania iliyongoza ukombozi wa Bara la Afrika kutoka kwenye makucha ya ukoloni, bali ni Tanzania mpya inayounga mkono na kushabikia ukoloni na uvamizi. Sisi si ile Tanzania yenye msimamo mkali tulioinga Taifa kubwa la Marekani dhidi ya

uvamizi wake kwa wanyonge wa Taifa la Vietnam, bali sasa ni Tanzania mpya ya kuunga mkono uvamizi wa Taifa onevu la Israel kule Palestina.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi si Tanzania ile ilioitetea China ipate nafasi na Kiti chake stahili kule *UN*, bali sasa sisi ni Tanzania mpya inayowaacha watu wa Palestina bila utetezi wa hadhi, kiti na nafasi yake stahili kule *UNESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi si ile Tanzania huru tena ya Mwalimu Nyerere, iliyowaheshimu watu na Mataifa kwa sababu ya utu wao na kuamini kwamba binadamu wote ni sawa. Sasa sisi ni Tanzania mpya, inayowapa heshima watu kwa sababu ya kitu inachotuhonga, tukiiza usuli wa Utaifa wetu kwa maslahi machache ya kifedha au kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwashi tena Mwenge na kuuweka Mlimani Kilimanjaro, hatumuliki tena nje ya mipaka yetu, hatuleti tena matumaini pale pasipo na matumaini, hatupeleki tena upendo kule kuliko na chuki na hatuleti heshima pale palipojaa dharau. Sisi si Tanzania ya Mwalimu Nyerere, sisi sasa ni Tanzania mpya, Tanzania mbaya, Taifa liliokiuwa misingi yake, Taifa linalowaacha Wapalestina wakiuawa kinyama na sasa linalosapoti waonevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujengewa uwanja wa mpira na msikiti visiifanye Tanzania likumbatie Morocco na kuacha kuiunguza mkono Sahara Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado niko kwenye Sera ya Mambo ya Nje ya Nchi yetu, si hii ya Tanzania mpya bali ile Tanzania ya tangu wakati wa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ya kusimama na wanyonge. Wakati tulipoamua kufuata 'Diplomasia ya Uchumi' bado msingi wetu huu wa kusimama na wanyonge ulibaki palepale. Ndiyo maana wakati wa Rais Benjamin Mkapa na Jakaya Kikwete bado tulibaki kuwa ni sauti ya Mataifa yanayoonewa kama Cuba (tukipinga vikwazo vyatvya Marekani dhidi yao), Palestina na Sahara Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi huo wa kusimama na wanyonge ni muhimu zaidi kwa Chama chetu cha *ACT* Wazalendo, ndiyo maana tulipinga ujio wa Mfalme wa Morocco hapa nchini tarehe 23 - 25 Oktoba, 2016. Kwa kuwa Taifa hilo bado linaikalia kimabavu ardhi ya wanyonge wa Sahara Magharibi, ndiyo msingi pia wa kutangaza wazi mahusiano yetu rasmi na Chama cha Siasa na Ukombozi wa Taifa hilo cha *POLISARIO* kinachopigania uhuru wa nchi ya Sahara Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wa Afrika (*AU*) uliamua kukubali ombi la Morocco kurudi bila masharti kwenye Jumuiya hiyo. Ikumbukwe kuwa kwa zaidi ya miaka 33 Morocco haikuwa na mahusiano na Jumuiya hiyo (tangu *OAU* mpaka sasa *AU*) baada ya kujitoa kwa kupinga *OAU* kuitambua Sahara Magharibi kama Taifa huru na kupewa Kiti rasmi ndani ya *OA* mwaka 1984.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa *OAU* wa kuiruhusu Sahara Magharibi kuwa mwanachama wa umoja huo ultokana na hukumu ya Mahakama ya Kimataifa ya Haki (*International Court of Justice-ICJ*) ya mwaka 1975 iliyopinga madai ya Morocco kuwa ina mahusiano ya kihistoria na kisheria na Sahara Magharibi (na hivyo kuitawala kinguvu) na kutoa haki ya kujitawala kwa Taifa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaheshimu maamuzi yale ya mkutano wa *AU* uliofanyika Januari, 2017 ulioirudisha Morocco kwenye *AU*, lakini tabia za Taifa hilo onevu bado hazijabadilika, hivyo ni muhimu tulieleze Bunge hili Tukufu masuala yafuatayo ili liweke msimamo wake kwa Serikali juu ya kuminywa kwa watu wa Sahara Magharibi:-

(1) Kikao cha *AU* cha tarehe 28 - 29Januari, 2018 kiliazimia kuwa Morocco iruhusu Kamati Maalum ya Uangalizi ya *AU* iende kwenye maeneo ya Sahara Magharibi ambayo inayakalia kimabavu ili kuja kujulisha *AU* hali ya mambo ilivyo.

(2) Tarehe 29 Machi, 2018 Morocco iliwajulisha *UN*juu ya kutoruhusu waangalizi wowote wa *AU* kwenda kwenye maeneo yote ya Sahara Magharibi inayokalia.

(3) Tangu mwaka 1991 Morocco imetumia mbinu, hila na uzandiki ili kuzuia Tume ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya kura ya maoni ya uhuru wa Sahara Magharibi (*MINURSO*) kufanya kazi yake kwenye maeneo inayoyakalia kimabavu ya Sahara Magharibi. Siku za karibuni Umoja wa Mataifa (*UM*) ulipitisha Azimio Na. 2414 (2018) la kuongeza muda wa mamlaka, uhai na madaraka ya *MINURSO* kwa miezi sita, Morocco imepinga jambo hilo na kutishia kufanya mashambulizi ya kijeshi kwenye maeneo ya Sahara Magharibi ambayo yameshakombolewa (*Liberated Zones*).

(4) Bado Morocco inaendeleza uvunjaji mkubwa wa haki za binadamu kwa watu wote wa Sahara Magharibi wanaodai uhuru wao.

(5) Kurudishwa kwa Morocco kwenye *AU* kulienda pamoja na Taifa hilo kuridhia '*AU Constitutive Act*' inayotaka Mataifa ya Afrika kuheshimu Maazimio ya *AU* na hata yale ya *UN* yanatolewa kwa ushirikiano na *AU*. Hata hivyo, kwa matendo yake tulivoyaainisha hapo juu ni dhahiri kuwa Morocco haitaki usuluhishi na Sahara Magharibi, bado inataka kuitawala na kuikalia kimabavu, ndiyo maana imekataa hata kumpa ushirikiano msuluhishi wa mgogoro huu, Ndugu Horst Kohler Rais wa zamani wa Ujerumani.

(6) Matendo ya Serikali yetu kwa sasa yanaonesha hatuna msimamo kwenye mambo ya msingi ya kidiplomasia, namna tulivyoenenda kwenye mahusiano yetu na wanyonge wa Palestina ni mfano hai, sasa tukijali vitu kuliko utu kama ilivyo zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, nataka kulishawishi Bunge lako litoe mwongozo kwa Serikali juu ya kuenenda kwenye hili jambo la Morocco na Sahara Magharibi ili kuzuia

ahadi ya kujengewa uwanja na msikiti na Serikali ya Morocco. Vitu visitufanye tuwaache ndugu zetu wanyonge wa Sahara Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni kimbilio la nchi ya Sahara, Serikali yetu chini ya Mwalimu Nyerere ililitambua Taifa la Sahara Magharibi tangu siku za mwanzo kabisa za harakati zao, ndiyo maana wanao Ubalozi hapa nchini. Kumuenzi Baba wa Taifa na kulinda misingi ya Taifa letu ni lazima tusimame na watu wa Sahara Magharibi na tusiwatupe kama tulivyofanya kwa watu wa Palestina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naliomba Bunge liibane Serikali ili itoe ahadi hiyo hapa Bungeni, pamoja na kuitaka Serikali kutumia ushawishi wake kule *AU* na *UN* kuibana Morocco iruhusu kura ya maoni ya kuamua mustakabali wa watu wa Sahara Magharibi kama ilivyordhiwa kwenye Azimio la *UN*. *Viva Sahara Magharibi*, *Viva POLISARIO*, Mungu Ibariki Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Diplomasia bila wanadiplomasia, tuna uhaba mkubwa wa Watumishi kwenye Balozi zetu. Msingi wa tano wa Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania unatutaka tushirikiane kikamilifu na nchi, Mashirika pamoja na Taasisi mbalimbali katika nyanja za Diplomasia, siasa, uchumi, utaalam na teknolojia. Wizara hii ina jukumu la kubuni na kusimamia utekelezaji wa misingi yote ya sera yetu ya mambo ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara hii pia ina jukumu la kusimamia na kuratibu mahusiano kati ya Tanzania na nchi pamoja na mashirika mbalimbali. Utimizaji wa jambo hilo unafanyika kupitia Balozi zetu zilizotapakaa kwenye nchi mbalimbali ulimwenguni. Kwa sasa ufanisi wetu si mkubwa kwa sababu ya uhaba wa Watumishi kwenye Balozi zetu mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wastani ukimwondoa Balozi, kila kituo cha Ubalozi wetu nje ya nchi kinapaswa kuwa na Mhasibu, mtu wa *TISS* pamoja na mwanadiplomasia

(*FSO*). Vituo vingi vya Balozi zetu havina kabisa Maafisa wa Diplomasia (*FSO's*), wale wachache waliokuwepo awali walirudishwa nchini kwa sababu mbalimbali (ikiwemo kumaliza muda wao wa Utumishi Nje ya Nchi). Tumerudisha watu bila kupeleka mbadala wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Balozi zetu mbalimbali Watendaji hasa wa kazi za Kibalozi na Kidiplomasia ni hawa Maafisa wa Diplomasia (*FSO's*). Sasa kwa uhaba huu tunawezaje kufanya diplomasia ya nchi yetu? Hiyo Diplomasia ya Uchumi tunafanyaje bila kuwa na hao wanadiplomasia?

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa tu mfano wa Balozi zetu chache ulimwenguni, China nchi ambayo ni mshirika wetu mkubwa kidiplomasia na kiuchumi, hatuna kabisa *FSO* huko, labda ndiyo sababu mauzo yetu kwenda China yameshuka mno, maana biashara ya nje ni diplomasia. Sasa wakati unamtaka ndugu yangu Charles Mwijage asafiri ni nani atakayemuandalia hiyo mikutano ya kupata wawekezaji huko China kama hatuna *FSO* hata mmoja? Wenzetu Uganda wana *FSO's* nane huko China, Kenya na Sudani wao wanaao tisa kila mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nydingine ambayo hatuna *FSO* ni Ethiopia-Makao Makuu ya *AU*, utaona tunavyodharau nafasi yetu katika Afrika. Pia hatuna *FSO* Afrika Kusini, nchi rafiki na moja ya zenye uchumi mkubwa Afrika, hatuna kabisa *FSO* Ujeruman, nchi kubwa zaidi kiuchumi katika Umoja wa Ulaya (*EU*). Hata India ambako tangu Bunge lianze Wabunge tunalalamikia kukosa soko la mbaazi kutoka huko nako hatuna *FSO* hata mmoja. Tumeufanya kuwa ubalozi wa kupokea wagonjwa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za *BRICS* (ukiondoa China, India na Afrika Kusini ambazo hatuna kabisa *FSO's*) zilizobaki, Brazili na Urusi tuna *FSO* mmoja mmoja tu. Hata *DRC Congo* nchi ambayo zaidi ya theluthi moja ya mizigo ya *transit* inapita kwenye bandari ya Dar es Salaam inatoka, nayo tuna *FSO* mmoja tu tofauti na watatu ilivyozoleka.

Kenya nchi ya Afrika Mashariki tunayofanya nayo biashara zaidi nayo ina *FSO* mmoja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali iko hivyo karibu katika Balozi zetu nydingi ulimwenguni, *FSO's* ndiyo Maafisa hasa waliyofundwa na kupikwa kutekeleza sera yetu ya Mambo ya Nje. *Foreign Service Officers (FSO's)* ndiyo *diplomats* (wanadiploma wetu). Kama hawapo vituoni na hatuwatumii maana yake hatufanyi diplomasia na kwa kuangalia mbali tunaua diplomasia yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitapitisha bajeti hii mpaka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki itakaponihakikishia kuwa itapeleka Maafisa wa Diplomasia (*FSO's*) katika vituo ambavyo hatuna kabisa na pia kuwaongeza katika vile vituo ambavyo wako wachache.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi katika Wizara hii. Naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Nampongeza Katibu Mkuu na Naibu wake na watendaji wote na Wakuu mbalimbali wa Idara zote zilizoko Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana na kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa dhamira yake ya dhati ya kutaka kuinua Taifa letu katika Diplomasia ya Uchumi na uhusiano mzuri na Mataifa mengine duniani kwa kuwapa nafasi wataalam wake kufanya kazi hiyo bila yeye kukanyaga katika nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakika uamuzi wake wa kuwaamini na kuwapa nafasi wataalam wote wakiwepo Mabalozi wetu wote walioko nje ya nchi na waliopo ndani ya nchi. Uwezo wao wa uzalendo wao, tumeuona kwani mahusiano ya Taifa letu yamezidi kuwa mazuri na kuimarika, kiuchumi, kiusalama na kisiasa, ahsante sana Mheshimiwa Rais na hongera sana watendaji na Mabalozi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kazi kubwa sana inayofanywa na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu ya kumwakilisha Mheshimiwa Rais kwenye mikutano mbalimbali na majukumu mbalimbali ya Kimataifa, huko nako hatujapungukiwa. Pia pongezi kwa Mabalozi ambao wao wako hapa Tanzania, lakini nchi nyingine ya kuibua mazuri yote kwenye Kanda wanazosimamia mfano, Mabalozi wanaosimamia Idara mbalimbali kama; Mashirika ya Kimataifa, Kanda ya Afrika, Kanda ya Asia, Kanda ya Ulaya na Kanda ya Amerika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana hawa balozi wanaosimamia Kanda hizi. Kwani mambo yanaenda vizuri sana tumeona viongozi mbalimbali wakija nchini na wafanya biashara wengi wakija nchini kwetu, pongezi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nipongeze utaratibu nzuri sana ambao Wizara imefanya wa kuleta vitabu ambavyo vina anwani za Balozi zote zilizoko nje ya nchi na ndani ya nchi yetu, pongezi sana. Pia kitabu kizuri cha utekelezaji wa diplomasia ya Tanzania kuelekea uchumi wa viwanda 2020. Utaratibu huu ni mzuri sana, naomba uendelee na ikiwezekana, angalau kuonyeshwe na moja ya fursa iliyoko katika nchi husika. Pongezi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri kuhusu nyumba na majengo ya baadhi ya Balozi zetu nje. Majengo haya yanatia doa nchi yetu kwa uchakavu. Naomba Waziri alipeleke shauri hili kwenye Baraza la Mawaziri ili jambo la bajeti ya kukarabati nyumba hizi lichukuliwe na Hazina, Wizara haitaweza bajeti yake ni ndogo. Mfano, nyumba za London niliwahi kwenda, haziridhishi. Naomba sana u-smart wa mtu humpa heshima kwa wanaomtazama. Hivyo, tunaweza tukadharaulika na Mataifa mengine kutokana tu na uchakavu wa majengo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na utaratibu wa kubadilishana wafungwa, Je. Serikali inasemaje juu ya kuwarejesha Watanzania ambao wamehukumiwa kwa makosa mbalimbali duniani?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, usalama wa Watanzania wanaoishi nchi za nje, suala hili limekuwa na changamoto kubwa sana kwa Watanzania wenzetu wanaojishughulisha na mambo mbalimbali ikiwemo kutafuta kazi za ndani na masuala mbalimbali yanayohusiana na biashara. Wanapopata matatizo wanaobeba jukumu ni ndugu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutumia diplomasia kwa wafungwa kwenye magereza zilizopo nje ya nchi kuwaomba waje watumikie kifungo kwenye nchi yao kwa maana ya Tanzania ili kuendelea kujenga ushirikiano mzuri. Kutumia balozi zetu kunufaisha Taifa letu. Serikali ifuatilie kwa karibu utendaji wa Mabalozi na kuwapa semina elekezi kwa kutazama uhitaji wa Taifa letu kwa wakati huo na kuwakumbusha wajibu wao ili Taifa letu liweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la diplomasia ya uchumi; jambo hili ni vyema likapewa kipaumbele kwa kuwa Taifa letu bado linakua na kujenga ukaribu kwa mataifa ambayo ni marafiki zetu ili kukuza uchumi wa Taifa letu. Kutumia diplomasia Serikali itumie fursa hiyo kutafuta masoko ya mazao ya biashara. Suala hili halijatunufaisha kama Taifa kuwa na manufaa ni pale ambapo tutatumia nafasi hiyo inapotokea na ziada ya kutosha na tukawa na ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha ya Kiswahili, suala hili tumelizungumza sana, nashauri Serikali kuititia diplomasia kushawishi nchi marafiki kutumia lugha ya Kiswahili ambayo itasaidia kwa Taifa letu kwa wakufunzi ambao watakuwa Watanzania na kama Taifa tutanufaika kwa kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutumia Ziwa Tanganyika, Victoria na Ziwa Nyasa kwa kuwa mazingira haya kushirikiana katika uvuvi ni vyema kama Taifa tukawa na uvuvi wa kisasa utakaoleta tija kwa Taifa letu badala ya kuchoma nyavu zetu za wavuvi. Kutumia Watanzania wanaoishi nje ya nchi

kunufaisha Taifa letu. Tukiwatumia vizuri Watanzania hawa katika biashara na katika elimu tutapata manufaa makubwa hasa pale ambapo na wao watatambua kuwa Taifa linatambua uwepo wao kule waliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliopelekwa kusoma nje ya nchi, Serikali kuptitua ubalozi watumie nafasi zao kushawishi na kuomba wanafunzi hawa kupunguziwa ada au kufutiwa kabisa ili kuwatia moyo wazazi na walezi ambao wamejitolea kuwapeleka watoto au ndugu kusoma nje ya nchi kwani ni kwa manufaa ya nchi nzima.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema. Pia nawatachia Waislam wote Tanzania na duniani kwa ujumla Heri na Baraka ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhanii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahusiano ya Kimataifa; Tanzania bado ni nchi inayotambulika kuwa bado amani na utulivu unapatikana, lakini kadri siku zinavyokwenda mbele Tanzania inapoteza heshima na umuhimu tunaopewa na dunia. Mfano, moja, demokrasia inaminywa kwa kutoruhusiwa mikutano ya hadhara ya Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, maiti zinazookotwa katika mito na fukwe za bahari na mito na Serikali kuptitua Wizara ya Mambo ya Ndani, Waziri Mwigulu Nchemba anajibu bila shaka hao maiti ni wahamiaji haramu. Napata shaka dunia itatuelewaje Watanzania? Je, wahamiaji hawatakiwi au tumepitisha sheria ya kuwaua hao wahamiaji haramu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri Mheshimiwa Dkt. Mahiga alijibu Bunge na kutoa tafsiri sahihi kwa kuwa badala yake Watanzania waishio nje ya nchi (*Diasporas*) wanaweza kudhuriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania waliofungwa nje; katika nchi nyingi duniani, Watanzania katika kutafuta maisha, wanapatikana na hatia mbalimbali kama vile:-

(a) Kuishi bila ya "Permit" au "overstay" baada ya VISA kuisha na kufungwa magerezani.

(b) Wanaotuhumiwa kujihusisha/kushirikiana na wafanyabiashara wa dawa za kulevyta. Mfano, familia ya Tanga iliyokamatwa China na mtoto wao wa miaka mitatu kurudishwa nchini kutokana na tuhuma za dawa za kulevyta.

(c) Wanaokwenda kutafuta ajira za viwandani, mashambani na majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali, je, Serikali ina mpango gani wa Kidiplomasia wa kubadilishana wafungwa ili warejeshwe Tanzania kuhukumiwa kwa Sheria zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vya Ubalozi tunavyovitelekeza; kwa masikitiko makubwa, natoa hoja hii nikiwa bado nashangaa kuwa Serikali ya Kifalme ya Oman imetupa Kiwanja "*Low Density*" huko Muscat, lakini mpaka leo tumeshindwa kukijenga. Nashauri Serikali itafute fedha na kujenga na kuondoa aibu hii inayochafua Taifa letu.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefikia wapi juu ya suala la mpaka eneo la Ziwa Nyasa baina ya nchi yetu na Jamhuri ya Malawi. Suala hili limekuwa ni la muda mrefu sana na hakuna ufumbuzi uliofikiwa juu ya suala hili la mpaka. Naomba kufahamu suala hili limefikia wapi? Naomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha mjadala tupate ufanuzi wa kina juu ya mahali walipofikia katika maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Ludewa ambayo imepakana kwa eneo kubwa na nchi ya Malawi kuliko Wilaya za Kyela na Nyasa lakini hatuna *customs* ambazo zingerahisisha kwa watu wanaosafiri kwenda Malawi badala ya kupitia Kyela ambako ni mbali na kunaleta usumbufo mkubwa kwa wananchi wanaotaka kusafiri kibashara na kushindwa kulitumia soko la nchi jirani. Wilaya ya Ludewa ni eneo zuri kwa uzalishaji wa mazao ya biashara

kama mahindi, maharage, chai, pareto, alizeti na kadhalika. Kuna umuhimu wa kuwa na bandari na *TRA* kurahisisha mienendo ya watu na bidhaa.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara, Mabalozi wetu wote wanaowakilisha Tanzania kwa jitihada kubwa ya kuitangaza nchi yetu pamoja na kuitafutia misaada mbalimbali kwa maendeleo ya nchi yetu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango na ushauri:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ipelekewe fedha kwa wakati ili kutekeleza majukumu yake kwa muda muafaka. Pia fedha za maendeleo ziongezwe ili kutekeleza miradi mingi ambayo inahitajika kwa muda huu na baadaye kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ya Muungano ijenge jengo jipya la Ofisi ya Mambo ya Nje huko Zanzibar. Serikali iombe kiwanja kwa SMZ na ijenge jengo jipya na la kisasa kulingana na kazi na mahitaji husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iendelee na juhudzi za kuwatafutia ajira vijana wa Tanzania nchi za nje na Taasisi nyingine za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania waishio nchi za nje ambao wamepata mafanikio na maendeleo makubwa, wahamasishwe zaidi kuja kuwekeza nchini kwao Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Balozi zetu ziongezewe fedha ili kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itenye fedha kwa madhumuni ya kufanya matengenezo Balozi zetu nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga Mkono hoja. Nawatachia utekelezaji mwema wa majukumu ya kazi na kulitumikia Taifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara hii muhimu niwatakie masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Israel, sera yetu ya mambo ya nje siku na katika Awamu zote Nne zilizotangulia, zilikuwa rafiki wa kweli wa Israel na Palestine. Awamu ya Tano imefungua Ubalozi kwa mbwembwe zote Israel. Je, wanajua mlivyoikwaza *the Arab World!*

Mheshimiwa Naibu Spika, Morocco/*Western Sahara*, awamu hii imefungua Ubalozi Algeria. Hii ni sawa, lakini wakati huo huo wanafunga ndoa ya rafiki na unafiki na Morocco. Algeria ndiyo mtetezi wa Sahara Magharibi. Mbinu zetu za ukombozi zimeishia wapi? Morocco ilikuja mwaka jana na kuweka mikataba 21, iko wapi sasa? Waziri atueleze mikataba yote imefika wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua hamna kitu, Mfalme wa Morocco alikuja kwa nia ya kuishawishi Serikali iunge mkono azimio la ombi la Morocco kurejea AU na siyo vinginevyo. Mengine yote yalikuwa danganya toto. Mbaya zaidi ukikutana na watu wa Morocco utasikia Dkt. Mahiga mtu wetu, Dkt. Mahiga mtu wetu. Sasa hapa ni Dkt. Mahiga au ni Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki hafifu wa nchi katika mikutano ya kimataifa na kimkakati. Safari za nje kwa Mheshimiwa Rais kuzikatisha amechemsha, Watanzania sasa lazima tumlazimishe Mheshimiwa Rais kuhudhuria mikutano muhimu. Mwaka huu tumlazamishe aende *UN* akahutubie Umoja wa Mataifa tufurahi kwa kuwakilisha nchi yetu na kupata fursa mbalimbali. Haiwezekani Mheshimiwa Rais awe ametembelea Rwanda na Uganda tu miaka yote hii, tukiuliza tunaambiwa ni kubana matumizi, hapana! Siyo kweli. Ikulu na Wizara ituambie tu ukweli, kuna tatizo gani? Je ni lugha? Kama ni lugha si atumie Kiswahili tu kwanza atakuwa

anakuza na kuitangaza lugha yetu. Je, ni afya? Je, ni usalama wake anahofia au ni majukumu? Katika haya yote sioni sababu labda kama ni ya kiafya.

Mheshimiwa Naibu Spika, msiba wa Winnie Mandela, kwenye msiba huu katika nchi yenye mahusiano mazuri ni sisi tangu enzi hizo hatukuweza kupeleka mwakilishi. Ajabu nchi zote za *SADC* zilituma wawakilishi, sisi Tanzania hatukwenda! Hii ni aibu sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kuna *economic diplomacy* tena nchini? Ipi! Hakuna *economic diplomacy*, sasa kuna diplomasia ya miundombinu tu, ambayo ni diplomasia ya barabara na *Bombadier*!

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi amesikika akisema kuwa kwenye vikao mbalimbali inapofika zamu ya Tanzania kuongea basi watu wote walikuwa wanaacha kwenda hata chooni, walikuwa na shauku ya kusikiliza. Sasa ni kinyume chake, sasa hawana shauku na kwa kweli hakuna cha kusikiliza. Tumefika hapo? *We are a laughing stock! Gone are the good days.* Inachosha sana leo Bungeni tumeshangilia nafasi walizopata wenzetu kwenye Bunge la Africa (*PAP*). Tumeshuhudia si Mheshimiwa Rais tu haudhurii bali hata Mawaziri na mbaya zaidi Wabunge katika mikutano ya jimbo ambayo ni *calendar meeting*, hii sio sawa.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Ofisi za Balozi zetu, nashauri Serikali kujenga Ofisi zake katika Balozi zetu kwani fedha nyingi zinatumika kugharamia Ofisi hizi wakati kuna viwanja. Mfano, Msumbiji kuna eneo la kujenga na tunashindwa kujenga. Tukope hata mikopo ya masharti nafuu ili ije ilipwe kwa fedha zile ambazo tungelipa kodi ya majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uteuzi wa Mabalozi; nashauri Serikali kuangalia uteuzi unaofanyika kama unaendana na

faida tunazopata kutokana na uwekezaji huo katika Balozi hizo. Ni kwa kiasi gani upimaji wa utendaji wa Balozi zetu ukichukulia kuwa kuna malengo mahususi ya uanzishaji Balozi hizo ikiwa ni pamoja na kutangaza vivutio vyta Tanzania ili kuwezesha Tanzania kupata wawekezaji.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kurejesha Wafungwa Nchini; naomba Wizara ishughulikie kurudisha Watanzania waliofungwa huko nje, kama vile Msumbiji, warejeshwe nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanajeshi Wanaofariki Kwenye Mapambano; kuna Wanajeshi wanaokwenda kusaldia nchi nydingine kwa ajili ya ulinzi kama vile Congo na sehemu nydingine, wanapofariki kwenye mapambano hayo familia zao zinasahaulika. Naiomba Serikali ihakikishe familia za Wanajeshi hao zinapata huduma stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Unyanyasaji wa Mabinti Wanaokwenda Kufanya Kazi za Majumbani Nje; naiomba Serikali ifuatilie wale wote wanaowasafirisha mabinti kwenda nje kufanya kazi za ndani, wachukuliwe hatua kwa sababu mabinti hao wanateseka sana na wengine wanakufa na hawapati masaada wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upungufu wa Maafisa Kwenye Balozi; Maafisa kwenye Balozi zetu hawatoshi. Naiomba Serikali ijitahidi kupeleka maafisa katika balozi zetu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanja Visivyoendelezwa. Kuna viwanja ambavyo havijaendelezwa basi viendelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kwa kumshukuru Mungu kwa kunifikisha mahali hapa salama ili nami nichangie hotuba hii muhimu

ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ya Mwaka wa Fedha 2018/2019. Naipongeza Wizara pamoja na wataalam wake kwa kuandaa bajeti nzuri. Bajeti hii itatekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi katika kuhakikisha nchi yetu inaimarisha ushirikiano na mahusiano mazuri na mataifa mengine duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa juhudhi mbalimbali inazochukua katika kuimarisha mahusiano yetu na mataifa mbalimbali duniani, ni hatua nzuri na ya kupongezwa, hatua hiyo italiwezesha Taifa kufaidika na masuala mbalimbali ya kimaendeleo na mataifa hayo. Juhudi hizo zitasaidia pia kulitangaza Taifa letu na kuvitangaza vivutio vyetu na kuvutia watalii, wawekezaji kuja nchini kuangalia fursa mbalimbali tulizokuwa nazo za kiuwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kufungua ubalozi mpya nchini Israel ni ya kupongezwa. Taifa hilo limepiga hatua kubwa kimaendeleo, uchumi, viwanda na teknolojia. Ubalozi huo utatuweka karibu, kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo. Naishauri Serikali kuitia Wizara hii kuwakumbusha Mabalozi wetu wote wanaotuwakilisha katika nchi mbalimbali, kutumia fursa hiyo kuvitangaza vivutio vya kitalii tulivyo navyo na fursa mbalimbali za kiuwekezaji zilizopo nchini, hatua hiyo itasaidia sana kunufaika kama nchi kwa sekta husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wetu wa Afrika Mashariki unazidi kuimarika na kuleta taswira nzuri ya kimaendeleo. Watu wetu wanaendelea kufaidika na ushirikiano huo kwa kiasi kikubwa, wafanyabiashara wetu wanavuka mipaka na kushirikiana na wenzao katika biashara mbalimbali. Hii ndiyo dhana ya ushirikiano huu ambaa una tija kwa kila Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hazikosekani, hivyo naishauri Serikali kuziangalia kwa jicho la pekee changamoto zote na kuzipatia ufumbuzi ambao utaleta malengo chanya kwa mataifa yote wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu ambayo ni kioo cha nchi yetu katika uso wa kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na ukarimu kwa kuendelea kutupa ruhusa ya kupumua pamoja na maudhi tunayomfanya kama binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo naanza na mchango wangu kwa kujielekeza hasa katika ukurasa wa 14; kuhusu Diplomasia ya Uchumi. Tanzania tunategemea kilimo kwa chakula, ajira, biashara na malighafi, lakini tatizo kubwa ni masoko ya uhakika na yenye bei nzuri na tija kwa wakulima wetu. Kwa mfano, zao la mbaazi kukosa soko mwaka jana 2017/2018 na bei yake kuanguka kutoka 2,000 ya mwaka 2016/2017 na kufikia 150 kwa kilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imeathiri uchumi wa Taifa na kipato cha wakulima wetu na kusababisha hasara kubwa. Pia imeleta madeni katika taasisi za fedha zikiwemo benki na *SACCOS* ambako waliwalichukua mikopo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mbaazi kuzingatia bei nzuri na ushindani wa soko kwa msimu wa mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina ardhi kubwa na faida ya kijigrafia katika mikoa mingi katika uzalishaji wa mbaazi ikiwemo Morogoro, hasa Morogoro Vijiji, Kilosa, Turiani na Ifakara na mikoa mingine kama Arusha, Manyara, Shinyanga, Pwani, Lindi na MtWARA ambayo ilikuwa inatoa ajira, chakula na kuongeza vipato vya watu wetu; ukizingatia kwamba zao hili la mbaazi kilimo chake hakina gharama kubwa na usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao hili si la kupuuza na kuliacha kwa sababu lina fursa nyingi za kiuchumi, lakini tatizo

kubwa ni soko lake, kwamba linategemea jamii moja tu na sehemu moja ambayo ni India. Kutokana na kutegemea soko moja wakulima wetu wanaathirika zaidi kwa sababu mabadiliko yoyote ya sera ya soko hilo au uzalishaji mzuri wa mbaazi wa India kunaathiri soko la mbaazi la wakulima wetu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri katika Wizara hii katika Diplomasia ya Uchumi kutafuta soko la mbaazi kabla ya msimu kuanza katika nchi ya India na hasa mnunuzi mkuu ambaye ni Serikai ya India ili kuwa na uhakika wa soko na bei nzuri kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuishauri Serikali kuingia mkataba wa ununuzi na Serikali ya India kutoka kwetu kwa bei ya kiasi ili kutumia vizuri Diplomasia ya Uchumi na kuongeza fedha za kigeni na kipato kwa wakulima na kuepuka hasara kama mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote kwa kutayarisha na kuwasilisha kwa umakini mkubwa hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kutoa mchango wangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwakilishi wa Tanzania katika Mabunge ya Nje. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wetu waliopata nafasi ya kuteuliwa katika nafasi kwenye Bunge la Afrika. Wabunge hawa wameonesha uwezo mkubwa katika nyanja za kimataifa na kuonesha kuwa Tanzania tunao watu ambao wanaweza katika maeneo ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matokeo hayo ya kihistoria yaliyopatikana bado juhudzi za uwakilishi wa nchi yetu katika Mabunge hayaridhishi kidogo. Bado kunakosekana uwakilishi katika Mabunge kadhaa kwenye mikutano ya Mabunge. Najua kuwa hali ya uchumi wa nchi yetu bado hajatengemaa vizuri, lakini naiomba Serikali kulipa umuhimu wa kipekee jambo hili la uwakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utafutaji wa Misaada kwa Ajili ya Miradi ya Maendeleo. Napenda kuipongeza Serikali yetu kuititia Wizara hii kwa namna wanavyochukua juhudzi za kutafuta misaada kwa wafadhili kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Jambo la kutafuta misaada ni jambo la kawaida kwa nchi nyingi ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika jambo hili ni kwamba, ni vyema Wizara ikawa na wafanyakazi wenye ujuzi wa aina zote hasa za mikataba ya miradi hiyo pamoja na biashara. Hii itatuepusha na ujanja wa mitego ya kisheria za mikataba ambayo mara nyingi baadhi ya wafadhili huwa wanaitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya Utumishi Wizarani. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni Wizara ya Muungano wa pande mbili za Tanganyika na Zanzibar. Wizara imekuwa ikilalamikiwa kwa kutotenda haki kwenye masuala ya utumishi ndani ya Wizara. Watumishi walio wengi ni wa upande mmoja wa Muungano. Wakati Wazanzibari wanapohoji Mawaziri wenye dhamana huwa wanatoa hoja ya kuwa utumishi huhitaji weledi na vigezo. Je, Wazanzibari wamekosa sifa hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (A/ICC). Wakati A/ICC inatimiza karibu miaka 40 tangu kuanzishwa kwake, kimekuwa kikifanya uwekezaji mkubwa upande wa Tanzania Bara pekee. Pamoja na

miradi hiyo iliyopo sasa hivi AICC bado ina malengo ya kujenga kituo kikubwa cha mikutano cha Mt. Kilimanjaro *International Convention Center* nyingine katika eneo la Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mazingira ya uwekezaji kwa shughuli za AICC yaliyoko yanaruhusu, ni sababu zipi zilizofanya Wizara isifanye uwekezaji katika Visiwa vya Zanzibar? AICC kutowekeza Zanzibar ni kuwanyima Wazanzibari fursa za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutafuta Wawekezaji Nje ya Nchi. Miiongoni mwa kazi ya Wizara ni kusimamia balozi zetu katika kutafuta wawekezaji, fursa za ajira, nafasi za masomo kwa bidhaa zetu. Wawekezaji wengi kutoka nje ya nchi wamekuwa wakija kuwekeza hapa nchini lakini kwa bahati mbaya wanaishila Tanzania Bara pekee. Ni kwa nini Wizara hii haiwaongozi wawekezaji kutoka nje kuwekeza katika visiwa vya Zanzibar kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa visiwa hivyo ambao unadorora? Niombe Wizara isifanye upendeleo katika kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Changamoto za Utawala Bora Zilizobainishwa na APRM. APRM inaanini kwamba Tanzania ina tatizo la kutozingatia utawala bora na unaokubalika kwa wananchi wake. Hii imetokana hasa pale Tanzania inapominya uhuru wa Wazanzibari wa kuiweka madarakani Serikali wanayoitaka wenyewe. Serikali ya Zanzibar iliyopo madarakani sasa hivi si chaguo la wananchi wa Zanzibar, ni Serikali iliyowekwa kwa nguvu za dola, hivyo basi Serikali hii si halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itoe ripoti kwa APRM kwamba Tanzania haiwezi Mfumo wa Vyama Vingi kwa sababu Chama cha Mapinduzi hakiko tayari kukabidhi madaraka pale wanaposhindwa kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia upande wa Serikali na tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba dakika tano, Mheshimiwa Balozi ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima na kuweza kusimama mbele yako na kuchangia katika hoja hii ambayo Waziri wangu ameiwasilisha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii ya kipekee kama wenzangu walionitangulia kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake madhubuti. Vilevile nimpongeze pia Waziri wangu ambaye nafanya naye kazi kwa karibu kwa kazi nzuri anayoifanya kuitetea Tanzania kuisemea, kujenga mahusiano kati ya nchi mbalimbali na kuhakikisha kwamba diplomasia ya kiuchumi inatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kwa sababu ya muda nimshukuru kwa namna ya kipekee mume wangu mpendwa Dkt. George Ayeso Mrikalia kwa uvumilivu wao kwangu pamoja na familia yangu watoto wawili wanajua kwamba nimepewa kazi na mimi nimekubali, tutapambana mpaka kieleweke. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda naomba niende moja kwa moja kwenye hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge najua kwamba hatutaweza kuzijibu hoja zote, lakini tunaahidi kwamba kwa niaba ya Wizara tutaweza kuzijibu kwa maandishi na kuzikabidhi kwao. Nikienda kwenye hoja ambazo zilikuwa zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge hasa kwenye Kamati nitajibu tu baadhi ya hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna suala la Kamati kutushauri kuhusu kuandaa sera ya Taifa ya *diaspora*. Nasema kwamba Wizara imeunda timu mahususi ili kufanikisha uandaaji wa sera hii ya Taifa ya *diaspora*

itakayoainisha mikakati na kutoa mwongozo kuhusu ushiriki wa *diaspora* katika kuchangia maendeleo ya nchi. Timu hiyo tayari imekwishaanza hatua za awali za maandalizi ya sera hiyo. Pia Wizara imetenga fedha kwa mwaka huu kwenye bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa ajili ya zoezi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu kuongeza kasi ya kukamilisha mchakato wa sera mpya yaani *Revise Foreign Policy*, niseme tu kwamba Wizara imekamilisha kuandaa rasimu ya Sera hiyo Mpya ya Mambo ya Nje ya Tanzania, lakini hatua inayofuata sasa ni kuandaa mkakati wa utekelezaji ambao pamoja na rasimu ya sera hiyo vitawasilishwa kwa wadau kwa maana ya Serikali na sekta binafsi ili kupata maoni yao na Wizara imetenga fedha kwa ajili ya zoezi hili ya bajeti ya 2018/2019 kwa ajili ya kukamilisha sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruke kidogo niende kwa Mheshimiwa Masoud ambaye alizungumzia kuhusu wale wafungwa 11 ambao wako kwenye gereza lile la BEO kule Msumbiji niseme tu nimeshakwisha wasiliana na Mbunge wao ambaye alikuwa anafuatilia hilo na tumewasiliana na Balozi wetu kule Msumbiji. Alimtuma Afisa kwenda kuangalia wiki mbili zilizopita, pia juzi alienda ye ye mwenyewe na anasema tu kwamba anasubiria taratibu za kimahakama watakavyomaliza *process* za kuandaa kila kitu tutakuwa tunaendelea kumtaarifu Mbunge husika na kuhakikisha kwamba maslahi ya wale Watanzania yanalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Masoud kwa kuhakikisha kwamba anafuatilia masuala ya Watanzania wakiwemo Watanzania ambao ye ye ni Mbunge wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikienda kwenye suala lingine ambalo pia limetolewa na Kamati kwa kushauri Wizara ambalo linahusu kuhusu upatikanaji wa fedha za ujenzi wa majengo ya ubalozi na makazi katika Balozi zetu. Suala hili limekwishaongeleta sana kwenye hotuba ya

Mheshimiwa Waziri na mikakati tuliyokuwa nayo mkakati wa kwanza wa miaka 15 ambao ulikuwa ulioanza mwaka wa fedha 2002/2003 mpaka mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sasa hivi tumetengeneza mkakati mpya ambapo tumejaribu kuangalia kuhakikisha kwamba suala la kutengeneza mkakati wa upatikanaji wa fedha na ujenzi pamoja na ukarabati wa Balozi zetu zilizoko nje unafanyika kwa haraka iwezekanavyo. Tutaendelea kulisimamia hilo na kufuatilia kwenye Wizara ya Fedha na kwa vile Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje ni Serikali basi nadhani Mungu atatusaidia na tutaweza kufikia mahali pazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie uwezekano wa kuziruhusu Balozi kubakiza angalau asilimia 40 ya makusanyo kwa maana ya maduhuli ili ziwezeshe kutekeleza majukumu yao kwenye Balozi husika; hili suala ni la kanuni na sheria. Tutajaribu kuangalia kukaa pamoja na Wizara ya Fedha na kupata ushauri wao wa kitaalam na kama sheria zitakuwa zinaruhusu basi sisi tuko tayari kupokea ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni wasikivu kama mnavyoona, tumetekeleza yale ambayo tumefanya, mmesema tufungue *Counsel* tumefungua, mmesema tufungue Balozi Cuba, tumefungua; lakini mmesema kwamba tuhakikishe jengo letu la Maputo linajengwa na kukarabatiwa na watu wanahamia, tumefanya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa sekunde 30, muda wako umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja ya Waziri wangu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Mahiga, mtoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie muda uliobakia kujibu baadhi ya maswali ambayo nimeyasikia kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ni lile linalohusu haki za Wapalestina na watu wa *Western Sahara*. Katika hotuba yangu nimesema misingi ya Tanzania katika Jumuiya ya Kimatifa ni kuheshimika, kuthamini utu na kulinda uhuru. Kama hilo ndio letu inafuata kwamba wale ambao wamenyimwa uhuru, wamenyimwa utu, lazima washughulikiwe na wapate haki zao. Sasa sisi kama Tanzania lazima tufanye mambo matatu; la kwanza, tutambue kutokuwepo kwa haki hizo kwa watu huku duniani maana yake kama tunalitaka sisi na tunataka wenzetu wapate na hilo hatuwezi kuliacha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sisi wenyewe Tanzania tumesema ili hilo lipatikane lazima iwe ni diplomasia ya siasa na diplomasia ya siasa kusaidia nchi moja au nyingine inapatikana kwenye majukwaa ya kimataifa. Utazungumzia uhuru na haki na heshima ya Wapalestina au ya *Western Sahara* kwenye majukwaa muda umepita. Wakati ambapo kutetea haki za Afrika Kusini au Msumbiji au Namibia tulisema tutatumia silaha hatutumii silaha tena, tunasema tutaongea na moja ya silaha zetu ni kwamba tutashiriki kikamilifu katika mijadala ya kimataifa katika majukwaa mbalimbali kuhusu suala la Palestina na suala la *POLISARIO*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati huo huo tuna diplomasia ya uchumi; wagomvi wa Palestina ni wa Israeli. Sasa hawa wa Israeli katika diplomasia ya uchumi kuna vitu pale tunaweza kuvipata na sisi tumesema hayo yanayozungumza kuhusu haki za wa Palestina tuyapeleke kwenye vikao, majukwaa ya kimataifa, Tanzania ni peke yake ilikuwa nchi ya kwanza kuipa Palestina *diplomatic status* hakuna nchi nyingine. Hiyo baada ya Mwalimu Arafati ondoa majeshi yako Uganda alipoondo majeshi Uganda wakati wa vita akasema tutawapa *diplomatic status*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni watu wa kwanza na nilifanya makusudi kwamba Trump anapokwenda kufungua Jerusalem mimi nafungua Tel Aviv kwa sababu hilo ni kutambua kwamba Jerusalem ni mji wa utata. Nilipokwenda kule kwa makusudi nilisema nipelekeni Gaza Strip pale kwenye kivuko nikaona pale na nimewaambia Waisrael kimacho macho nikasema *this is a time bomb* lazima muishughulikie suala hili tulizungumze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *resolutions* 12 za Umoja wa Mataifa kuhusu Palestina na kuhusu Israeli nimewaambia pande zote mbili na umoja wa Mataifa wanakubali kwamba tukae tutazame kwamba kuna *resolution* nyingine zimepitwa na wakati na tufanye zoezi hilo tutazame lakini hatutaweza kuacha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kabwe leo katika hotuba yangu nimeanza na aya inayosema *POLISARIO* na imeishia maneno ya *POLISARIO* sijawasahau. Ni kweli kwamba suala hili linazungumzwa mbele ya Umoja wa Mataifa, lakini maadam tumewaambia Morocco warudi ndani ya Afrika suala hili litaongezewa tija zaidi kama pia Afrika itachangia. Nadhani suala hili sio rahisi kihivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, wakati huo huo Morocco ni nchi yenye uchumi mkubwa ya tano ndani ya Afrika, sio uwanja tu wa ndege au uwanja wa mpira au *stadium*, lakini kuna maeneo hasa katika diplomasia ya kutengeneza mbolea na utalaam na mafunzo ambavyo tunaweza kupata. Hiyo haitatuzuia katika majukwaa yote Afrika *and non-aligned countries* au Umoja wa Mataifa kuwaambia jamani hili suala tulishughulikie kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la diplomasia ya uchumi uliojikita kwenye viwanda ili uwe na viwanda na vinyoyofanya kazi kuna mambo manne muhimu. La kwanza, ni mtaji lazima kupata *investors* tupate pesa, kama zinatoka hapa au zinatoka nje. La pili, huwezi kuwa na viwanda kama huna *energy*, nishati ya kutosha, huwezi kuwa na viwanda

kama huna miundombinu mizuri na huwezi kuwa na viwanda kama huna wataalam wanaoshika ule umeme na kufunga na kufungua wale watalii wataalam na hatimaye lazima uwe na soko. Sisi katika kuandaa vijana wetu tumesema hayo unapokwenda kule, hayo ndio uyafuate matano utafute pesa, mtafute wawekezaji, kwenye miundombinu, mtafute watakaoshiriki katika nishati, watakaoweza kutoa mafunzo na masoko ambayo lazima tuwe nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili linaingia katika kutayarisha vijana wetu wanaokwenda nje kwa miaka miwili tumekuwa tunarudisha watu kuna wengine walikuwa wanakaa miezi na miezi, miaka na miaka hawarudi, tumehekikisha kwamba Balozi zote zinatazamwa na tunarudisha watu. Kurudisha watu ni fedha nyingi sana, tumerudisha 109 katika miaka miwili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaandaa kupeleka vijana ambaa wanafanana na haya matano niliyoyasema. Tayari tumeshawatambua na sasa hivi tuko katika ngazi ya upekuzi, lazima wapekuliwe na vyombo vinavyohusika kabla hatujawapeleka. Natumaini hela nitakayopata kutoka bajeti hii ndio itakayotumika kuwapeleka vijana katika vituo vyote. Wote majina yao tumeshayaandaa na tunasubiri wapate kibali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wa Mataifa ulizaliwa mwaka 1945, leo una wanachama 193. Katika 193 chombo chenye nguvu kupita vyote ni Baraza la Usalama na Baraza la Usalama lina watu wa kudumu Mataifa matano Marekani, Uingereza, Ufaransa, Urusi na China. China isingeingia *Security Council* bila Tanzania, kabla ya mwaka 70 China ilikuwa inawakilishwa na Taiwan au **Formosa au Sheing Tang Sheing** lakini sisi Mwalimu akasema haiwezi kuwa Umoja wa Mataifa bila China. Hivyo ikarudi na ndio tuliiweka kule kwenye *Security Council*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mageuzi ya mwisho yalifanyika mwaka 1963 kuongeza Baraza la Usalama kutoka tisa kufika 15, tangu mwaka 1963 hakujawa na

mabadiliko. Sasa kuna aina nydingine ya mabadilko, kuna wale wanaosema tuingie na tupewe turufu na hao ni wakubwa Japan, Brazil, German...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri dakika moja umalizie.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa basi ni kwamba hayo mageuzi Afrika nayo inadai ipewe haki kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa mchango wao. Maswali mengi nimeyapata na mengi tutayajibu kwa maandishi na haya yataleta tija sana katika kuboresha, kuna mengine ambayo lazima niseme wazi hatuwezi kuyafanya bila nyinyi kutusaldia kuititisha bajeti hii ili tuweze kuendeleza vizuri zaidi kwa pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

Kif.1001- *Administration and HRM*.....Sh.23,914,247,000/=

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni ya 104(1) naongeza nusu saa. Sasa nitawahoji, kuhusu kifungu kilichotajwa hapo juu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

kif. 1002 - *Finance and accounts* .....Sh.993,726,000/=  
Kif. 1003 – *Foreign affairs office Zanzibar*.....Sh.840,334,000/=  
Kif. 1004 – *Policy and Planning* .....Sh.1,332,414,000/=  
Kif. 1005 – *International Cooperation*.....Sh.1,000,950,000/=  
Kif. 1006 – *Europe and America* .....Sh.667,956,000/=  
Kif. 1007 – *Asia and Australia* .....Sh.703,969,000/=  
Kif. 1008 – *Africa* .....Sh.1,889,751,000/=  
Kif. 1009 – *Regional cooperation* .....Sh.766,223,000/=  
Kif. 1010 – *Protocol* .....Sh.8,557,024,000/=  
Kif. 1011 – *Legal service*.....Sh.2,175,611,000/=  
Kif. 1012 – *Government communication unit*Sh.464,403,000/=  
Kif. 1013 – *Middle East Division* .....Sh.567,591,000/=  
Kif. 1014 – *International audit unit*.....Sh.403,640,000/=  
Kif. 1015 – *Procurement management Unit*...Sh.649,580,000/=  
Kif. 1016 - *Information and Com. Technology*Sh.418,139,000/=  
Kif. 1017 - *Diaspora Engagement and Opportunity*.....Sh.618,397,000/=  
Kif. 1018 – *Economic Infrastructure and Social Support Service*.....Sh.759,689,000/=  
Kif. 1019 – *Political defense and Sec. Affairs*....Sh.687,626,000/=  
Kif. 1020 – *Trade investment and productive sector division*.....Sh.707,658,000/=  
Kif. 1021 – *Embassy of Tanzania – Addis Ababa*.....Sh.2,632,428,000/=  
Kif 2002 - *Embassy of Tanzania Berlin*.....Sh.3,414,752,000/=  
Kif. 2003 – *Embassy of Tanzania – Cairo*.....Sh.1,648,331,000/=  
Kif. 2004 – *Embassy of Tanzania- Kinshasa* ..Sh.1,955,480,000/=  
Kif. 2005 – *High Commission of Tanzania – Abuja* Sh.....2,698,660,000/=  
Kif. 2006 – *High comm. of TZ – London*.....Sh.3,792,141,000/=  
Kif. 2007 – *High Comm. of TZ – Lusaka*.....Sh.1,420,114,000/=  
Kif. 2008 – *High Comm. of TZ – Maputo*.....Sh.1,625,383,000/=  
Kif. 2009 – *Embassy of Tanzania–Moscow*....Sh.3,359,266,000/=

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kif. 2010 – *High Commission of TZ-*  
*New Delhi*.....Sh.2,999,406,000/=

Kif. 2011 – *Permanent Mission to the*  
*UN – New York*..... Sh.5,399,267,000/=

Kif. 2012 – *High Comm. of TZ-Ottawa*.....Sh.2,652,964,000/=

Kif. 2013 – *Embassy of Tanzania -Paris* .....Sh.3,027,266,000/=

Kif. 2014 – *Embassy of Tanzania Beijing* .....Sh.3,428,158,000/=

Kif. 2015 – *Embassy of Tanzania -Rome*.....Sh.4,175,232,000/=

Kif. 2016 – *Embassy of Tanzania –*  
*Stockholm*.....Sh.3,596,012,000/=

Kif. 2017 – *Embassy of Tanzania – Tokyo*..... Sh.3,133,070,000/=

Kif. 2018 – *Embassy of Tanzania –*  
*Washington*..... Sh.4,414,961,000/=

Kif. 2019 – *Embassy of Tanzania – Brussels*....Sh.2,999,051,000/=

Kif. 2020 – *Permanent Mission to the*  
*UN-GENEVA*.....Sh.6,146,258,000/=

Kif. 2021 – *High Commission of Tanzania –*  
*Kampala*.....Sh.2,309,551,000/=

Kif. 2022 - *High Commission of Tanzania –*  
*Harare*.....Sh.1,673,975,000/=

Kif. 2023 – *High Commission of Tanzania –*  
*Nairobi*.....Sh.4,486,684,000/=

Kif. 2024 - *Embassy of Tanzania Riyadh* ..... Sh.3,099,463,000/=

Kif. 2025 - *High Commission of Tanzania –*  
*Pretoria*.....Sh.3,215,352,000/=

Kif. 2026 - *Embassy of Tanzania- Kigali* .....Sh.2,047,230,000/=

Kif. 2027 - *Embassy of Tanzania- Abudhabi*.Sh.3,450,132,000/=

Kif. 2028 - *Embassy of Tanz. - Bujumbura*.....Sh.1,718,702,000/=

Kif. 2029 - *Embassy of Tanzania- Muscat*.... Sh.2,627,554,000/=

Kif. 2030 - *High Commission of Tanzania –*  
*Lilongwe*.....Sh.1,549,824,000/=

Kif. 2031- *Embassy of Tanzania- Brasilia* .....Sh.3,404,104,000/=

Kif. 2032- *High Commission of Tanzania –*  
*Kuala Lumpur*..... Sh.2,179,889,000/=

Kif. 2033 - *Embassy of Tanzania- The Hague* Sh.2,963,353,000/=

Kif. 2034 - *Embassy of Tanzania- Morocco*...Sh.1,893,979,000/=

Kif. 2035 - *Embassy of Tanzania- Kuwait*.....Sh.1,567,422,000/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, aliyewasha *mic*, azime.

Kif. 2036 - *Embassy of Tanzania- Algiers*....Sh.2,402,105,000/=  
Kif. 2037 - *Embassy of Tanzania- Ankara*.....Sh.2,531,037,000/=  
Kif. 2038 - *Embassy of Tanz. - Khartoum*.....Sh.2,114,141,000/=  
Kif. 2039 - *Embassy of Tanzania- Seoul*..... Sh.4,092,976,000/=  
Kif. 2040 - *Embassy of Tanzania- Tel-Aviv*.....Sh.2,620,398,000/=  
Kif. 2041 - *Embassy of Tanzania- Doha*.....Sh.2,100,178,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

Kif. 1004- *Policy and Planning*..... Tsh.10,400,000,000  
Kif. 2010- *High Commission of Tanzania – New Delhi* ..... 0

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

(*Bunge lilitrudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae, mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia

mapendekezo ya bajeti ya Wizara na kuyapitisha. Sasa naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono sasa kwa mujibu wa utaratibu wetu sasa nitawahoji. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2018/2019 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nichukue fursa hii kwanza kuwapongeza sana Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kuweza kutuletea kama Bunge makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 lakini pia wataalam ambao mmefanya nao kazi. Tuipongeze pia Kamati yetu ya Bunge ambayo imefanya kazi nzuri imetuletea, mapendelekezo mazuri na pia imeonesha namna gani Wizara inashirikiana na Kamati hii katika kusikiliza ushauri ambao Bunge linatoa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo, nichukue fursa hii kuwashukuru sana Kamati kwa niaba ya Bunge kwa kazi nzuri mlioifanya. Pia Waheshimiwa Wabunge walipopata fursa ya kuchangia kwa maandishi na kwa kuzungumza humu ndani, Waziri na Naibu wake wameahidi hoja hizo zitajibowi. Kwa hiyo, naamini kwamba itatuweka mahali pazuri kwa kuweza kuisimamia vizuri hii Wizara hii ili iweze kufanya vizuri katika Nyanja za kimataifa, lakini hata hapa nchini kwenye suala la diplomasia.

Waheshimiwa Wabunge, badala ya kuyasema hayo, ninayo taarifa ya Mheshimiwa Selasini anataka kuomba mwongozo halafu nitaleta matangazo kabla hatujamaliza. Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru Bunge hili lilifanya uchaguzi wa wawakilishi wetu katika Bunge la Afrika na kama tulivyosikia ni kwamba wenzetu wawili wamechaguliwa kuongoza katika nafasi mbili tofauti na kubwa katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, Bunge hili tumewashangilia kwa nguvu wenzetu kwa sababu wameliletea sifa Bunge na nchi. Hata hivyo, Wabunge wote wanne wamekuwa wakijitegemea katika kufanya shughuli zao, wamekuwa hawapatiwi tiketi, hawapatiwi fedha kwa namna yoyote. Kazi hili waliyofanya wameifanya kwa nguvu zao. Naomba mwongozo wako kama kweli hawa tunawahitaji kutuwakilisha kama Bunge la Taifa, ni kwa nini Bunge linashindwa kuwahudumia ili waweze kufanya kazi kikamilifu?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka Mheshimiwa Spika alipata kueleza kwa kirefu jambo hili hapa Bungeni na sina lengo la kurudia maelezo aliyokuwa ameyatoa kuhusu jambo hili. Mheshimiwa Selasini ameomba mwongozo huo kuhusu wenzetu Wabunge wa Bunge la Afrika na yale ambayo Waheshimiwa Wabunge tumepata fursa leo ya kushangilia ushindi wao kwamba wanajihadumia wakienda kutuwakilisha sisi kama Bunge, lakini pia kama nchi kwenye Bunge la Afrika.

Sasa kwa sababu maelezo mahususi kuhusu jambo hili si kwa Bunge tu la Afrika, lakini jambo hili la ujumla kwa uwakilishi wa wa Wabunge kwenye vyombo vya huko nje, ambavyo huwa vinaenda kutuwakilisisha sisi kama Bunge, lakini pia kama nchi alishalitolea ufanuzi. Huo ndio mwongozo wangu ufanuzi aliota Mheshimiwa Spika unaendelea kuwa hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, nilete kwenu matangazo niliyonayo mezani sasa, Waheshimiwa Wabunge Mwenyekiti wa *TWPG* Mheshimiwa Magreth Sita anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote, kwamba *TWPG* imeandaa hafla ya uchangishaji fedha itakayofanyika hapa Dodoma mwishoni mwa mwezi Juni, 2018 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya mfano katika Majimbo 264 ya uchaguzi nchini.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli hii itawahuisha Waheshimiwa Wabunge wenyewe na Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa mmoja kati ya Viongozi Wakuu wa Nchi hivyo kumeandaliwa burudani mbalimbali ikiwepo maonesho ya mitindo, yaani *fashion show*, vichekesho, kuimba na kucheza mziki katika kunakshi siku hiyo, ikiwa ni sehemu ya kuchangisha fedha.

Pia mwanamitindo maarufu hapa nchini Hadija Mwanamboka atatoa mafunzo hapa Bungeni kwa ajili ya kuwafundisha Waheshimiwa Wabunge miondoko ya jukwaani kimitindo yaani *catwalk*. Hivyo basi, Waheshimiwa Wabunge wote wanawake na wanaume, mnaombwa kushiriki katika burudani hizo, kwa kujiorodhesha katika fomu maalum iliyopo katika meza ya mapokezi lango kuu la kuingilia Bungeni, leo tarehe 23 Mei, 2018 hadi tarehe 24 Mei, 2018 hadi saa nne asubuhi.

Kwa hiyo mnaombwa mpitie hizo fomu Waheshimiwa Wabunge ili mjiorodheshe, kila mtu atashiriki kwenye lipi kati ya hayo. Pengine baadhi yetu tutakuwa tumeshashauriana tutashiriki kwenye lipi kuna wengine ni wazuri katika uchekeshaji, basi nadhani tutashauriana.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine kutoka kwa Mheshimiwa Shally Raymond ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuia ya Mtakatifu Thomas Moore, Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge ambaao ni Wakristo Wakatoliki kwamba mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge kutakuwa na ibada katika ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wengine wote mnakaribishwa kuhudhuria ibada hiyo.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya,  
naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho asubuhi saa tatu  
tarehe 24 Mei, 2018.

*(Saa 7.40 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya  
Alhamis, Tarehe 24 Mei, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*